AFRIKA KUSINI ANGOLA BOTSWANA DENMARK FINLAND ICELAND LESOTHO MALAWI MSUMBIJI NAMIBIA NORWAY SWAZILAND SWEDEN TANZANIA ZAMBIA ZIMBABWE

USHIRIKIANO WA KIKANISA BAINA YA JUMUIA ZA KIKRISTO ULAYA KASKAZINI NA KUSINI MWA AFRIKA



# MwiliMmoja

KITABU CHA KWANZA



## Tafakuri Baina ya Kaskazini na Kusini kuhusu UKIMWI

# MwiliMmoja

KITABU CHA KWANZA

Tafakuri Baina ya Kaskazini na Kusini kuhusu UKIMWI

Mwili Mmoja Kitabu cha 1 kina makusanyo ya mitazamo kuhusu changamoto, kwa ajili ya kanisa na unyanyapaa unaohusiana na UKIMWI.
Mwili Mmoja Kitabu cha 2 kimejikita katika maombi, utaratibu wa ibada, kuabudu na kujifunza Biblia, ikichanganyikana na shuhuda binafsi kutoka kwa watu waishio na UKIMWI. Vitabu vyote (cha Kwanza na cha Pili) vimetolewa katika lugha za Kiingereza, Kireno, Kiswahili na Kinorwejiani.


| | |
|---|---|
| MHARIRI | Elizabeth Knox-Seith, DanChurchAid |
| MRATIBU | Jan Bjarne Sødal, Baraza la Kikristo, Norway |
| BODI YA UHARIRI | Precious Mwewa, Mwandishi wa Labari, Zambia. Mch. Japhet Ndlovu Baraza la Makanisa nchini, Zambia. Mch. Elias Zacarias Massicame, Baraza la Makanisa, Msumbiji. Jan Bjarne Sodal, Baraza la Kikristo, Norway. Mch. Birthe Juel Christensen, DanChurchAid, Denmark. |
| MSHAURI WA NJE | Gillian Paterson |
| WATAFSIRI | George Mwita - CUAHA, Edwin Msiri - Tanzania Development Mates. Ivan Chetwynd (Kiingereza na Kinorwejiani). Melodien na Tony Winch (Kireno) |
| MPIGA PICHA | Ulrik Jantzen, Das Büro, Copenhagen |
| WANAMITINDO | Beauty Chandra na Preben Bakbo Sloth, wanaharakati VVU+ |
| MICHORO YA KITAALAMU | Anne Mousten na Kit Harding |
| MPIGA CHAPA | Jonsson Grafisk, Copenhagen |
| IMETOLEWA NA | Ushirikiano wa Makanisa ya Kaskazini na Kusini (NORDIC-FOCCISA) |
| ISBN | 978-82-7941-030-0 |
| © | Baraza la Kikristo, Norway, post@norkr.no |
| JINA LA AWALI LA KITABU | One Body (Mwili Mmoja) |


Ushirikiano wa NORDIC FOCISSA ni uhusiano wa pamoja baina ya mabaraza ya makanisa kumi na moja ya Kusini mwa Afrika na mabaraza ya makanisa ya nchi za Kaskazini mwa Ulaya.

Ushirikiano wa Makanisa Kusini mwa Afrika na Ulaya Kaskazini (Nordic Foccisa) inato shukrani zake kwa NORAD na DANDA/ DanChurch Aid kwa uhisani wao kuusaidia Mradi huu.

Kitabu hiki si cha kuuza au kutumiwa kwa malengo ya kibiashara. Maandishi yanaweza kunukuliwa au kurudufiwa, ili mradi upendeleo unatolewa kwa mwandishi na mtoaji wa kitabu hiki.


NAKALA ZA TOLEO LA KISWAHILI KITABU CHA KWANZA NA CHA KITABU PILI ZINAWEZA KUAGIZWA KUTOKA:

| | | |
|---|---|---|
| Jumuia ya Kikristo Tanzania | Simu +255 262324445 | email: gs@cct-tz.org |
| Baraza la Kikristo Norway | Simu +47 23081300 | email: post@norkr.no |

NAKALA ZA TOLEO LA KIINGEREZA ZINAWEZA KUAGIZWA TOKA:

| | | |
|---|---|---|
| Baraza la Kikristo Norway | Simu +47 23081300 | email: post@norkr.no |
| Baraza la Makanisa Zambia | Simu 260-1-229551-224622 | email: info@ccz.org.zm |



# Mwili Mmoja

KITABU CHA KWANZA

Tafakuri Baina ya Kaskazini na Kusini kuhusu UKIMWI

- Ujinsia wa Mwanadamu
- Kanisa lenye uvumilivu
- Taswira za Mungu

USHIRIKIANO WA KIKANISA BAINA YA JUMUIA ZA KIKRISTO ULAYA KASKAZINI NA KUSINI MWA AFRIKA

UTANGULIZI
Uthibitisho wa Awali 3
Changamoto ya Unyanyapaa 4

UJINSIA WA MWANADAMU 10
MSUMBIJI Nafasi ya Kanisa Katika Elimu ya Jinsia 12
ZAMBIA Madhambi ya Kidume 14
NORWAY Mwiko Ulio Dhaifu 18
DENMARK Karama ya Mungu na Wajibu wa Mwanadamu 21
DENMARK Ujinsia na Kifo 22

KANISA 28
ZAMBIA Kanisa Linaloponya 30
DENMARK Mwili wa Kristo 34
MSUMBIJI Unyayapaaji 38
NORWAY Pasipo Hofu 40
DENMARK Kuudhibiti Upweke 42

SURA ZA MUNGU 46
NORWAY Utambulisho Wetu Mkuu ni Upendo 48
DENMARK Sura Zilizoharibiwa na Zile Zilizotengenezwa 50
NORWAY Maana na Utambulisho 52
DENMARK Hatia na Msamaha 54
DENMARK Aibu 56
ZAMBIA Rehema za Mungu 58

HITIMISHO
Tumeitwa kuwa Tofauti 62



# Uthibitisho wa Awali

"Mwili Mmoja" ni matokeo ya mazungumzo ya karibu na ya pamoja baina ya wananchi wa nchi nne: Msumbiji, Zambia, Norway na Denmark.

Sote tumeunganishwa na ushirikiano wa Jumuia za Kikristo Ulaya Kaskazini na Kusini mwa Afrika. Kazi yetu ilihamasishwa na mwito wa kustawisha ushirikiano wa kikanisa na wa Kimadhehebu na kuukabili UKIMWI Afrika na popote pengine. Hatua hii yaweza kuchukuliwa kama utekelezaji wa wito wa Baraza Kuu la Makanisa Ulimwenguni (WCC) wa kufanya kazi kwa kuvuka mipaka lakini kwanza kuzungumzia masuala yanayohusu unyanyapaa.

Sisi ni mkusanyiko wa walei na waliosimikwa, wa kike na wa kiume, tunaotoka katika tamaduni, nchi na madhehebu mbalimbali. Tunatoka katika makanisa, mashirika ya kikanisa na jumuia za Kikristo na asasi za wananchi wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Tunashiriki maumivu ya virusi vya UKIMWI vilivyotuingilia na kutuathiri, kwanza kama wanadamu binafsi na pia kama jamii ya kikanisa. Katika nyakati hizi za UKIMWI, tunashirikiana kukabili changamoto za kufanya kazi kithiolojia kuudhibiti unyanyapaa kwa kuyazungumzia masuala ya ujinsia, na kutafakari upya utume wetu na kuibadili mifumo yetu.

Msingi mkuu wa kazi yetu ni imani kuwa sote tumeumbwa katika sura ya Mungu. Mungu alituumba kwa manufaa yetu na yale ya nafsi ya Mungu. Hivyo miili yetu imekuwa hekalu la Mungu.

Tunathibitisha ya kuwa Mungu:

- Ni Muumba wetu anayetukumbatia kwa neema, upendo, na fadhili:
- Huteseka pamoja nasi tunapoteswa:
- Yu pamoja nasi katika uzima na katika mauti

Tunathibitisha ya kuwa kanisa lina wajibu wa kukabili unyanyapaa utokanao na UKIMWI kwa:

- Kustawisha uwepo wake miongoni mwa watu wanaoishi ama walioathirika na Virusi vya UKIMWI ama UKIMWI:
- Kufanyia kazi ustawishaji wa jumuia zilizo tayari kushirikisha rasilmali watu zilizopo ikiwemo stadi na busara ya watu wanaoishi na UKIMWI.
- Kutoa kipaumbele kwa watu wanaoishi na UKIMWI
- Kukumbuka ya kwamba watu wanaoishi na UKIMWI ni miongoni mwa hazina zenye nguvu katika mapambano dhidi ya maradhi haya.

Tunathibitisha kuwa ujinsia wa mwanadamu unapaswa kufurahiwa na kusherehekewa. Tumeumbwa kama viumbe wenye jinsia, lakini tumeagizwa kuwa mawakili bora juu ya ujinsia wetu, na kuwa na mwenendo wajibifu mbele ya kila mmoja wetu na kwetu wenyewe. Tukiutambua utu na heshima ya kila mmoja, pia tunaubeba wajibu wa kulindana dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na unyanyapaa unaoambatana nao kila mara.

Sisi tunaotoka Kusini mwa Afrika na wale wanaotoka katiki nchi za Kaskazini mwa Ulaya, tunatambua kuwa unyanyapaaji unaoambatana na UKIMWI unadhihirika katika mazingira tofauti ya kitamaduni na kitaifa, na kwa hivyo sura yake pia hutofautiana. Juhudi njema katika eneo moja inaweza isifae katika eneo lingine. Pamoja na kuzikubali tofauti zetu tunatambua kuwa tunahitaji zaidi kufanya kazi pamoja. Kwa maana hiyo tunapokea changamoto za kila aina zilizoibuliwa na mjadala wetu tukijua ya kuwa huo uliweka bayana hali halisi ya kiulimwengu tunayojaribu kuizungumzia. Tunaamini ya kuwa ugunduzi wa kuwepo tofauti za kimazingira baina yetu umeboresha kazi tunazofanya katika nchi zetu mbalimbali, na kutoa mchango katika mapambano dhidi ya unyanyapaa unaoambatana na UKIMWI.



Ushirikiano baina ya kaskazini na kusini katika nyakati za UKIMWI

# Changamoto ya Unyanyapaa

NA JAPHET NDHLOVU, BARAZA LA MAKANISA NCHINI ZAMBIA, JAN BJARNE SODAL, BARAZA LA MAKANISA NORWAY, BIRTHE JUEL CHRISTENSEN, SHIRIKA LA MISAADA LA KANISA DENMARK, ELIAS MASSICAME BARAZA LA MAKANISA MSUMBIJI

Moja ya vikwazo vyenye nguvu katika kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI na pia tiba inayofaa, ni unyanyapaa na ubaguzi unaokabiliwa na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI, jamaa zao na wahanga wao. Dini zimekuwa na mwelekeo wa kuimarisha unyanyapaa badala ya kuupinga.

Sauti nyingi zimesikika zikiuagiza ulimwengu kuukabili UKIMWI na changamoto zake. Juhudi zilizopo sasa zilizaliwa na azma ya kuitikia sauti hizo: hususan kuunga mkono mapambano dhidi ya unyanyapaa, kuhamasisha sharika zinazowapokea watu wote na kuimarisha udugu baina ya Kaskazini na Kusini. Dhamira ilikuwa ni kufanya ugunduzi wa fursa na maarifa mbalimbali yanayoweza kupatikana kutokana na mjadala wa kithiolojia baina ya Kaskazini na Kusini juu ya masuala yanayohusu UKIMWI – muhimu zaidi mjadala ambao wananchi wanaoishi na VVU na UKIMWI wamekaribishwa kushiriki kikamilifu.

Mnamo Mwaka 2001, mjini Nairobi Baraza Kuu la Makanisa Ulimwenguni (WCC) liliandaa Kongamano la Kidunia kuhusu Juhudi za Umoja wa Kimadhehebu kukabili changamoto ya UKIMWI barani Afrika. "Kwa makanisa", imeandikwa katika dibaji ya Mpango wa Utendaji wa kongamano hilo "…mchango mkubwa tunaoweza kuutoa katika kukabiliana na maambukizi ya VVU na UKIMWI ni kuutokomeza unyanyapaa na ubaguzi."

Mchakato wetu wa kuzungumza pamoja na kushirikiana ulikuwa ni mwitikio wa moja kwa moja kwa wito huo. Ilitarajiwa ya kuwa mitazamo mipya itakayotokana na mazungumzo haya itasaidia kutambua baadhi ya vyanzo vya kithiolojia na kikanisa vinavyosababisha unyanyapaaji unaoambatana na UKIMWI. Sehemu iliyoongezwa, lakini muhimu katika jukumu hili ni kutoa machapisho yatakayokuwa na manufaa kwa jumuia za mahali, hususan wale walio na wajibu wa kufundisha, kuhubiri, kuabudu, na kufanya shughuli zingine za kisharika.

Ushirikiano wa Kikanisa baina ya Jumuia za Kikristo Ulaya Kaskazini na Kusini mwa Afrika ni matunda ya uhusiano wa karibu baina ya jumuia hizo. Ushirikiano huo unaoundwa na umoja wa Jumuia za Kikristo Kusini mwa Afrika na Mabaraza matano ya makanisa katika nchi tano za Ulaya Kaskazini. Ikiundwa na mabaraza 16 ya makanisa ya kitaifa, ushirikiano huu ulibuniwa mwaka 1988 kutokana na haja ya kutafuta njia mpya za kutoa mchango dhidi ya sera za kibaguzi Afrika Kusini. Mnamo mwaka 2003, wakikabiliwa na changamoto ya UKIMWI katika maeneo husika makatibu wakuu 16 waliafikiana kuanzisha mchakato wa tafakuri ya kithiolojia juu ya uzoefu uliopo kuhusu unyanyapaa na ubaguzi unaoambatana na UKIMWI.

Mabaraza ya makanisa ya kitaifa nchini Zambia, Msumbiji, na Norway, pamoja na Shirika la Misaada la Kanisa Denmark, yaliombwa kuendeleza mchakato huo kwa niaba ya kundi lote. Jopo liliteuliwa nalo limekutana na kuwasiliana mara kwa mara, na linahusika na chapisho hili ulilo nalo mkononi mwako sasa hivi.

## Umoja na Kristo

Toleo hili ni kusanyiko la makala yaliotayarishwa kutafakari baadhi ya masuala ya kithiolojia yaliyoibuka katika harakati za mchakato huo. Toleo la pili ni mkusanyiko wa hazina za kutumika kwa maombi, sala, ibada, kuabudu, na kujifunza Biblia, ikishirikishwa na shuhuda binafsi kutoka watu wanaoishi na VVU na UKIMWI katika maeneo yote Kusini na Kaskazini.

Tumeyapa matoleo haya kichwa cha habari "Mwili Mmoja", kwa kuwa katika Kristo sote tu wamoja. Sisi tu mwili mmoja tulioumbwa kwa damu na nyama ingawa tu kila mmoja peke yake. Kristo Mponyaji, Kristo Mpatanishi anatuinua na kutupa maisha mapya kama watu binafsi na kama jumuia. Hata kama tu dhaifu kiasi gani, hata kama tu wagonjwa, hata kama tumechanganyikiwa na maisha yetu halisi kuwa magumu, sisi tu kamili machoni pa Mungu. Tuliumbwa kwa sura ya Mungu na kupewa maisha mapya katika Kristo kupitia Roho Mtakatifu. Hali ni vivyo hivyo kwa jumuia ya Kanisa.

"Kusiwepo na faraka katika mwili" ni kauli aliyoitoa Mt. Paulo. Katika Injili ya Yohana Yesu anaenda mbele zaidi, alipoomba kwa Baba: "Kwamba wote wawe na umoja . Kama vile wewe Baba ulivyo ndani yangu nami ndani yako, wao nao wawe ndani yetu, ili kwamba ulimwengu uamini kuwa wewe ulinituma."

Mungu anadhihirishwa katika umoja wa mwili ambao unabeba mfano wa umoja wetu na Mungu. Hivyo basi mfano tulio



nao wa Mungu, tunavyojifahamu wenyewe kama Kanisa, na mtazamo wetu juu ya ujinsia wa mwanadamu vina uhusiano kila kimoja kwa kingine. Umoja huu ndio tunaousherehekea tunapokusanyika pamoja kama jumuia.

Ni katika taratibu zetu za ibada, tunapoabudu na katika ujumbe wa mahubiri yetu ambapo "Mwili Mmoja" unasherehekewa na kuzingatiwa. Lakini kwa masikitiko hapa ndipo migawanyiko inaumbika na kukuzwa, mahala ambapo hisia za unyanyapaa zinajengeka na kuendelezwa na Mungu anaonekana kama muumbaji anayependa kulipiza. Kama Wakristo tunaoelewa kazi ya Mungu ya kuleta umoja, lazima tuwe makini dhidi ya nguvu hizi za migawanyiko. Pale ambapo nguvu hizo zinachukua sura ya unyanyapaa na kukataliwa ni lazima tuelekeze nguvu zetu kuukataa katiba na daima kuimarisha kutegemeana kwa mwili wa Kristo.

## Taswira inayopotosha haki

Virusi vya upungufu wa Kinga Mwilini (VVU) ni moja ya changamoto kuu zinazoukabili ulimwengu kwa sasa zikiwa ni tishio kwa kizazi cha binadamu duniani katika kuharibu maisha ya watu binafsi, familia, jamii, na mataifa. Kwa wale waishio na VVU na UKIMWI, unyanyapaa ni sababu kuu inayowafanya wasite kutangaza hali za afya zao ama kujitokeza kupokea ushauri nasaha wa hiari, huduma ya afya, ama matibabu ya kuzuia maambukizi toka kwa mama mja mzito hadi kwa mtoto mchanga tumboni.

UKIMWI na Virusi vyake umeathiri maisha ya binadamu kwa njia kanganyifu na kwa kina sana. UKIMWI umekuwa kioo kinachotoa taswira ya upotoshaji wa haki, inayoondoa usawa, iletayo unyanyapaa na ubaguzi ambao tayari upo katika jamii. Katika maeneo yaliyoathirika sana, UKIMWI umejizatiti katika tamaduni husika na unaupindua ulimwengu juu chini ukitoa changamoto kwa asasi zote za jamii katika ngazi zote. Kwa hiyo tunapoutafakari UKIMWI na Virusi vyake tunatambua bayana mihimilli yake halisi ya kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi.

Mjadala wa kimataifa juu ya UKIMWI umechochewa zaidi na vyombo vya habari na umaarufu wa kifedha unaotokea kaskazini mwa ulimwengu. Tiba ya kiafya ni mfano mojawapo. Mapambano juu ya haki miliki za kiuvumbuzi, haki za hifadhi za kitaaluma na fursa ya kuyapata madawa ya kurefusha maisha yametangazwa sana na kutawala habari kuu katika vyombo vya habari hata kuhamasisha fikra mpya na kubadili mipango mbinu ya utafiti na tiba. Kwa kuzingatia zaidi usambazaji wa madawa na rasilmali, miundo ya mifumo ya kiafya, fursa za kufanya utafiti na vipaumbele vinavyozuiwa na taratibu zinazotumika kutibu, UKIMWI umeibua maswali muhimu juu ya mfumo uliopo wa kidunia.

Tukitumia maneno ya kasisi wa Uganda Padri Gideon Byamugisha, anayeishi na Virusi vya UKIMWI: "Sasa inafahamika ya kwamba katika UKIMWI, si hali yenyewe inayoleta maumivu sana, bali ni unyanyapaa na uwezekano wa kukataliwa na kutengwa, kutoeleweka na kutoaminiwa hali ambazo wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wanapaswa kukabiliana nazo."

Kwa Waafrika suala la rangi ya mtu limekuwa la muhimu sana. Picha iliyopo ya Afrika kama "chimbuko la UKIMWI", inaupatia nguvu sana ubaguzi na utengano na hivyo kuthibitisha uhalisi wake. Kuna hofu kuwa hisia za kibaguzi zinachochewa na utolewaji na uenezaji mkubwa wa takwimu zinazojaribu kuhusisha kizazi cha Kiafrika na ongezeko la maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo matokeo ya unyanyapaa unaotokana na UKIMWI yanafika mbali zaidi ya mtu binafsi, familia, ama jumuia ya mahali na kuupa mandhari mjadala wa kiulimwengu juu ya UKIMWI.

Unyanyapaa wanaoupitia watu ni kama kirusi kilichoshikamanishwa kwa kirusi kingine hatari. Vita dhidi ya unyanyapaa inaokoa maisha, inapunguza mateso, na inaongeza maradufu uthamani wa maisha hata mahali ambapo tiba mathubuti haipatikani.

## Kanisa liliposuka na Ulimwengu uliopasuka

Katika nyanja za Kikristo UKIMWI umekuwa sababu kuu ya utengano wa kijamii, ubaguzi na unyanyapaa. Waumini wengi wameona na wakingali kuuona UKIMWI kama kiashiria cha dhambi na mmomonyoko wa maadili. Wazazi wanapokua wamefariki ama kuishi na Virusi vya UKIMWI watoto wao huondolewa kutoka katika shule za Kikristo na wanafamilia wao kusutwa na sharika zao.



UKIMWI umetumika kama kisingizio cha kuhubiri maadili na njia sahihi ya kuishi, na papo hapo kudumisha tabia ya kujihesabia haki ya kundi kubwa la wanaoonekana kuwa na "maadili safi". Kwa wakati huu pia hospitali za misheni, shule, na programu za afya ya jamii zenye uhusiano na makanisa kwa siri na kwa subira zimekuwa zikitoa huduma kwa wale wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kuwaunga mkono katika kudai huduma bora na heshima ya kimsingi anayostahili mwanadamu. Hata hivyo haishangazi kuona kwamba wengi wamependelea kuwa kimya na kuikana hali yao, kuliko kukaribisha dharuba ya unyanyapaaji na kutengwa kijamii waliyoona wengine wakilazimishwa kustahimili. Kulingana na mateso hayo na maafa ya kijamii yaliyo dhahiri mbele ya macho yetu tunajiuliza ni ipi iliyo "dhambi halisi"?

## Hoja ya Unyanyapaa

Unyanyapaa maana yake kumbandika mtu alama ya yule asiyefaa kuhesabiwa kama sehemu ya jumuia. Mara nyingi hali hii imeleta ubaguzi na kutengwa kwa watu. Tujue kuwa alama hii haihitaji kuonyeshwa waziwazi ingawa namna jeuri zaidi za unyanyapaa zilizojificha zaweza kudhihirika kama zile zilizo wazi zaidi, kwa mfano, hali tabia, kampeni za kunon'gona, kuepuka kugusana ama kutazamana ana kwa ana, na kutojumuishwa kundini. Ni yakini kuwa wale wanaopitia hali za jinsi hii huhifadhi mioyoni ishara zote za kunyanyapaliwa na hatimaye hupatwa na aibu kuu na kujiona wana hatia, mambo yanayoashiria kujinyanyapaa.

Hivyo, ni wazi kuwa, zipo sababu nyingi kwa nini mtu angependa kuficha hali yake ya kuwa na virusi vya UKIMWI ama kuepuka kupima kutakaodhihirisha ukweli huo. Katika baadhi ya jumuia idadi ya walioambukizwa yaweza kuwa kubwa kiasi cha kutoweza kuuficha UKIMWI. Katika jumuia zingine kuna kiwango cha ufahamu kilichopo kisicho rasmi, ambapo jambo linafahamika na kutambulika jinsi lilivyo kimya kimya katika ngazi moja, lakini bado picha itatolewa kana kwamba hali sivyo ilivyo. Mbali na hayo, jitihada za watu kuziweka wazi hali zao hakuleti maana kuwa unyanyapaa utatokomea. Sababu za kuwepo unyanyapaaji ni nyingi na ni za kiutamaduni zaidi na mara nyingi si rahisi kuzitambua. Mwishoni hakuna atokaye nje awezaye kuhakiki kama upo ama la, ni wale tu wanaoishi ama kuathirika moja kwa moja na virusi vya UKIMWI ndio wanaoweza kueleza kama unyanyapaaji unaombatana na UKIMWI ungalipo katika jumuia zao.

## Huruma ya Yesu

Kanisa limeitwa kuwa tofauti. Ni ufahamu gani wa kina ambao imani ya Kikristo inatupatia katika jitihada zetu za kuukabili unyanyapaaji na kutenga wengine kunatokana na UKIMWI?

Baadhi ya maandiko ya Agano Jipya yanatoa msaada muhimu katika kutafuta mwitikio halisi wa Kikristo katika kupambana na ukimya, aibu, na unyanyapaa unaombatana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI wenyewe.

Katika Mashariki ya Kati ya karne ya kwanza, ukoma ulichukuliwa kama maradhi ya kutisha na ulinyanyapaliwa kwa kipekee kabisa.

Yesu alipokutana na mwenye ukoma katika barabara moja Galilaya aliamua kuunyosha mkono wake na kumgusa mwenye ukoma huyo wakati akimponya. Kwa kufanya hivyo aliinajisi mila ya kijamii na kuivunja miiko yake, na pia kujihatarisha na uwezekano wa kupata maambukizi yanayosababishwa na ukoma. Kwa kifupi, Yesu alichagua kuihatarisha afya yake na kibali chake mbele ya jamii. Kwa nini alifanya kitendo cha aina hii katika namna isiyokubalika kijamii na hata kiafya?

Uponyaji wa mwenye ukoma haukuwa tukio lililojitenga. Bali, huruma ilitawala huduma na maisha yote ya Yesu. Kila mara alionyesha huruma alipokutana ana kwa ana na ujinga, njaa, maradhi na hata mauti. Yesu alishikwa na huruma alipowaona wenye maradhi na wasioona miongoni mwa makundi ya watu na kuiona huzuni ya wale waliowapoteza wapendwa wao. Lakini huruma za Yesu hazikubakia katika kiwango cha hisia tu, bali zilidhihirika katika huduma aliyoitoa kila siku. Kutokana na huruma hizo alifufua wafu, aliyafundisha makundi makubwa ya watu na aliwaponya wagonjwa.

Katika kuwahudumia wenye shida, Yesu hakuogopa kuishika miili yao. Aliishika mikono ya wagonjwa na waliopagawa na pepo wachafu. Vidole vyake viligusa macho yasiyoona, masikio yasiyosikia na ndimi zisizosema. Hata hivyo, la kushangaza kuliko yote, ni pale Yesu alipowagusa wenye ukoma - wale waliotengwa na jamii katika zama zake. Kwa jinsi hiyo Yesu alitoa kielelezo cha kina juu ya huruma aliokuwa nayo.

Huruma ya Yesu haikuwa na mipaka, ikitiririka kuwavuka marafiki wake hata kuwafikia na kuwavutia maadui zake. Kulingana na Agano Jipya Yesu si mfano bora tu wa huruma ya kibinadamu. Muhimu zaidi, anautwaa moyo wenye huruma wa Mungu wa Biblia. Huruma ya kimungu hufuatiwa na utendaji wa kimungu na hii imejitokeza zaidi ya mambo yote katika Yesu Kristo. Tunapaswa kuyaangalia makanisa yetu ambayo ni mwili wa Kristo kupitia kioo hiki na kutazama jinsi ambavyo yanakabiliana na ukweli halisi wa VVU na UKIMWI.



## Mapatano Baina ya Tofauti Zilizopo

Katika mchakato uliotupatia vitabu hivi jukumu kubwa limekuwa kujaribu kubaini baadhi ya misingi ya kithiolojia na kikanisa ya unyanyapaaji na ubaguzi unaofanyika makanisani dhidi ya wale wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, ama familia zao na wahanga wao. Kwa kuwezesha kupatikana kwa tafakuri hizi tunatarajia kusaidia ustawishaji wa jumuia halisi, kamili katika kutobagua wengine na zilizopenywa na upendo wa Mungu.

Ukizingatia kile kilichokwisha kusemwa hapo juu, basi na ijulikane dhahiri kuwa hili si jukumu lililo rahisi. Mnamo mwaka 2003 huko Namibia, Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu UKIMWI (UNAIDS), liliandaa warsha juu ya unyanyapaa kwa wanathiolojia maarufu kutoka mabara matano duniani. "Thiolojia ya Kikristo," kwa mujibu wa makubaliano ya warsha hiyo, "wakati mwingine bila kukusudia, imeendeleza kazi zake kwa namna iliyodumisha unyanyapaa, na kuongeza uwezekano wa kuwepo ubaguzi." Kulingana na wanathiolojia walioshiriki warsha hiyo nchini Namibia, hali hii inapaswa kufanyiwa kazi katika ngazi nne tofauti: kile waumini wa Kikristo wanachokiamini, kile makasisi wao wanachokihubiri, kile wanachokiimba na jinsi wanavyoomba, na kile kinachofundishwa katika vyuo vyao vya kidini.

Mazingira ya mambo haya nchini Zambia, Msumbiji, Denmark, na Norway ni tofauti kabisa. Bila shaka katika mchakato wetu wa pamoja tulifikia hitimisho kuwa tafakuri za kithiolojia juu ya unyanyapaa unaohusiana na UKIMWI zimeibua maswali ya kawaida kuhusu mada kuu tatu:

1. Kufanana kwetu na Mungu
2. Itikadi yetu ya Kanisa
3. Suala zima la Ujinsia wa Mwanadamu

Kwa mfano: tukifikiria dhana kuwa ambukizi la UKIMWI ni adhabu toka kwa Mungu mwenye hasira na aliye katili, tunawezaje kuipima dhana hiyo na Mungu wetu wa maandiko ama Mungu yule tunayekutana naye Kanisani? Pale ambapo watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ama UKIMWI wanajisikia kunyanyapaliwa na kutengwa na sharika zao, hilo nalo linatueleza nini juu ya uelewa wetu wa Kanisa tunaloamini kwalo?

Pale uhusiano baina ya UKIMWI na ujinsia unapochukuliwa kuwa ni sababu mojawapo ya unyanyapaaji wa wengi walioambukizwa ama kuathirika na virusi vya UKIMWI, je hii inatupa picha ya mtazamo wa Kikristo juu ya ujinsia wa mwanadamu ama la?

Mchakato wetu haukuwa wazi zaidi hapa. Utofauti wa mazingira yetu bila mshangao umetuletea pia tofauti kubwa ya michango ya mawazo ambayo wakati mwingine yalijipinga yenyewe moja kwa moja. Lakini huu ndio ukweli wa hali ya sasa ya Kanisa. Ni matumaini yetu kuwa maandiko haya yenye mitazamo tofauti yatakuwa kichocheo cha mijadala ya kweli. Litakuwa zoezi la kupendeza kwa kikundi chochote kusoma kwa pamoja makala chache kutoka mabara tofauti, juu ya mada mojawapo kati ya zile tatu kuu, na pia baadhi ya nukuu, na kulifuatilia somo hilo kwa kubadilishana fikra na tafakuri kulingana na matukio halisi ya kimaisha ya washiriki.

Siyo nia yetu kujifanya kuwa tumefanikiwa kuzungumzia mada zetu tatu kwa kina kile cha kithiolojia kama kila moja inavyostahili. Si kwamba tunaomba radhi kwa hilo bali ni juu yako msomaji, kama utapenda kuuendeleza mbele zaidi mjadala wa mada hizo.

Matarajio yetu ni kuwa maandiko haya:

- Yatazaa fikra na juhudi mpya katika UKIMWI
- Yatakuwa zana muhimu kwa vikundi vya mafunzo, uendeshaji wa ibada, mafundisho ya Biblia na shughuli zingine.
- Yataanzisha tathmini na michakato zaidi kama huu kwa masuala mengine yanayohusishwa na kile kinachosababisha unyanyapaaji; na
- Kuipa nguvu miradi ya kimataifa na ile ya kimajimbo inayoyatafakari masuala haya na kutoa maandiko mengine zaidi.

Ni matarajio yetu kuwa, "Mwili Mmoja" unaleta tafakuri inayojumuisha fikra tofauti zilizoafikiana kuzingatia ubinadamu wetu na ushirikiano wetu wa kimadehehebu. Sisi tunatoka Kusini na Kaskazini, Mashariki na Magharibi, na pia kutoka makanisa mengi. Sisi tu walei kwa waliosimikwa, waume kwa wake, wenye kuishi na virusi vya UKIMWI kwa wasioishi na hivyo.

Sote pamoja tumeitwa kuishi katika mapatano, ikiwa ni ishara ya upendo wa Mungu katika ulimwengu huu. Ama kwa hakika tu Mwili Mmoja.



Mchango mkubwa wenye nguvu ambao makanisa yanaweza kutoa katika kupambana na maambukizi ya UKIMWI ni kuendesha elimu juu ya unyanyapaa na ubaguzi. Miongoni mwa Makanisa yaliyojihusisha na UKIMWI tokea awali mengi yameendesha programu zenye kutoa huduma, elimu na ushauri nasaha bora. Lakini changamoto inayokabili makanisa inasikika katika kina kirefu zaidi kuliko hiki. Kadiri jinsi janga hili limeendelea kujitokeza limeumbua, madhaifu yetu yaliyobebwa na fahamu zetu za kithiolojia, maadili yetu, taratibu zetu za ibada, na kwa jinsi tunavyoendesha huduma zetu za kila siku.

Siku hizi, makanisa yanapaswa kukubali - hata kama ni kwa shingo upande- kuwa tumechangia moja kwa moja ama kwa njia nyingine kuenea kwa virusi. Ugumu wetu katika kuyazungumzia masuala ya ngono na ujinsia wa mwanadamu umetuletea uchungu sana kujaribu kuyazungumzia hata kama ni kwa uwazi na kwa njia ya kweli masuala ya elimu ya ngono na uzuiaji wa maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

Mwelekeo wetu wa kuwatenga wengine, tafsiri yetu ya maandiko na uelewa wetu wa fundisho juu ya dhambi yote kwa pamoja yamejiunga kuuendeleza unyanyapaa, ubaguzi na mateso kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ama UKIMWI wenyewe. Hii imeathiri matokeo bora ya utoaji huduma, elimu na juhudi za kuzuia maambukizi mapya na badala yake imeongeza mateso ya ziada kwa wale ambao tayari wameathirika na virusi vya UKIMWI.

Kutokana na umuhimu mkubwa kwa hali iliyopo sasa, na imani kuwa makanisa yana nafasi pekee ya kusimama katika kulikabili janga hili, tunatakiwa kurejea upya utume wetu, kuleta mabadiliko katika mifumo yetu na njia zetu za kufanya kazi.

BARAZA KUU LA MAKANISA ULIMWENGUNI (WCC), MPANGO WA UTEKELEZAJI, NAIROBI,2001





# Ujinsia wa kibinadamu

MADA, KAMATI TENDAJI, USHRIKIANO WA JUMUIA ZA KIKRISTO ULAYA KASKAZINI NA KUSINI MWA AFRIKA, LUSAKA, 2004.

Makanisa yetu bila kutarajia wakati mwingine yamesababisha unyanyapaa na ubaguzi kwa ukimya wao juu ya, ama kwa mitazamo hasi ya kithiolojia waliyofundisha. Dhambi za ujinsia zimenyanyapaliwa juu zaidi kupita dhambi zote zingine. Hata hivyo imani ya kibiblia inaelewa dhambi kimahusiano, yaani, katika kuvunja uhusiano wetu halisi na Mungu, uhusiano baina yetu kila mmoja kwa mwenzake, na kwa uumbaji wote uliopo katika kila fani ya maisha yetu ya kila siku. Yesu alithibtisha kuwa dhambi, hata ile ya zinaa, haikuwa sababu ya hukumu ya papo kwa hapo, bali ilihitaji msamaha pia. Kanisa limejipanga katika nafasi inayohukumu dhambi za ujinsia na kwa sababu hiyo watu wameshindwa kujiweka wazi na kulizungumzia jambo hilo.

Mazingira tofauti ya kiutamaduni pia yamechangia kwa miiko mbalimbali iliyopo juu ya ujinsia. Imekuwa vigumu kuyajadilli masuala haya kwa wazi hata katika kanisa na hali hii bado haijakosolewa kanisani. Kwa upande mwingine, Kanisa limekataa ukweli unaozunguka tabia zinazoambatana na ujinsia, na limejifanya kana kwamba ngono haifanyiki. Bali tunajua kwamba hilo lipo na linafanyika kila siku miongoni mwa washirika wa kanisa. Unyanyapaaji wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI umekomaa kutokana na kuwepo kwa kiunganishi potofu baina ya dhambi na ujinsia ambacho mara nyingi kimedhihirika katika fikra za kikristo.

Hii imesababisha watu wengi kujisikia kutelekezwa na hivyo kuendelea kukaa mbali na kanisa. Hukumu na kukosekana kwa uwazi kumerudisha nyuma jitihada za kuuzuia UKIMWI na utoaji huduma.

## Ujinsia wa Binadamu kama Kipawa toka Mungu

Sisi tumeumbwa kwa mfano wa Mungu na ujinsia ni sehemu ya uumbaji wa asilia ya binadamu. Mungu ametuumba kama binadamu wenye ujinsia pamoja na tofauti zetu na ujinsia unapaswa kusherehekewa, kufurahiwa, na kushughulikiwa kwa uwajibikaji mkubwa kwa maana hiyo kanisa linahitaji kuzungumzia ujinsia kwa hisia chanya na kuleta simulizi njema zinazohusika. Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI pia ni binadamu wenye ujinsia na hivyo wanahitaji ukaribu wetu.

Katika kuzungumzia masuala ya ujinsia changamoto kuu kwa kanisa ni kuwahudumia na kuwahurumia walioambukizwa na walioathirika na UKIMWI, kwa kuvuka mipaka ya hofu na ubaguzi tukiubeba mtazamo wa Yesu tukiwafikia na kuwagusa wale walio na shida. Kwa mguso rahisi bali ulio muhimu Yesu aliondoa vipingamizi, changamoto, mila na sheria zilizoleta utengano na hivyo kudhihirisha uelewa wake juu ya maana halisi ya milki ya Mungu inayojumuisha. Hii ina maana ya utendaji, kwa mfano kuanzisha kikundi cha huduma katika usharika mdogo ama kuwasaidia wale wanaotoa huduma hii.

## Maadili ya Ujinsia

Mungu alituumba kwa ajili ya kila mmoja wetu na kwa ajili yake. Miili yetu ni hekalu la Bwana na matumizi mabaya ya miili yetu hii ni uhalifu kinyume cha Mungu na pia uumbaji wake. Mungu alituumba tufurahie uhusiano wa kimapenzi na katika kuthamini kipawa hiki, kuna maadili ya msingi yanayotakiwa kuzingatiwa kama vile heshima, uwajibikaji, utoaji huduma, kusamehe, kupenda na usawa.

Tunapojadiliana juu ya ujinsia, yapo masuala yanayotakiwa kuzungumziwa na kanisa kama vile matumizi mabaya ya madaraka, dhuluma, uonevu, unyanyasaji, dharau, na uonevu wa kimapenzi. Tunapoheshimiana baina yetu kama viumbe wenye ujinsia tunayapa heshima maisha yetu pia. Kanisa lazima likubali kwamba watu wengi wamelazimishwa kuchagua kuishi nje ya uhusiano wa kimapenzi wakati mwingine ikisababishwa na unyanyapaa unaohusika na ujinsia. Kwa hiyo kanisa lazima lichukue nafasi ya mbele ya kuyashughulikia masuala haya.

Watu binafsi ni lazima wawajibike na ujinsia wao ikiwemo wajibu wa kujilinda. Kanisa lazima likubali kuwa ujinsia ni sehemu ya maisha ya kila siku, na kwamba watu wanapaswa kujilinda. Mbinu rahisi za kujikinga zinapaswa kupewa changamoto. Kanisa ni lazima pia lihimize mawasiliano ya wazi miongoni mwa waliooana katika masuala yanayohusu ujinsia wao.

## Changamoto kwa Kanisa

Kanisa ni lazima:

- Litoe elimu ya ujinsia;
- Lizungumzie kwa uwazi ujinsia toka madhabahuni;
- Litoe ushauri nasaha wa ujinsia kwa watu – likiweka mkazo maalum kwa vijana;
- Litoe mafunzo ya stadi za maisha yatakayohimiza ushupavu kwa watu;
- Lisikilize maelezo ya uzoefu walionao watu;
- Lijumuishe somo la UKIMWI katika mafunzo ya kithiolojia;
- Lihimize uasisi wa vikundi vya kuhudumia wale walio na virusi na wale wasio navyo;
- Liingize UKIMWI katika utaratibu wa sala
- Lijadili masuala ya kijinsia

Tunaamini ya kwamba mapendekezo haya yatatoa mchango katika kupunguza unyanyapaa unaohusiana na ujinsia na VVU.

MSUMBIJI

# Kanisa na Nafasi iliyo nayo katika kutoa Elimu ya Kujamiiana

NA ELIAS ZACARIAS MASSICAME

VVU na UKIMWI umeendelea kuwa suala nyeti la kuzungumzia kanisani kwa sababu ya sura yake ya ujinsia. Nchini Msumbiji matatizo yanayolikabili Kanisa yanahusu zaidi jinsi lilivyoundwa, na pia jinsi utamaduni wa Kiafrika unavyoingiliana na VVU na UKIMWI.

Ni vigumu kuzungumzia VVU na UKIMWI kwa baadhi ya makundi yanayouona kama ni uovu na adhabu kwa wenye dhambi. Zipo sababu nyingi nyuma ya hali hii, moja ni kuwa katika mchakato huo wa kujenga mahusiano na katika mazingira ya kidini. Waafrika wanaiangalia ngono kana kwamba ni kitu kinachopatikana nje ya himaya na milki yake Mungu. Kwa jinsi hiyo ukimya umejitokeza kama jawabu asilia la masuala yanayohusu ngono.

Hata hivyo njia halisi ya kutafuta ufumbuzi katika vita dhidi ya VVU na UKIMWI haina budi kuuweka ujinsia mahala pake na kuuona kama sababu inayounganika na ubinadamu na jamii yake yote. Ni lazima izungumziwe kwa uangalifu, kama kitu chema na nyeti kinachohusishwa na uzazi na utakatatifu wa mwendelezo wa kizazi cha binadamu.

Binadamu wameumbwa kwa sura na mfano wa mwenyezi Mungu na miili yao ni hekalu la Roho Mtakatifu. Kwa hiyo wanapaswa kuheshimu ukweli.

Katika zama hizi za teknolojia na mifumo mingi ya habari, haja ya kuondosha hekaya zinazozunguka VVU na UKIMWI inapaswa kufanyiwa kazi upesi ili kutoa habari sahihi za ngono kwa vijana na kuidhibiti hamu ya ngono huru kama inavyoenezwa na vyombo vya habari. Hamu ya vijana chipukizi kujitafutia uhuru na ukombozi kwa gharama zozote imesababisha kujitawala kunakodharau mamlaka na pia kuvunja msingi wa familia.

Urahisi wa kupata habari usipoambatana na mafunzo na elimu bora, hauwasaidii vijana kujenga viwango vinavyokubalika vya kimaisha, kimaadili na namna ya kuukabili ukweli.

## Kuvunja Ukimya

Jambo hili linaleta changamoto kubwa kwa Kanisa. Hata hivyo ni muhimu sana kuzingatia kuwa Kanisa bila migongano ni kanisa bila historia. Matatizo daima yapo na lazima yatazamwe kama fursa za kufikia njia mpya za kuleta ufumbuzi. Kinachotakiwa kufanywa na Kanisa leo ni kutafsiri, katika lugha nzuri, kile kinachohusika na VVU na UKIMWI wenyewe, lakini bila kuyaharibu maelezo ya kisayansi yaliyomo.

Changamoto iliyopo hasa katika mwanga wa injili ni kupata mifano hai itakayoweza kutumika, kulingana na ukweli wa tamaduni zetu, ili kuweza kuthibiti kikwazo hicho na kuuvunja ukimya unaozingira ujinsia wa binadamu. Injili lazima ichukuliwe kama kichocheo cha kuhamasisha na kuelimisha watu juu ya tatizo la VVU na UKIMWI.

Tukiuangalia uhuru wa fikra tulionao leo, wazazi wamepoteza uwezo wa kutumia mamlaka yao juu ya watoto wao. Mfumo wao wa mamlaka umeharibiwa, nao wamenyanganywa nafasi yao kama wazazi. Hali hii imesimikwa zaidi na vyombo vya habari, ambavyo vinakilisha kizazi hiki kipya na picha zinazojenga hamu yao ya kutowajibika na ngono changa. Udhaifu wa sekta ya elimu hauwawezeshi vijana kuwa na nafsi bora na mwili ulio bora. Matokeo yake ni kuwa vijana wanakua wakiwa na msingi dhaifu wa kimaadili na hivyo kukosa malezi yatakayowafanya kuwa watu wazima wanaoheshimu ujinsia katika usafi na utakatifu wake.



Mch. Dinis Matsolo, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Msumbiji [CCM] anasema kwamba makanisa yanaitwa kutoa elimu ya kujamiiana. Anasema:

"Zingatia ya kwamba katika tamaduni nyingi jukumu la elimu ya kujamiiina lilikuwa ni jukumu la wajomba na mashangazi, na hivyo lilikuwa ni jukumu kwa wazazi kujadiliana juu ya ngono na watoto wao. Lakini mabadiliko ya mifumo katika jamii, ikiwemo kuongezeka kwa miji mikubwa, imesababisha ukweli mwingineo na katika zama za VVU na UKIMWI aina hii ya elimu ya kujamiiana haina nafasi ya kufanyiwa kazi tena.

Hivyo elimu ya Kujamiiana ni lazima ionekane kama kifaa muhimu sana cha kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI katika bara la Afrika, ambapo zaidi ya asilimia 85% ya maambukizi ya UKIMWI yanapatikana kupitia zoezi la kujaamiana. Shughuli ama vitendo vinavyoelekezwa kwa vikundi vilivyo na utayari mkubwa wa kujamiiana kama vile vijana lazima viendelezwe.

Aina hii ya elimu lazima ijumuishe habari juu ya ujinsia na afya ya uzazi ya mwanaume ili kwamba watu waelewe ya kwamba mbali na kuepuka mimba zisizotakiwa, ngono changa ina matokeo hasi mengineyo. Sote tunahitaji kutenda kwa kuwajibika ili kuweza kuzuia na kudhibiti kuenea kwa magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya tendo la ngono ikiwemo VVU na UKIMWI.

## Mtazamo wa Kibiblia

Biblia ina mtazamo chanya juu ya ngono ikiiona kama sehemu ya uumbaji wake Mungu. Nayo inazungumzia ngono katika hali ya uwazi na ukweli huku ikifundisha ya kwamba ngono ni jambo la kufurahiwa ili mradi tu inafanyika ndani ya mfumo wa ndoa [Mwa 4:1; Mith 5:15-20].

Dinis Matsolo ametoa hoja: "ukweli uliopo juu ya VVU na UKIMWI umeleta changamoto kwa ubinadamu kuona haja ya kubadili mitazamo yake juu ya ujinsia. Wanaume na wanawake wameitwa awali kabisa wote wachague kujitenga mbali na mahusiano ya ngono kabla ya ndoa, na baadaye kuwa waaminifu katika ndoa zao kwa wale waliooana.

Mafundisho ya Biblia yameeleza kuwa hii ni hali sahihi ya kuishi na kuenenda na ujinsia wa mwanadamu. Lakini mafundisho haya yametafsiriwa vibaya. Tunachokiona sasa ni wingi wa matumizi mabaya ya ngono katika jamii na huu ndio ukweli unaotukabili. Kama tunavyojua kubadili mitazamo si jambo rahisi, bali ni mchakato. Hii ina maana kuwa katika kuzuia si tu tuzingatie mabadiliko ya tabia lakini pia ni lazima tuhimize mafunzo juu ya tabia zinazotakiwa. Kama vile msemo wa Kiingereza unavyosema: "waweza kumfundisha mbwa aliyezeeka mbinu mpya."

Mwanathiolojia Mmalawi, Mch. Dk. Augustino Musopole anashauri kuwa ili Kanisa liweze kuhamasisha mabadiliko ya tabia katika masuala ya ngono na ujinsia ni lazima lifanyie kazi hali ya kutokuwa makini katika mambo kadhaa. "Tunahitaji thiolojia fasaha juu ya kanuni zetu za kijamii zinazohusu maendeleo ya ujinsia na tabia, tukiongeza pia mazungumzo juu ya thiolojia ya mwili, na ya ujinsia na starehe yake, na ya vitendo vya kidesturi vya ngono vinavyofanyika katika mazingira ya uhusiano wa kibinadamu ulimwenguni": anaeleza.

Kwa kuwa VVU husafirishwa zaidi kwa njia ya tendo la kujamiiana, kanisa na jamii zote kwa pamoja wanaaswa kuanza kutazama mitazamo ya kibinadamu na tabia zinazohusu ngono ili kuuvunja ukimya. Tafakuri za kithiolojia, mijadala na kampeni za uhamasishaji, zinahitajika mbali na shughuli zingine. Kinachoitwa thiolojia fasaha ya VVU na UKIMWI kinawezekana ikiwa makanisa na jumuia za Kikristo zitaendeleza na kutetea kuendeshwa kwa elimu ya kujamiiana inayojumuisha pamoja masuala yanayohusu VVU na UKIMWI.



Tafakuri za Kithiolojia na kiutendaji juu ya

Ujinsia, jinsia na VVU na UKIMWI

ZAMBIA

# Madhambi ya Kidume

NA JAPHET NDHLOVU

Kama vile ilivyo sana katika ulimwengu wa kibiblia, makanisa na jamiii za Kiafrika bado zingali katika milki ya Kidume. Kama jinsi ilivyo katika jamii nyingi Kusini mwa Afrika, jamii ya Kizambia bado inawakandamiza wanawake na kuwatenga mbali na kuhodhi mali na kushiriki kufanya maamuzi. Wengi ya wale walioolewa ama walio na mahusiano wanaogopa kusisitiza ngono salama kuepuka kutelekezwa na kuachwa bila chakula ama mahali pa kujisitiri na waume ama hawara zao wanaowatunza. Zaidi ya hayo ukatili wa wanaume umeongozeka kwa kasi kubwa katika zama hizi za VVU na UKIMWI hadi kwamba wasichana wengi, wanawake na bibi vizee vikongwe wamebakwa, pote majumbani na hadharani. Katika mazingira kama hayo utaratibu wa kuwa mwaminifu haufanyi kazi kwa wanawake wengi walioolewa na wasioolewa.

Utaratibu mwingine unaoshauriwa wa kujiepusha na ngono unazidiwa nguvu na mfumo jamii uliopo wa kugawa madaraka isivyo sawa.

Tafiti juu ya VVU na UKIMWI zimeonyesha kuwa sababu kubwa ya kuenea kwa VVU na UKIMWI ni hali nyonge ya wanawake, hususan kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya maisha yao kutokana na kutokuwa na mali wanazomiliki wenyewe na madaraka ya kufanya maamuzi. Kwa mantiki hiyo, makanisa ya Zambia mara nyingi zaidi, ni walinzi wa mamlaka hayo ya kianaume na mahusiano mengine yasiyo na usawa. Ikiwa wanaume na wanawake wataendelea kuainishwa kama wale wasio na usawa, basi itakuwa changamoto kubwa sana kujaribu kudhibiti VVU na UKIMWI. Huu ni wito sasa kwa Kanisa na uongozi kutubu na kuacha kuukumbatia ubabe wa kianaume na badala yake wajitahidi kuielezea kwa fasaha thiolojia inayosisitiza kuwa wote wanaume kwa wanawake wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wote ni sawa mbele ya Mungu (Mwa 1:27). Yesu tangu zamani alikwisha weka msingi unaofaa kwa kuudharau ubabe wa kianaume na badala yake kutaka ustawi wa Kanisa linalotambua usawa kati ya mwanaume na mwanamke

## Uelewa unaojumuisha mambo

Hatutafika mahali tukachoka kusisitiza kuwa VVU na UKIMWI ni suala la kimaendeleo. Tabia ya kujaamiiana nchini Zambia, ikiwemo ile inayofanyika ndani ya ndoa, zaidi imeathiriwa na desturi za kidini, kijamii na kitamaduni. Kwa mfano mwanamke anafundishwa asikatae kufanya ngono na mumewe hata kama yeye amejulikana kuwa ana mahusiano ya zinaa kinyume cha ndoa ama anashukiwa kuwa tayari ameambukizwa VVU ama magonjwa mengine ya zinaa. Ndoa ya wake wengi nayo imehusishwa kama moja ya mianya inayomweka mwanamke wazi kwa maambukizi ya VVU. Ngono nje ya ndoa inayofanywa na wanaume waliooa inavumiliwa na jamii na haionekani kuwa na athari yoyote kwa ndoa: lakini ngono nje ya ndoa inayofanywa na mwanamke aliyeolewa ni uhalifu usiosameheka. Mtazamo huu unakubalika pia na makanisa mengi na kuonekana kuwa ni wa kawaida. Kinachojulikana kama "ngono kavu" kinatendeka katika nchi yote ya Zambia ndani na nje ya ndoa. Baadhi ya wanawake walioolewa hulazimika, ikiwa ni kama zoezi la kuiga tu ama mbinu ya kukabiliana na hali ngumu ya kiuchumi, kushiriki

**Ipo haja ya uongozi uliojawa na uaminifu unaoweza kusababisha maamuzi na mitazamo isyotawaliwa na kuhukumiana. Makanisa ni lazima yawe mahali ambapo uwazi upo na mahali ambapo watu ambao maisha yao yameguswa na UKIMWI wanaweza kuyataja maumivu yao na kutegemea kupata huruma na faraja. Ushirika wa kiimani haulingani na Yesu kikamilifu ikiwa mtu yeyote mwenye VVU ama UKIMWI ametengwa na jumuia hiyo ama kuachwa nje. Kanisa linaloponya ni lazima livunje vikwazo hivi.**

JAPHET NDHLOVU

ngono na wanaume wengine ili kupata fedha ama zawadi zingine. Wajane nao hujikuta wakifanyiwa matambiko ya kuondoa uovu unaodhaniwa kuleta kifo cha mume. Utakaso huo hufanyika kwa njia ya ngono baina ya mjane na ndugu wa marehemu. Imani kuwa kufanya ngono pamoja na msichana bikira inaweza kuwaponya wanaume wenye VVU nayo imechangia sana ongezeko la visa vya ngono baina ya baba na binti yake na kuwaweka katika hali ya hatari wasichana wadogo. Vitendo hivi vimeongeza uwezekano wa kupata maambukizi ya VVU kwa wote wanawake na wanaume lakini imewaweka wanawake katika nafasi moja ngumu sana na kuwafanya wawe wazi zaidi kupata maambukizi ya VVU kwani hawana uwezo wa kuitawala miili yao.

Kuna muingiliano mkubwa baina ya Imani ya Kikristo, ndoa, jinsia na VVU na UKIMWI. Mahusiano na majukumu ya kijinsia katika ndoa yana athari kubwa katika mwenendo na matokeo ya VVU na UKIMWI. Jinsi tunavyoyaainisha na kuyaelewa majukumu ya kijinsia katika jamii ndivyo tunavyoyaweka mazingira halisi ya wanaume na wanawake kupata maambukizi ya VVU na hivyo kubaini matokeo yake kwa wanawake na ndoa zilizopo. Hivyo basi ikiwa kanisa litashiriki na kutoa mchango wake katika kuzuia maambukizi zaidi ya VVU, suala la haki ya kijinsia kanisani lazima litiliwe maanani kwa dhati.

Ujumbe kwa makanisa unaotolewa na wanawake wanathiolojia nchini Zambia ni kuwa haki ya kijinsia haikuzingatiwa ipasavyo kanisani. Hao wanashauri utafsiri wa maandiko matakatifu usioegemea jinsia moja dhidi ya nyingine na unaowaeleza watu upendo wa Mungu na matarajio waliyonayo watu wote kwake. Kwa mfano ule msisitizo wa wahubiri karibu katika makanisa mengi ya kuwa wanawake lazima wanyenyekee kwa wanaume si sahihi hata kidogo na unatumika nje ya mantiki husika. Si kwamba tu tafsiri ya aina hiyo inadumisha nguvu ya waume juu ya wake zao katika maeneo yote ya maisha yao ikiwemo mahusiano ya kujamiiana, lakini pia inapotosha nafasi ya wanawake wote nchini na kuwaweka chini ikiwanyang'anya mamlaka yoyote ya kumiliki ujinsia wao.

Ikiwa yapo matumaini ndani yetu ya kuzilinda familia zetu na kujenga jamii zenye afya na imara, watu wenye imani lazima waangalie mbali zaidi wasijiangalie wenyewe tu. Imani katika Kristo inaweza kuwapatia watu nguvu ya ndani ya kupokea majukumu ya kijamii na kisiasa, na kuwa na nia ya kutenga rasilimali muhimu kwa ajili ya programu zinazotetea haki za kijinsia, na pia kujenga mifano bora ya kuigwa ya ndoa na katika kudhibiti msukumo wa hamu ya kufanya ngono ambao unaweza kusababisha kupata VVU na UKIMWI. Katika kitabu cha Warumi Paulo anaelezea tatizo na ufumbuzi wake kwa pumzi moja, "Basi, nimegundua kanuni hii: ninataka kufanya jema, lakini najikuta kwamba lile lililo baya ndilo ninalochagua. Ndani kabisa katika moyo wangu naifurahia sheria ya Mungu. Lakini naona kwamba kuna sheria nyingine inayofanya kazi mwilini mwangu, sheria ambayo inapingana na ile inayokubaliwa na akili yangu. Hiyo inanifanya niwe mtumwa wa sheria ya dhambi ifanyayo kazi mwilini mwangu. Maskini miye! Nani atakayeniokoa kutoka mwili huu unaonipeleka kifoni?" [Warumi 7:21-24].

Katika Waefeso 5:22-33 Paulo alikuwa mwangalifu kuutunza uwiano katika mafundisho yake kwa kuwafundisha waume kuwapenda wake zao kama wanavyojipenda wenyewe. Kwa hiyo andiko hili ni lazima lieleweke katika mantiki kuwa upendo na kunyenyekea ni pande mbili za sarafu ile ile. Upande mmoja hauna nguvu pasipo kuwepo ule mwingine. Hii inawaweka wote mume na mke katika fungu moja.

## Ushirikishwaji wa Wanaume

Wanaume wana nafasi muhimu sana katika kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa sababu ndio kwa kawaida walio mstari wa mbele katika mahusiano ya kujamiiana na ndio wanaodhibiti matumizi ya mbinu za kinga ikiwemo kondomu. Hivyo wanaume wanachangia sana kuenea kwa virusi na hivyo wanahitaji kuhamasishwa kama sehemu kubwa katika vita vya kuuzima UKIMWI.

Ni pale tu programu zinazoandaliwa zitakapokuwa zimeelekezwa kushughulikia tabia ya kujamiiana ya wanaume ndipo tutakapopata punguzo halisi dhidi ya kasi ya kuenea kwa VVU na UKIMWI nchini Zambia. Njia kuu ya maambukizi ya VVU ni kujamiiiana. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwaamsha wanaume kuchukua daraka la kuwa watoa maamuzi wakuu katikia familia hasa katika jamii ya kianaume ya Zambia. Wanaume ndio wanaoamua watafanya ngono na nani, wapi na kwa namna gani. Wanaume kwa kawaida huwa na wapenzi wengi wa kujamiiana nao kuliko wanawake na wanaume hao mara nyingi hawatumii kondomu inavyopasa. Kwa nini wanaume wanakuwa na tabia ya namna hii? Zaidi sana ni kwa sababu jamii imewaeleza wanapaswa kuenenda namna hiyo. Wavulana wanakua wakitegemea kushiriki kwa kiasi kikubwa katika zoezi la ngono. Wanaume na wanawake wengi hudhani kuwa ni kitu cha kawaida kwa wanaume kuwa na wapenzi wengi na kwamba hamu yao ya ngono ni kubwa kiasi cha kutoweza kuidhibiti. Hivyo wavulana wanakua wakiamini kuwa wanayo haki kufanya ngono wakati wowote wanaoutaka na wasichana wanakua wakiamini ni wajibu wao kuwaridhisha wanaume. Wanawake wanaotaka kujilinda wenyewe mara nyingi hufikiri kuwa haiwezekani kuzungumzia mambo hayo na wapenzi wao.

# Mungu na Ujinsia

JAPHET NDHLOVU

**Uwepo na uwezo wa Mungu, ambao Yesu aliutangaza kama utawala wa Mungu unahusu mabadiliko ya kibinafsi, kijamii na kiulimwengu. Ukweli kwamba Mungu hakujulikana na kuelezewa kwa semi za kijinsia ilikuwa ni mafanikio dhahiri ya dini ya Kiyahudi**

**Hata hivyo, mwanzo na maendeleo ya ujinsia wa binadamu ulihusishwa na desturi hiyo, kwa namna ya kipekee na Uwepo wa Mungu wa uumbaji na nguvu yake. Katika simulizi moja kutoka kitabu cha Mwanzo (Mwa 1) pale Mungu alipowaumba wanadamu, "mwanaume na mwanamke aliwaumba, kwa sura yake aliwaumba": wapendane na washirikiane, kwa ajili ya kuzaa na kuendeleza kizazi. Kipawa hiki cha kujamiiana kwa hao wawili kwa pamoja kilitolewa kwa wanadamu walio na mfano wa Mungu.**

**Katika aina hii ya upendo wa kibinadamu, upendo wa kijinsia wenyewe unasherehekewa kama kipawa katika "Wimbo Ulio Bora". Katika maandiko mengine ya Biblia inatambulika kama kielelezo cha upendo wa Mungu kwa Israeli na pia kama ishara ya upendo wa Kristo kwa Kanisa, iliyo jumuia ya wanafunzi wake.**

**Kipawa cha kimungu cha ujinsia kina maana ya wito na majukumu aliyopewa mwanadamu. Malengo mapana zaidi ya kibinadamu ya kupendana na kuendeleza kizazi yanapata kielelezo chake maalum katika ujinsia. Malengo haya yanapaswa kufanyiwa kazi kwa kipindi cha kutosha kwa kukuza na kuijumuisha hazina hii ya ujinsia katika maisha kamili ya mtu ya kijamii na ya kimahusiano.**

**Ujinsia ni jambo safi na ni hali ya kimsingi kabisa. Hii ina maana kwamba lazima itambuliwe kama ni sehemu ya mapenzi yake Mungu. Awali kabisa ngono ni wazo toka Mungu. Hivyo haiwezi kuwa 'chafu'. Basi ujinsia ni sehemu ile ile ya uumbaji ambayo muumba aliiona kuwa ni 'njema'.**

**Ni siri takatifu baina ya watu wawili ambayo imeandaliwa kwa makusudi ya kukubalika kwa wote wawili kimwili na kihisia. Kwa maana hiyo kujamiiana kunaleta mshikamano wa kiakili unaodumu na ambao unahitaji uaminifu wa aina hiyo hiyo toka pande zote mbili. Tendo la ngono ni sehemu tu ya kitu kizima. Ni kama tamu tamu katika kitafunwa kile cha uhusiano wa maisha marefu. Matendo ya ngono baina ya watu binafsi ni kama mapumziko katika visima vya maji baridi vilivyoko jangwani baada ya safari ndefu ya taabu katika eneo hilo.**

Mitazamo ya jinsi hiyo ilipewa nguvu na ndoa asilia ya wake wengi, ambapo mwanamume angeweza kuwa na wake zaidi ya mmoja. Wapenzi wote waliheshimu utaratibu huu wa ndoa ya wake wengi na kuwa waaminifu, hii iliwapa wanaume mamlaka juu ya wake zao lakini ilipunguza uwezekano wa kuambukizana magonjwa. Leo hii desturi ile inayoruhusu ndoa ya wake wengi mara nyingi imetafsiriwa kama kielelezo cha haki ya wanaume kufanya ngono na wanawake wengi kama wanavyotaka. Nao wanafanya hivi bila kuzingatia wajibu wao wa uaminifu katika ndoa na majukumu ya kifamilia. Katika hali hii wanawake wote huchukuliwa kama vifaa vya ngono kwa kuwastarehesha wanaume. Zaidi, wanaume wanaweza wasiogope ndoa zao kuvunjika, kwa sababu wake zao kwa namna nyingi wamekuwa wakiwategemea kiuchumi na hivyo ikiwa ndoa itavunjika basi na mahari ilikuwa imekwisha lipwa, watoto watakuwa ni mali ya ukoo wa mume na si wa mke.

Wanaume wana mamalaka ya kutosha katika tendo la ngono; na si mara zote wamekosolewa kwa kuwa na wapenzi wengi mno. Wao kwa kawaida wametegemewa kutawala masuala ya ngono na daima wametarajiwa kutimiziwa haja zao za kimwili. Matumizi mabaya ya madaraka haya imekuwa ni sababu kuu ya msingi ya kuenea kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI. Hivyo ni muhimu kwamba  wanaume wahamasishwe kutambua na kufanyia kazi kwa kipaumbele masuala yanayowahusu katika kinga dhidi ya VVU na UKIMWI, utoaji huduma na kuendesha harakati za kutetea hoja halisi zilizomo katika masuala haya. Kutokana na sehemu waliyo nayo wanaume katika jamii ya Zambia ni muhimu sana kukuza uweza wao katika kukabili changamoto za Kinga ya VVU na UKIMWI.

## Mapungufu

Mbinu za sasa za kinga dhidi ya UKIMWI kimsingi zinaagiza ndoa ya mke mmoja, uaminifu katika ndoa, na matumizi ya kondomu, hasa kulingana na utu na dini – kama vile mbinu ya ABC ambayo ni kifupi cha jizuie [A]  uwe mwaminifu [B], na utumie Kondomu [c].

Kwa kuwa mbinu hizi zimeshindwa kuzungumzia kwa ukamilifu dhana zilizofichika kuhusu uanaume, mazingira yenye kiwango cha juu cha hali hatarishi na pia vitendo vya nguvu vya kijinsia, zote zimedhihirika kuwa hazitoshi na pia zina madhara. Kutokana na mifumo isiyo sawa ya kijinsia na udhaifu wa wanawake katika jamii, wanawake hawajaweza kuzatiti mikakati hii ukiwalinganisha na wenzi wao wa kiume. Mara nyingi wamewaongezea mzigo katika maisha ya wanawake kama vile mazungumzo juu ya ngono salama  yamekuwa nje ya wajibu

**VVU na UKIMWI si tu suala la kiafya, lakini pia ni suala la kimaendeleo, kijinsia, kijamii na kiuchumi, na hivyo lazima lizingatiwe kijumla. Kwa hiyo ni muhimu kulikabili tatizo la VVU na UKIMWI tukiwa na changanuzi ya kijinsia na kuangalia miitikio iliyo na hisia za kijinsia. Hii inahitaji programu pana na zenye kulenga wahusika wa mahala na lugha mpya inayotumika, tukiepuka unyanyapaa na ukandamizaji.**

JAPHET NDHLOVU

wa mwanamke. Mbinu hizi za kinga zimewaweka mahali pabaya wanawake na pia zimewakandamiza zaidi wanawake wenye maambukizi ya VVU. Mbinu yenye mafanikio sharti izingatie masuala ya jinsia kwa makini zaidi.

Kuwawezesha wanawake ni muhimu sana katika kutumia mbinu inayozingatia mambo kwa upana. Kuwaondoa wanwake katika mazungumzo nyeti inasababisha uwezo mdogo wa kukabili changamoto inayoletwa na UKIMWI. Ni katika upeo huu tukiwa na mantiki hii akilini tutashughulikia mapungufu yaliyopo katika mbinu za kinga tulizo nazo leo.

Kumekuwa na mapendekezo ya kufanyia kazi katika mazingira yetu mbinu ya ABC yaani [A- Jizuie, B-uwe Mwaminifu na C- tumia Kondomu] na hata kuiendeleza hadi iwe mbinu ya ABCDE. Badala ya kulaumu watu binafsi – hasa wanawake – kwa ajili ya tatizo la UKIMWI, ambayo kwa kweli mbinu ya sasa hivi ya ABC inafanya, wajibu wa kuleta mabadiliko urudishwe kwa jumuia za mahali. Ni muhimu sana kushugulika na kuhamasisha mazungumzo katika mazingira ya mahali tukizingatia mahusiano ya kimadaraka. Wanaume lazima wawajibishwe kwa tabia zao za kujamiiana, na mamlaka ya mahali, makanisa ama taasisi za kijamii ama kielimu lazima zikutane na changamoto kali zinapotetea matendo yenye ubaguzi na maadili mabaya.

ABCDE:

A- Utetezi kwa ajili ya usawa wa kijinsia

B- Kuusikiliza Mwili na Ujinsia

C-Kufanya kazi na jumuia na kwa kuzingatia mazingira

D. Mazungumzo kuleta maendeleo

E.Uwezeshwaji ili kushirikiana madaraka

Mwelekeo wa kina na mpana ulioegemea utetezi wa usawa wa kijinsia unahitajika na pia ule unaowatia moyo wanawake na wanaume katika jumuia za kawaida kuleta mabadiliko.

## Wito wa Uongozi

Hali halisi ya muingiliano baina ya ndoa, jinsia na VVU na UKIMWI inahitaji uongozi kanisani kukabili maadili ya kijamii yanayompa mwanamke na msichana nafasi nyonge na yale yanayokumbatia fujo na uonevu dhidi yao. Uongozi pia unapewa changamoto ya kuinua usawa wa kimamlaka baina ya mwanamke na mwanaume. Kwa njia hii wanaume watafanikiwa kutokana na utaratibu huo kama vile watakavyofanikiwa wanawake. Mzigo mzito umewaangukia wanaume kutokana na nafasi na majukumu ya kijinsia ambayo yanafananisha uume na uwezo wa kufanya ngono, kuwa na wapenzi wengi zaidi, mashambulizi ya kimwili, kumtawala mwanamke, na utayari wa kushiriki tabia hatarishi sana. Ikiwa wanaume watahimizwa kuenenda katika njia ambazo zinalingana na maandiko ya Biblia na zinapunguza uwezekano wa wao wenyewe kuambukizwa, wao kwa upande mwingine wataibuka na nguvu zaidi, hawakunyanyapaliwa tena kwamba wao ni madereva wa UKIMWI lakini wao wamesajiliwa kama washiriki na viongozi wenzetu katika kutafuta ufumbuzi.

Pia ni muhimu kutambua kazi na wajibu wa utawala wa wanaume. Ukuu wa wanaume una mizizi yenye nguvu katika Biblia na utamaduni. Ijapokuwa zipo jitihada zinazoendelea za kutaka kubadili mahusiano yasiyokuwa na usawa yaliyopo baina ya wanawake na wanaume, ndani ya Kanisa na nje katika dunia utawala wa wanaume bado ungali na nguvu. Inakubalika kwa sehemu kubwa ya kuwa Kanisa na asasi za kidini ni wadhamini wa mamlaka na utamaduni.

Hii ndiyo sababu kwa nini dhambi za wanaume zieleweke na kuondoshwa. Badala yake Kanisa linahitaji kuzipa maana harakati hizi kwa kusisitiza juu ya kugawana madaraka baina ya wanawake na wanaume. Kwa kufanya hivyo, itaiinua imani kwamba tabia ya kujamiiana yenye kuwajibika na yenye kujiheshimu kwa wote wanaume kwa wanawake lazima iwe imani ya msingi na mbinu muhimu katika kuzuia maambukizi zaidi ya VVU na UKIMWI.



Fikra, tafakuri na matukio ya makundi ya watu wanaoishi ama kuathiriwa na virusi vya UKIMWI

NORWAY

# Mwiko Hatari



Katika jamii ya Kinorway na katika makanisa ya nchi hiyo, VVU na UKIMWI vyote katika fikra za watu vimehusishwa na ngono na ujinsia. Matokeo yake ni kuwa ujinsia umekuwa ni kianzio cha mjadala wowote kuhusu Mungu na maadili. Katika kundi moja tulijiuliza wenyewe " Je Mungu ana nafasi yeyote katika ujinsia?" "Na kuna uhusiano gani baina ya mfano wetu na Mungu na uelewa wetu wa ujinsia?"

Mara nyingi imedhaniwa hasa na waumini wa kidini ingawa si wao tu kwamba ngono ni mali ya upande ulio gizani mwa maisha ya wanadamu. Katika kingo moja ya ulimwengu wa mwanadamu amesimama Mungu aliye mwanga; na katika kingo nyingine aliyekandamizwa na hatia, aibu na miiko mbalimbali ni ngono. Katika jamii ya magharibi, kumekuwa na hali ya kukimbia na kujiweka mbali na mtazamo wa jinsi hii. Ngono imekuwa ni rahisi kupatikana na inazungumzwa kwa uhuru hadharani, na kwamba imekuwa ni vigumu mtu kusema haihitaji ama anaiona kuwa ni tatizo kwake. Ile hali ya uwazi, unyeti, na tabia isiyoeleweka ya ujinsia inaonekana kudhibitiwa kabisa. Ingawa mwiitikio wa jinsi hiyo dhidi ya fikra zenye maadili safi una nafasi yake ni ule utamaduni wa ujinsia ambamo ngono imepoteza kiungo chake na imani, maadili ama wakati mwingine na mahusiano ya kibinadamu. Kwa hiyo ngono na Mungu bado zipo katika pande mbili zinazotazamana za kingo zile za ulimwengu wa mwanadamu, na imekuwa vigumu kuupata upinde wa mvua utakaojenga daraja baina ya pande hizo.

## Upendo

Je ipo nafasi kwa ajili ya Mungu katika ujinsia? Bila shaka, walijibu washiriki: ngono ni sehemu ya sura ya Mungu aliyefanyika mwili ambayo imo ndani yetu sisi sote. Lakini si rahisi kama inavyoonekana, tatizo moja ni kuwa hali yetu ya kiroho inaukataa mwili: ingine ni kuwa mfano wetu wa Mungu unatufanya ituwie ugumu kuamini kuwa Mungu alifanyika mwanadamu katika mwili wa kibinadamu akiwa na hisi za kijinsia. "Ndiyo ngono ni kipawa toka kwa Mungu" mshiriki mmoja alisema. "Lakini wakati huo huo inaleta hukumu na hatia na aibu". Inaanza kwa upendo wenye nguvu na ndipo huja hatia na aibu".

"Lazima tuwe tayari kuzungumzia ngono kama kitu kingine", alisema mwingine. Ni muhimu kuzungumzia VVU katika lugha ambayo maneno kama huba, upendo, haja ya mapenzi, msamaha, na upendo kwa jirani yanatawala. "Lakini hii si hali ilivyo siku hizi." Na bado watu wengi wanapata maambukizi ya VVU kupitia ngono ya kawaida katika mazingira ya mapenzi. Haihitaji uwe mtu wa ajabu ama uwe umeshiriki ngono mara nyingi zaidi kuvipata VVU. Tatizo kubwa mojawapo linalosababisha mitazamo waliyo nayo Wakristo juu ya VVU, ilikuwa ni kwa namna ile inavyounganishwa kikawaida katika fikra za watu na ngono, ujinsia na dhambi". "Neno dhambi limekosa matumizi." Alisema mshiriki mmoja. Limeharibiwa na kutumika vibaya limetiwa na wenye nguvu kuwaharibu na kuwadhibiti wanyonge. Watu wamelitumia kusisitiza kusanyiko la amri ambazo unaweza kujificha nyuma yake, pasipo na sababu ya kutumia kichwa chako".

## Dhambi inawatenga Watu

Dhambi inatutenga sisi na watu wengine, sisi wenyewe na sisi na Mungu. Katika mijadala yetu tulirejea mara kwa mara kwa swali alilopewa Yesu katika Yohana 9:3. " Mwalimu, nani aliyefanya dhambi, ni mtu huyu ama wazazi wake, hata akazaliwa kipofu? Swali hili linaweka mkazo kwa tabia ya kibinadamu ya kuhusisha ulemavu ama ugonjwa na makosa ya kimaadili.. "Ndani ya swali hili kuna dhana kuwa watu wengine wana hatia zaidi ya wengine, na hivyo wanastahili kile kinachowatokea. Ni kana kwamba inatufanya sisi wengine tuliobakia kuwa wenye hatia kidogo kuliko wao". Inakuwa dhahiri kuwa wale miongoni mwetu wanaoishi na VVU hujisikia kana kwamba wanachukua nafasi hiyo ya kuubeba mzigo mkubwa wa hatia.

Hali yetu ya kuwa na VVU inafanya kazi kama unyanyapaa wa kimaadili, inayoruhusu wengine kutuhukumu kama wenye dhambi, na hivyo kuwafanya wao wajisikie wakiwa wenye dhambi chache kuliko sisi. Kwa namna hii neno "dhambi" limetumiwa na Wakristo kufanya dhambi: kuvunja na kuharibu mahusiano na kujenga tabaka la wale walio ndani na wale walio nje ya kundi, ijapokuwa kinyume chake Kanisa linapaswa kuwa katika mstari wa mbele wa mapambano ya kupinga wazo la kuwepo "wenye hatia na wale wanaotembea na VVU bila kuwa na hatia".

Wakati mwingine imenipasa kukiri kuwa nilifanya maamuzi mabaya, alisema mshiriki mmoja, na sasa nabeba matokeo ya uamuzi huo: lakini si kweli kuwa sote tumewahi kufanya maamuzi mabaya?. "Ni lazima uwe na uwezo kukiri makosa, hata ndani ya Kanisa" mwingine alisema. Lakini ipo tofauti kati ya kusema juu ya matokeo na kuzungumza juu ya adhabu.



## Maadili

Maadili na amri zinahitajika kama msingi wa mahusiano mazuri na yenye uzima baina yetu, sisi kwa sisi, jumuia pana na uumbaji wote.

Sisi hatuna shaka na hilo. " Lakini amri zipo kutusaidia kutafsiri maadili hayo ya msingi katika mazingira halisi ya kimaisha. "Amri hazipo hapo kuhukumu na kutenga." Maalum sana amri lazima ziwepo hapo kutunza maisha "ndani ya uhusiano" kwa kulinda na kukinga sehemu nyeti na nyepesi kuvamiwa katika jamii na katika uumbaji. Kwa tafsiri hii, kufanya dhambi ni kuvunja ama kuharibu ujumla wote wa uhusiano, kuleta utengano toka Mungu, sisi kwa sisi na kila kitu kilichoumbwa. Leo ingawa dhana ya dhambi imebinafsishwa katika tamaduni zetu, kiasi kwamba kwa haraka zaidi tunahitaji msamiati utakaoweza kuunyoshea kidole mwenendo unaohujumu misingi bora ya uhusiano na kuiweka katika kapu kubwa la maadili tuliyo nayo siku hizi.

Katika mjadala huu washiriki walisaidiwa na usemi wa Yesu kwamba "Sabato imefanywa kwa ajili ya wanadamu na si wanadamu kwa ajili ya sabato. Hapa Yesu hasemi kwamba amri hazifai: anachosema ni kwamba ni kazi ya amri na sheria kutusaidia sisi kupata njia ya kutafsiri maadili ya msingi katika mazingira ya maisha mazuri na bora. Amri hazipo huko ili kujenga waliomo na wasiokuwemo, ama kuliwezesha kundi moja la watu kujisikia lina nguvu zaidi kuliko lingine. Tukiondolewa toka katika uelewa huu wa kuwepo amri zinazoshirikisha na zile zinazotenganisha ndipo tutakapoweza kujifunza kuzungumza kwa ukweli juu ya ujinsia na uhusiano ambapo ujinsia unatimizwa kimaisha.

Kwani ukweli ni kwamba ngono inaweza ikawa nzuri na mbaya: inaweza kudhalilishwa ama la: na hivi ndivyo hata ndoa inaweza kuwa. Kama vile mshiriki mmoja alivyoiweka "Kanisa si kwamba daima lina ukweli juu ya hali halisi ya ndoa, hususan masuala ya nafasi za kijinsia na madaraka". Ama kwa maneno mngine ya mwanamke anayeishi na VVU, "Kuna mambo mengi mabaya yanayoendelea katika ndoa, hasa kwa wanawake". "Hii ina maana kuwa", alisema mwingine, "tunapaswa kuyatazama matukio halisi katika maisha ya watu, na yale yalio yetu na si katika mambo tunayodhani yanafaa kuwa vile tunavyotaka yawe"

## Uwakili Wenye Kuwajibika

Ni kwa jinsi gani basi tutaweza kuzielewa amri kwa namna ambayo hazibagui ama kutenga wengine? Wazo la uwakili wenye kuwajibika likawa lenye umuhimu mkubwa kwetu na mjadala ukaelekea kiungo kilichowekwa baina ya uwakili na maadili ndani ya Injili. Sisi si watumwa ama vinyago hai, na miongozo haikuwekwa ili ifuatwe kama afanyavyo mtumwa. Kinyume chake, sisi ni mawakili huru na wenye kuwajibika, tunaojaribu kupata kwa wingi toka rasilimali tulizopewa na katika hali tunayojikuta tumo ndani yake. Tunahitaji kukumbuka kwamba dunia kwa hali halisi haina haki, viwango vya kuanzia maisha yetu na mazingira yake vinaweza kutofautiana sana. Na haijatokea kwamba Mungu akaweka begani mwa mhanga jukumu kuu la kupambana na upotofu wa haki.

"Tunahitaji miongozo," alisema mshiriki mmoja, akizungumzia amri; 'na kwa mawakili miongozo hii na maadili yake yanafaa kuwekwa moyoni kabisa. Lakini inachukua muda kuyafanya maadili haya kuwa yako binafsi." Katika kutusaidia kuishi kulingana na maadili ya Injili, kazi ya kanisa ni kuamsha ndani yetu wema wa msingi tulio nao, na kusaidia kukidhi hamu na kiu yetu ya Ufalme. Hii ina maana kuwa na kiu cha haki na kumpenda jirani yetu. "Mchakato wa kuyajenga maadili haya ndani yetu ni kama ile punje ya haradali", alisema mshiriki mmoja. "Tangu kuwa ndogo sana na labda laini inaweza kukua hata kuwa kitu kikubwa na chenye nguvu. Kupitia machafuko na kutokuwepo na uhakika wa mambo unaweza kufikia hatua kwa hatua ufahamu na utambuzi".

## Kutogawanyika kwa Upendo

Tafakuri juu ya ngono na ujinsia inaongoza hadi tafakuri juu ya maisha yenyewe." Nilikuja ili wawe na uzima." Yesu alisema, "na wawe nao tele." Kazi ya amri ni kuyafanya maisha yetu haya yawezekane kwa wote. Baina ya Maisha na Amri, hivyo kuifanya ngazi ya utawala iwe dhahiri: amri haziwezi kuwa juu, ama sivyo tutakuwa watu wa kisheria na hivyo kuudhuru wito wetu, na hata ule wa wengine – na kuwa mawakili wa maisha na uumbaji. Ikiwa Mungu aliumba maisha ya binadamu na jumuia zina nguvu katika ngazi yetu ya kipaumbele cha maisha safi, basi tunayo changamoto ya kuweka mkazo laini katika kuzitii amri na mkazo wenye nguvu katika wajibu tulionao juu ya maisha yetu, jumuia na uumbaji. Kwa njia hii, amri zinakuja kuandikwa katika mioyo yetu. Mungu – anayeona mioyo yetu na mwenye kujua siri zote – anatuamini kuwa tutaweza kuzitafsiri amri hizi inavyotakiwa. Ni mioyo yetu ya nyama, na si vitabu vyetu vyenye amri vinavyowezesha amri kuumbika katika dunia halisi iliyoumbika.

Kama vile tu makanisa na pia kama watu binafsi, Mungu ametuita kuheshimu, kukubali na kuwa mawakili wenye kuwajibika katika ujinsia wetu na ule wa watu wengine. Kwa kumaliza nanukuu maneno haya ya mshiriki anayeishi na VVU. "Kwa uhusiano unaopatikana kutokana na upendo wa Mungu na upendo kwa jirani, ile amri iliyojirudia mara mbili inayohusu upendo inasababisha mlolongo wa majibu toka ndani kabisa ya asili ya ubinadamu. Lakini tunahitaji kukumbuka kutogawanyika kwa upendo. Ili tuweze kuwapenda jirani zetu na kumpenda Mungu. Ni muhimu sisi tujipende wenyewe.

**Kujinyanyapaa ni hali ya kujisikia aibu kwa ndani kabisa. Inayoweza kufikiwa kwa wale ambao jamii inawanyanyapaa. Ni hali ya kuitikia kwa ndani kukabili matukio ya nje ya unyanyapaa, ambayo makundi na watu binafsi walionyanyapaliwa wanakutana nayo ama wanaamini upo katika mienendo na matendo ya wengine. Kuhusiana na VVU na UKIMWI, sura, mawazo na maana ambayo watu hubeba – kwa mfano ujinsia, maambukizi ya damu, na kifo – haya yote yanagusa maeneo ya ndani kabisa na yaliyo dhaifu katika ufahamu wao. Ni vigumu kwetu kuwa wazi na waaminifu juu ya hali zetu za kujinyanyapaa ama kunyanyapaa bila kuhatarisha maeneo haya dhaifu.**

KUTOKA TAFAKURI ZA NORWAY

**Kuambikizwa na mtu ambaye hakudiriki kusema ukweli, lilikuwa pigo kwa imani yangu kwa watu wengine. Inawezekanaje mie kumwamini mtu mwingine tena, wakati ambapo imani yangu imesalitiwa kwa kiasi kikubwa kwamba imenipatia virusi hatari? Nitawezaje kupata imani tena katika maamuzi yangu? Je inawezekana mie kujitegemea na kuwajibika na maisha yangu? Maswali haya yamesababisha kujiona mnyonge sana na kujiona kuachwa kabisa.**

PREBEN BAKBO SLOTH, ANYEISHI NA VVU, DENMARK



DENMARK

# Tuzo ya Kimungu na Jukumu la Binadamu

CARINA WØHLK

"Si vema kuwa mwanamume awe peke yake", Bwana muumbaji alisema katika Mwanzo 2:18. Maisha bora zaidi ni yale ambayo watu wanashirikiana. Mungu ametuumba tuishi pamoja katika mahusiano. Naye ametuwezesha tuungane kila mtu na mwenzake kijinsia.

Ujinsia wetu na hisia zetu ni za asili, ni namna tulizopewa na Mungu ambazo kwa hizo maisha yanapata kielelezo chake. Watu wawili waliovutwa pamoja wanaweza kuzishinda hali zao za kibinafsi na kutengeneza kitu ambacho ni kikubwa tena kina nguvu kuliko wote wawili. Tukio la kukutana kimwili laweza kuwa na nguvu na lenye ubunifu. Laweza kujenga upendo wa dhati na mkamilifu katika upeo mkubwa na kuleta starehe, heshima na kutoa nafasi ya kutosha kwa wapenzi hao. Kufanya mapenzi kwa kweli ni kipawa.

Lakini kipawa pia ni jukumu. Tunajianika sisi wenyewe katika ujinsia wetu. Tunajilaza mahala pa wazi kwa ajili ya mtu mwingine. Uwazi huu waweza kuwa jaribu pia. Inaweza kutufanya tutumie vibaya ujinsia wetu na kuwa na choyo na ubinafsi mkubwa, ili tuweze kujiridhisha wenyewe ama kuonyesha mabavu yetu na kumuumiza mpenzi wetu.

Tunapokaribiana sisi kwa sisi hasa katika hali ya kuhitaji japo kimichezo-michezo lazima tuwe waangalifu tusidhalilishane. Mungu ametupatia wajibu wa kutumia ujinsia wetu katika hali ya kuwajibika. Yeye anawapenda wengine kwa hiyo anataka ujinsia wetu uyatumikie mapenzi.

Wanadamu ni viumbe wenye ujinsia, kwa sababu Mungu ndivyo alivyotaka. Katika ujinsia tunapata chimbuko la maisha – yaani uwezekano wa mimba ya mtoto kutungwa na upendo mkuu zaidi kufanyika na kutokea. Hivyo basi ni juu yetu kutunza cheche hii ya uzima.

Kama tunataka kumkaribia Mungu na kugundua mpango wake kwa maisha yetu, lazima tuzingatie wajibu wetu kwetu sisi wenyewe na kwa wengine. Lazima tufanyie kazi uhuru ambao Mungu ametupatia. Hii ina maana tutulize vichwa vyetu na kuipasha moto mioyo yetu. Ni lazima tudiriki kuishi na kupendana.

Na lazima tuyafungue maisha yetu binafsi na yale yetu yalio ya pamoja kwa dhamiri njema. Hii ina maana kuwa ni lazima tujitunze sisi wenyewe na pia tuwatunze wenzetu – kihisia, kijamii, kisaikolojia na kimwili.



DENMARK

# Ujinsia na Kifo

ELIZABETH KNOX-SEITH

UKIMWI ni mchakato wenye mafunzo – una mlolongo wa matukio mazito lakini yasioungamanishwa na yanayotofautiana kwa msukumo usiyotabirika. Unaweza kuwa hai na mwenye afya nzuri siku moja na kutupwa tena kuurudia ugonjwa bila maonyo yoyote. Dalili mpya hujitokeza kila mara kiasi kwamba hata zile kanuni za kawaida zinazofahamika na madaktari haziwezi tena kubaini nini kinaendelea ndani ya viungo vya mwanandamu. Kila mtu ni wa pekee na kitu kimoja pekee ambacho mtu anaweza kukisema kwa uhakika ni kuwa hakuna awezaye kusema kitu chochote kwa uhakika.

- Je nitakufa kesho?
- Je ninaweza kuishi kwa miaka minne zaidi?
- Huenda
- Kumi?
- Ndiyo, inawezekana….

Haiwezekani wale wanaoishi na VVU kuyapanga maisha yao. Ugonjwa unaweza kutokea wakati wowote na kuwafuta toka katika uwanja – lakini kwa upande mwingine hakuna sababu ya maana ya kujiandaa kufa. Watu wengi wanaishi maisha mazuri yanayoendelea vema, ingawa wakati mwingine kuna shida kidogo za kiafaya – na kwa mazingira kama hayo inakera ikiwa mtu atakuwa ameacha elimu yake na vitu vingine vingi, kwa sababu tu ya kufikiri kwamba hataweza kuishi maisha marefu. Wengi wanabakia hai kwa miaka mingi – labda kwa muda mrefu zaidi kuliko ule tunaoujua leo. VVU na UKIMWI umejulikana tu kwa miaka 25, kwa hiyo haikuwa rahisi kukusanya takwimu juu ya maendeleo yake kwa kipindi kirefu zaidi.

Wakati ujinsia ni hitaji la kustawisha maisha, kifo ni alama ya namna maisha yanavyoisha. Katika tamaduni nyingi kifo hakichukuliwi kama hitimisho la mwisho la maisha, lakini kama mwanzo tu wa maisha mapya ila kwa njia nyingine. Lakini hata hivyo mchakato wa kufa unaweza kuonekana kama tukio la kutisha na la muhimu sana: ni kipindi cha mpito chenye kutisha kwa sababu kinajumuisha maumivu, mapambano na mashaka.

Ujinsia unaonekana kuwa umenaswa katika wavu wa mawazo yenye nguvu sana na yaliyo na upeo mkubwa, na hivyo inakuwa vigumu sana kuushughulikia zaidi kuliko kifo. Kifo ni tishio kwa maisha, tukizungumza kwa hali ya kimwili – lakini kwa kina zaidi kifo hakitishii uhusiano baina yetu na Mungu ama baina yetu na mambo yake. Kifo chaweza kuchukuliwa kama adhabu toka kwa Mungu, lakini kinyume chake zaidi chaweza kuonekana kama mlango wa kufika kwa Mungu.

Ujinsia, kwa upande mwingine una ugumu mkubwa kuushughulikia. Ni hitaji la msingi kwa maisha lakini muda huo huo kuonekana kama tishio katika uhusiano wetu na Mungu. Mvutano huu huonekana hasa katika desturi ya Kikristo – na tatizo hilo limeweza kutatuliwa kwa kusisitiza kuwa ujinsia unahusika tu ndani ya ndoa na umeandaliwa kwa ajili ya kujamiiana na kuongeza jamii. Katika desturi ya Kikatoliki hii imekuwa na sura moja na yenye msimamo mmoja kiasi kwamba vifaa vya kuzuia uzazi vimekatazwa, hata pale vinapotumika ndani ya ndoa. Ujinsia haukubaliki kama starehe mojawapo, na pia kama njia ya kugusana kwa dhati baina ya watu binafsi.

Ujinsia umeonekana kama 'mwiba mwilini', mfano wa mtu aliyefungwa na ulimwengu. Useja umeonekana kuwa ni njia iliyoonyoka zaidi ya kumwelekea Mungu, kutokana na hali kwamba wale ambao wameuchagua useja, kwa hakika wamechagua kujikomboa kutoka kifungo cha kiulimwengu ambacho hukuzwa na mahitaji ya kimwili. Kulingana na Paulo

**Tatizo la VVU na UKIMWI ni moja ya dalili ya mmomonyoko tulio nao leo. Hapo, upendo na mauti umeng'ang'aniana katika mkumbatio katili. Vijana katika kukata tamaa wanajaribu kutafuta upendo na ushirika, wakihatarisha maisha yao kufanya hivyo.**
HENRI NOUWEN

mwili ni hekalu la Roho Mtakatifu – lakini inaonekana kana kwamba hekalu hili linaweza kunajisiwa ikiwa ujinsia utaruhusiwa kujistawisha wenyewe katika starehe isio na kiasi. Kuidhibiti haja ya kimwili na kuishi tu ndani ya Mungu na kwa ajili yake tu yamekuwa ni madhumuni ambayo watu wengi katika vipindi vyote vya historia walijiwekea – bila kufikiria kuwa Mungu anweza pia kupatikana katika ujinsia.

Pale tukio halisi la kidunia kama vile UKIMWI linapojitokeza uwanjani haliwi jambo la kushangaza kuwa karne nyingi za mapambano ya kihistoria na maumivu yake zimeibuliwa tena. UKIMWI ni mfano wa matukio ya jinsi hiyo yaliyochochewa na hisia kwa sababu yanaibua maswali ya msingi na mara nyingi yanayobeba uchungu halisi wa kimaisha. Pale ujinsia unapounganishwa na kifo, upunguani unatokea katika akili ya mwanadamu, na hii kwa hakika ndiyo sababu ya ule wasiwasi wa kutisha ambao UKIMWI huweka ndani ya watu wengi. Uwezekano mkubwa wa kusambaa kwa maradhi unageuka kuwa uwanja wa vita dhidi ya ukandamizaji – na hapa lazima tuyakabili masuala yaliyopo ama sivyo yatafunikwa chini ya zulia.

## Tishio kwa Upendo

Ujinsia unatoa kielelezo kipana cha undani wa mtu. Ni msukumo wa kina toka ndani unaomsogeza karibu mtu kwa mwenzie, katika haja ya kuunda kitu kilicho kikubwa ambacho mmoja baina yao hawezi kukikamilisha peke yake.

Uundaji huu unaweza kuwa wa kuzaa watoto – lakini haiishii hapo tu yaani katika kutoa matunda ya kimwili ya ujinsia peke yake. Katika huba yake, na katika ukaribu wake, mpaka halisi unavukwa – ndipo ninapogundua kuwa mimi ni zaidi ya vile nilivyo, na hapo ufahamu mpya wenye kina ulio na thamani kubwa unafikiwa. Kwa ujumla hiki kiwango kipya cha kujifahamu mwenyewe ndicho kinachokuwa kusudi kubwa la ndani na lenye kupendeza la ujinsia.

Huko Kaskazini, tumekabiliana na ukimwi wakati ambapo uzoefu huu wa ujinsia umechanwachanwa na kusambaratishwa. Ujinsia umekuwa bidhaa mojawapo miongoni mwa nyingi na tunafanya biashara ya miili ya binadamu kwa njia za kushangaza, tukitumia alama na taratibu zilizo wazi kabisa. Hatuko pamoja tena kwa sababu za kukutana na mwingine katika hali ya uwazi juu ya haja iliyopo wakati huo – tunatafuta, kwa maumivu na kwa kukata tamaa, ili kuzithibitisha nafsi zetu, ujulisho wetu na maana yake. Ujinsia unakuwa daraja tunalotarajia kupita na kupata kile tunachokitafuta: uhakika kwamba tunapendwa, kwamba sisi ni zaidi ya kule kusikostahili tunaohisi unavamia nafsi zetu.

UKIMWI, haukuibukia kwenye utupu, lakini wakati ambapo upendo tayari umekuwa umeelemewa na kifo- si kifo cha kimwili ama cha nje, bali kifo cha taratibu kilichozama kwa kina ndani

yetu. Kifo hiki hutokea wakati ambapo hatuoni tena kupendwa kwa asili ya kawaida, na maana ya maisha na upendo huporomoka. UKIMWI unatugonga kama ngumi iliyotupwa vema, na kutua katika eneo laini katika fahamu zetu ambapo tayari pana vidonda ambavyo havijapona bado.

Shauku ambayo wengi wanayo kuhusu VVU na UKIMWI ni matokeo ya taswira ambazo tumezijenga katika fahamu zetu kwa miaka mingi ya majadiliano makali katika vyombo vya habari. Taswira nyingi hucheza cheza mbele ya mboni za akili zetu mara tu tunaposikia neno "UKIMWI". Na ni katika hizi taswira na si ugonjwa wenyewe kulipo na tatizo.

UKIMWI unanyofoanyofoa kamba ndani kabisa ya fahamu zetu: hofu ya kuangamia, hofu ya ujinsia....hofu ya kufedheheshwa na ugonjwa unaotufanya tusiwe na uwezo wowote wala nguvu ya kudhibiti chochote.

Kwa kweli kinachotuathiri ni ile sehemu ya ujinsia katika VVU na UKIMWI. Wazo kwamba ujinsia ni sehemu ya ulimwengu wetu halisi limekandamizwa kwa karne nyingi zilizopita, kiasi kwamba linazungukazunguka ndani yetu kama bomu ambalo halijalipuka bado – na pale ugonjwa hatari unaoambukizwa kwa njia ya kukutana kimwili unapojitokeza hutokeza pamoja na tabaka nzito la shauku na wasiwasi.

UKIMWI ni zaidi ya "maradhi" bali ni sawasawa na mkusanyiko mkubwa wa dalili zinazoweza kuchunguzwa na kufafanuliwa kwa taratibu za kiafya. UKIMWI pia ni "ugonjwa"- hali ya kijamii, kisaikolojia na kihisia inayosababisha mabadiliko makubwa ya ghafula. Si tu katika maisha ya watu binafsi lakini pia katika mchakato mzima wa kijamii wa kushirikiana na wa kupata maana ya mambo.

UKIMWI ni kichocheo cha kukusanya taswira nyingi za pamoja, mifano halisi na ile isiyo halisi ambayo inatangua kabisa namna tunavyofikiri juu ya maisha na kifo.

## Hatari ya Kuambukizwa Pamoja na Sifa Njema ya Mtu Binafsi

UKIMWI unagusa eneo laini kabisa – eneo nyeti kabisa la maisha ya binadamu, ambalo kupitia hilo maisha mapya ya kimaumbile yanastawishwa: yaani ujinsia. UKIMWI unasababishwa na VVU, ambavyo husambazwa kwa mbegu za kiume na damu – na hivyo majimaji haya ya mwilini yamehusishwa na ugonjwa hatari. Upendo wenyewe hauna maambukizi lakini inaonekana kana kwamba chanzo halisi cha maisha kinayo maambukizi hayo. Nguvu ya uharibifu wa kimwili inatutisha kama vile shetani mkorofi aliye ndani ya mwili. Ili tuweze kujadiliana namna ya kuzuia kuenea kwa UKIMWI, ni muhimu

# Upendo na Ujinsia

> Mengi yameandikwa katika Biblia na mengi yamesemwa Kanisani juu ya kumpenda jirani yako na wengine pia. Kuhusu upendo wa Mungu kwetu na upendo wetu kwa Mungu. Huu ni msingi wa imani ya Kikristo – na inasikitisha kwamba watu wa Kanisa wanaiogopa sana ngono. Ni kweli kuwa upendo wa milele wa kimungu kama tunavyoufahamu una namna isiyoshikika. Lakini tunapoishi maisha yetu tunakutana na namna nyingine ya upendo, upendo wa kijinsia. Na ninadhani tunapaswa kuzingatia hili kwa sababu unao nafasi ya muhimu sana katika maisha binafsi ya mtu ya kihisia na kifahamu. Ngono inaunda msimamo wenye nguvu ndani yetu kwa mfano dhana yetu ya Mungu ama imani yetu ya kidini. Ni kana kwamba watu wa Kanisa wanaogopa sana kipengele cha ujinsia kinachohusu nini hutokea watu wawili wanapokutana –na kwamba wao kwa ujumla wanakizungumzia  kama mfano wa kila kitakachoharibika. Badala yake wangeweza kusema tu, tazama jinsi gani inavyopendeza, ikiwa mtaruhusu kupendana ninyi kwa ninyi na kuonyesha hayo katika roho zenu, akili zenu na hisia zenu….. na pia kwa miili yenu. Na kisha kuyashika barabara yale wanayoyasema  ili kwamba isiwe tu maneno tupu nusu-nusu. Nafikiri ni huzuni kutenganisha ngono na upendo, kwa sababu vyote hivyo vinaenda pamoja, kwa kina kirefu ndani zaidi.
>
> USHUHUDA WA JESPER ALIYEKUFA KWA UKIMWI, DENMARK.

kuzingatia sababu kuu za kisaikolojia zinazoupatia ujinsia msukumo wake, ili tusifikiri tu kuwa tatizo linaweza kutatuliwa kiufundi kwa kusisitiza mahitaji ya kondomu, ama kimaadili kwa kuhubiri kujitenga mbali na ngono. Hatua yoyote kati ya hizo yaweza kufaa kutegemea mazingira tuliyomo na uchaguzi wetu wa aina ya ufumbuzi. Lakini hakuna yoyote kati ya hizo mbili inayozingatia kikamilifu uwanja wenye maumivu ya kihisia ambapo ujinsia unapatikana.

Kujitenga na ngono ama kutumia kondomu inahitaji uwezo kamili wa mtu kuilinda sifa njema ya utu wake – na hii kwa upande mwingine inahitaji utambulisho imara alionao mtu, yaani ufahamu wa kuwa mimi ni nani na ninataka nini. Kwa nyongeza inahitaji mtu kuwa na hamu ya kuishi – hiyo ni sawa na kusema namna mtu anavyoweza kujihudumia mwenyewe katika eneo lake. Kama mtu hana utambulisho wowote, haoni maana yoyote katika maisha akilini mwake, na hana ufahamu kuwa anayo haki ya kuishi maisha yenye heshima na yenye furaha – basi mazungumzo yote yanayohusu uamuzi wenye kutumia akili katika mazingira ya ujinsia  ni bure, ikiwa mtu anafikiria kutumia kondomu ama kujizuia kabisa na ngono.

Kwa maneno mengine, si rahisi kujadili kuzuia kuenea kwa VVU bila kuzingatia sababu za kijamii na kisaikolojia zinazochangia kuwepo kwa hali ambapo hatua za kibusara na kiakili hazichukuliwi kabisa. Utaratibu wa kueneza habari rasmi jinsi ambavyo mtu anaweza kuepuka kuambukizwa na VVU bila shaka unapaswa kupewa kipaumbele kikubwa. Lakini kwa nyongeza ni muhimu kuendelea zaidi. Hali ya kujiona duni iliyomo ndani ya watu wengi katika jamii leo ni sababu kuu ya kukosekana motisha wa mtu kujilinda mwenyewe na kuwalinda wengine – na jambo la msingi hapa ni kuwahakikishia kwamba makundi yaliyo katika hatari [kama vile vijana] wana mtandao maalum unaowazunguka, wenye uwezo wa kutoa huduma na wenye ufanisi mkubwa.


## Kupoza Mifadhaiko

Inajulikana sana kuwa mtazamo usioeleweka sawasawa juu ya ujinsia na kushindwa kuweka mipaka inayohitajika katika masuala ya jinsi hiyo mara nyingi imekuwa ni matokeo ya kukutana na udhalilishaji katika eneo hilo la ujinsia. Upendo wa kweli haupatikani tena, na mara nyingi umechanganywa na haja ya kujikabidhi mwenyewe kijinsia si katika himaya yake bali ya mwingine, bila masharti na bila mipaka. Nia ya ufahamu wa ndani wa kurudia rudia mfadhaiko uliotokea imekuwa kichocheo katika ujinsia – na maumivu yanapozwa kupitia ujinsia ambao kwa njia ya mzunguko umekuwa kioo cha ukatili ambao mtu ameupitia.

Uwezo wa kubeba matatizo ya watu wengine na kutoa huduma inayotakiwa, kwa mtu binafsi na hata kwa wengi, inaleta maana kuwa wewe kama mtu binafsi umepokea na unaendelea kupokea upendo wa kutosha na huduma inayoambatana nayo. Ikiwa hili halipo, utaona shida sana kuonyesha upendo, utulivu, na kujijali wewe mwenyewe na hata kuyajali mazingira yako kwa jumla. Utajiona kana kwamba haustahili kabisa upendo wa dhati na hata huduma yake pia - na unaweza kuishia katika mzunguko wenye uharibifu unaosababishwa na kujisikia kwa namna hiyo.  Ukosefu wa kujiheshimu unakufanya ushindwe kujiangalia mwenyewe na hata kulinda heshima yako - hususan katika masuala ya ujinsia.

Kwa wale ambao wanajiona kuwa wapweke, ngono inaweza kuwa njia pekee ya kupata joto na kujizatiti katika utu wako na hapo ndio inapowezekana kufikia matakwa ya mwenzi wako.

Nia yako huwekwa pembeni unachukua kile tu unachoweza kupata na huna madai. Unajiweka wazi kwa matukio yanayodhalilisha – lakini kwa wale ambao ni dhaifu kihisia, kutafuta ukaribu wa kimapenzi inaweza kuwa jambo kubwa kiasi cha kushindwa kutoa pingamizi.



Vijana wadogo wana hitaji maalum la kupata kila aina ya ushauri na msaada wa kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi – na ni muhimu kuwa na mtazamo wenye uwiano mzuri juu ya nafasi alizonazo kila mtu. Watu wazima wanaokutana na vijana kila siku wanalo jukumu rasmi hapa, kwa sababu maamuzi ambayo vijana wanayafanya hayachukuliwi katika siku moja. Matukio yaliyojaa hisia ya kupanda na kushuka yatazingatiwa- na tena itakuwa muhimu sana kuimarisha mioyo ya vijana katika kujiamini kwamba yapo maeneo yanayosubiri kufanyiwa kazi na mikono na miguu hii mipya. Upo utambulisho, nafasi ya kujaza, ingawa kuna ukweli kwamba kiwango cha kuishi kinachotarajiwa ni kifupi kuliko kile cha wengi.

## Ukaribu na Uhitaji

Kwa vijana wengi, hamu ya kumpata mpenzi na kuufurahia ujinsia na miili yao ni kichocheo kikubwa. Ndani ya mpenzi huyo wanakuwa na kioo kitakachowafanya waelewe utambulisho wao wenyewe na pia kutambua kwamba wanapaswa kupendwa – kupendwa kama mtu fulani tu na si kama mtoto mwema wa baba na mama. Kumgundua mtu ambaye siku moja watashirikiana katika kila kitu, katika hali yenye usawa kama watu waliokomaa ndio unaounda mchakato halisi wa kujikomboa kutoka kwa mikono ya wazazi.

Jitihada ya kumpata mwenzi wa mtu, ambaye ni kioo cha mapenzi chenye kumtambulisha ni ya msingi na ya undani kabisa ikitoa minyambulisho ya kuhamasisha maisha. Katika jitahada yao ya kuwapata wapenzi, watu wanaoishi na VVU na UKIMWI si kwamba tu wameambukizwa virusi, lakini wanazuiwa katika jitahada zao za kupata maisha wakiwa na  hamu ya kuzigundua nafsi zao kupitia mtu mwingine. Kile kilichohusishwa na hamu ya maisha, chenye haja ya kumwezesha mtu kujigundua mwenyewe na nafasi alizo nazo mtu katika hali yake halisi mara tu huhusishwa na kifo. Hivyo kinachotokea ni mabadiliko ya tabia ya mtu.

Kuwanyoshea watu vidole hakutakiwi hapa. Hakuna maana kusema. "kwamba ungeweza kusema hapana" – kwani nani angewaambia vijana wajiepushe na kufuata misukumo yao ya ndani kabisa, yenye nia ya kujipatia nafasi ndani ya maisha ya mtu mwingine? Ujinsia ni nguvu iliyo na peo nyingi zingine kuliko zile tunazofikiri, na upeo huu uliounganishwa na utambulisho, unapasawa kusahauliwa mwisho kabisa. Katika ujinsia tumewekwa pande mbili, na kuvutwa baina yetu na hivyo kufikia kujifahamu kwa namna mpya kabisa inayoshangaza.

Wengi wetu hatulijui hili – lakini hata hivyo imekuwa motisha ya kutuwezesha kuendelea kumtafuta yule ambaye anataka kuwa na umoja pamoja na sisi kwa ndani kabisa. Si wengi walio na ufahamu mzuri wa ndani wa kumpata mtu huyo mapema tu. Kwani wengi wetu utafutaji huo ni wa muda mrefu na mgumu, ingawa tunaweza kupata cheche za furaha na kutambuliwa. Ikiwa utapambana na VVU njiani, inaweza kuwa vigumu sana kustawisha mtazamo chanya katika ujinsia wako na kwa kila kitu ndani yako ambayo hapo awali ilileta maana na matumaini katika maisha.

Vijana wanaofanikiwa kupata utambulisho ulio dhahiri katika njia nyingine mbali kabisa na ujinsia wanao ulinzi bora zaidi dhidi ya VVU na UKIMWI kuliko wale ambao hawana. Wanacho kitu cha kuwasababisha watake kuishi, kitu cha kulinda na wanayo nafasi nzuri ya kusema hapana kwa ngono isiyo salama kuliko wale wenye utupu mkubwa katika tumbo zao wanaogopa kukataliwa. Nia ya kuwa pamoja na mwingine ili kuweza kujifahamu inaweza kuwa yenye kukatisha tama kweli kweli kiasi kwamba kondomu yaweza kuonekana kama kipingamizi na kikwazo kisichokuwa na maana.

Watu wengi walio na VVU wanaona vigumu sana kustawisha tena uwiano mzuri katika maisha ya kujamiiana, kumfikia mwingiine, kutafuta utulivu na upendo, wakati huo huo aki-



heshimu mipaka inayohakikisha ya kwamba wengine hawaambukizwi. Wengi huchagua kujitenga na kutotaka kugusana kimwili na yeyote – na kama wakifanya hivyo, basi itahitaji ujasiri mkubwa kuwaeleza wapenzi wao kwamba wanavyo VVU. Hicho si kitu cha kwanza unachokiongelea mnapokutana wawili, na hata pale mnapochagua kufanya ngono salama swali huja kama kweli na ni lini uhusiano wenu utakuwa wa kudumu zaidi. Nitaelezaje kile ambacho bado sijakieleza kwa mwenzangu? Na ni kwa njia gani nitaeleza kwa nini sikukieleza hapo awali? Hofu ya kukataliwa, na ya kutokueleweka inakufanya ujisikie haupo huru kusema chochote

## Wajibu Uliopo

Njia yenye nguvu na yenye kuwa na matokeo bora ya kuzuia kuenea kwa maambukizi ni kuwawezesha watu binafsi kujiepusha na chaguzi zinazomsababisha mtu ajiletee madhara. Ikiwa una upendo wa nguvu ndani ya moyo wako hivyo basi haupo tena katika mashaka mengi ya jinsi ya kukutana nao – na utaweza kujihisi mwenyewe kuwa mwenye thamani kubwa kuwa na uhusiano usiokuwa na makubaliano ya msingi ya kuhudumiana.

Ingawa mtu mwingine anaweza kuvaa vizuri na kushiriki mbio za kimaendeleo wanaweza kuwa laini sana kwa ndani – na tunapozungumzia ulinzi dhidi ya VVU na UKIMWI kwa vijana ni muhimu kuwa wachunguzi. Hii ni kweli ikiwa wewe ni mtu uliye na mawasiliano na vijana kwa kipindi kirefu, ama u sehemu ya mtandao wao, kama familia ama rafiki, kiongozi wa vijana ama mwalimu. Viongozi wa vijana Kanisani wanayo jukumu rasmi – kwani Kanisa ni nini ikiwa si kimbilio la wale ambao hawatadiriki kuwa wazi juu ya matatizo yao ya binafsi mahali pengine?

Tukizungumzia, kuhusu UKIMWI, wewe unakuwa katika upande mwingine usio sahihi ikiwa utadhani upo nyumbani na mkavu kweli kweli ikiwa tu utataja "salama" na "ufumbuzi wenye busara" - kama utaegemea matumizi ya kondomu ama kujiepusha na kujaamiiana, kulingana na fikra zako juu ya maadili na ujinsia. Inaweza kuwa muhimu sana kujadili mambo ya ku-

**Mapenzi ya Mungu ni kuvunja unyanyapaa, aibu, kukataa ubaguzi na mambo yote yale yanayokana maisha. Zambia imepata taabu sana kutokana na ukimya wa kithiolojia juu ya suala zima la VVU na UKIMWI. Tunapaswa kukabili masuala mawili ambayo Makanisa yetu ya leo na tamaduni zetu tulizorithi, zote za Kiafrika na za Kimagharibi, zimeshindwa kubeba wazi wazi na kwa mpango mzuri kifo na ujinsia. Je ni kwa namna gani VVU, "silaha za maangamizi", ziwe karibu sana na zimeunganishwa na silaha ile ile inayotumika kuendeleza vizazi kijacho?**

JAPHET NDHLOVU

fanya wazi wazi kwa watu binafsi, na kutoa njia mbadala kwa vijana – lakini pia ni muhimu kutojaribu kuwashawishi kwamba ipo njia moja tu na finyu ya kuenenda.

Chochote kile kinachosemwa, watachagua kuishi maisha yao kwa msingi wa hali walizo nazo ndani yao – ndiyo kusema, mtazamo wao wenyewe wa maisha ambao wamepewa kupitia malezi yao, mazingira ya kijamii n.k. Wale wanaojiona kuwa wamekandamizwa na kuachwa katika familia zao mara nyingi wataitika kwa maasi – ambayo ni kusema wataenenda katika njia tofauti na zile ambazo wazazi, walimu, ama wengineo wamejaribu kuwashawishi kuenenda. Habari zote kuhusu UKIMWI lazima zitolewe katika mazingira ya vijana, kuanzia hali halisi waliomo, sasa na wakati huu tukizingatia kwa hisia kuu huzuni, maumivu na saburi ambayo kila mtu anabeba ndani yake kwa njia yake mwenyewe.

Mtenda kazi bora wa UKIMWI ni yule anayelifuata kwa karibu kundi la vijana kwa kipindi kirefu ili kwamba aweze kuelewa kwa sehemu hali ambayo kila mmoja yumo, kuichungua mioyo, mawazo yanayotekelezeka, na matukio yaliyotokea ya ujinsia. Kanisa linatakiwa kama mahala mbadala pa kulaza mgongo kwa vijana wasiojua waende wapi wakiwa na haja kubwa ya ushirika utakaowasaidia kuvuka vipindi vya matatizo. Kipo kilio kikubwa kupata viongozi walio wazi na wasikilizaji wazuri na ambao huguswa hata na mambo yale yasioelezeka kirahisi kwa maneno.

Ni jukumu kuu kuwapa msaada vijana, ili waweze kupata ukomavu ndani mwao utakaowawezesha kufanya maamuzi chanya, si tu kuhusiana na ngono, lakini kwa jumla. Tatizo ni kuwa mara nyingi watu wazima wameshindwa kufikia viwango hivyo vya ukomavu, na kwa kweli wao nao wameharibika na kushikwa na hofu kama walivyo vijana. Uwezo wao wa kujizuia umeweza kujengeka katika miaka kadhaa – lakini kwa upande mwingine wanaweza wasijue usuluhisho mwingine wowote ule zaidi tu ya udhibiti. Uwezo wao kuchukuliana na kusikiliza u mfinyu hali kadhalika uwezo wao kusaidia.

Katika duru za kikanisa ni muhimu kuwa na ufahamu na ulimwengu wa ndani unaochoma wanamoishi watu wengi. Mahitaji ya kimaadili yanayofikirika yanaweza kuwa sahihi kama mahitaji unayojiwekea mwenyewe, lakini unapojaribu kuyashindilia ndani ya koo za watu wengine bila kuzingatia ni hali gani wanamoishi, basi matokeo yake hayataridhisha. Katika hali mbaya kabisa unaweza kushindwa kutekeleza wajibu wako kusaidia na kupunguza mateso – katika hali iiyo bora utawatenga wale wanaohitaji msaada wako, kiasi kwamba wataenda mahali pengine wakitumaini huko wataeleweka zaidi.

Watu wengi, vijana kwa wazee, wanapungukiwa na mtandao utakaoweza kuwasaidia kupita vipindi vya misukosuko ya kawaida kabisa. Kanisa, katika hali yake ya asili kama lililo na nguvu, na jumuia yenye uhai, lazima liwe ushirika ambao watu wanauhitaji kwa nguvu sana – lakini kwa kweli hilo ni jambo ambalo kwa bahati mbaya liko mbali sana na ukweli.

Msingi wa Kanisa ni maono ya ndani, maono ya dhati kabisa ya jumuia ya binadamu inayovuka mipaka yote, ushirika ambao unawapa pia watu binafsi maana na uponyaji wa kiroho. Kupitia historia yake ndefu, kanisa limekuwa hivyo lilivyo – lakini limekuwa vinginevyo pia.

VVU na UKIMWI ni changamoto na kilio kwa Kanisa kustawisha jumuia zenye maana – ni makao kwa wale ambao hawajisikii kuwa nyumbani ndani yao. Mkono unahitajika, mkono unaoufikia moyo kwa kina kirefu – ndani ya mioyo iliyovunjika katika kivuli cha kukataliwa. Fujo na machafuko lazima zibadilishwe na kuwa nzima zenye mwingiliano mzuri ikihusiana na undani wa watu na maisha yenyewe.

Hii haihusishi ujenzi wa uzio kuwazuia watu binafsi katika kujieleza, lakini kinyume chake kujenga imani kuwa kila mmoja anayo maono kwa ajili yake na maisha yake. Na kwa msingi huu, ujasiri katika mapenzi unaweza kukua – na tukiwa na uwezo wa kuuongoza ujinsia, ili kwamba haibaki tena kuwa uwanja wa vita wa ukandamizaji bali chanzo cha maana cha maisha.

Dhana

asili

kufaa

# Kanisa lililokamilika

MADA. KAMATI MAALUM YA BARAZA LA MAKANISA KASKAZINI MWA ULAYA NA KUSINI WA AFRIKA

Katika suala zima la VVU na UKIMWI Kanisa limepokea shutuma nyingi sana juu ya nafasi yake ya mbele katika eneo la huduma na msaada. Limelaumiwa na kufananishwa na jitu kubwa lililolala; kwa kueneza na kuchochea unyanyapaa na mitazamo mingine iliyojengwa juu ya hofu na ubaguzi; kwa kutamka hukumu kali za kimaadili kwa wale waliombukizwa; kwa kuzuia juhudi za ulimwengu nje ya kanisa katika kuzuia, na katika kuyashusha masuala ya UKIMWI hadi yakawa matamko rahisi ya kimaadili. Makanisa hayajatambulika kama mahali pa makimbilio na faraja, bali mahali pa kuwatenga wale wote ambao "wapo pale nje" ambao kwa kifupi "wanateseka kutokana na kuyaharibu maadili yao wenyewe na dhambi'.

Kama vile VVU na UKIMWI una matokeo ya kina katika kila fani ya maisha katika jamii, ikiwa pia umebeba mateso na huzuni nyingi, kuna haja kubwa inayoendelea kukua, kwa kanisa kuirejea mizizi yake kugundua tena hali yake halisi - yaani ina maana gani kuwa Kanisa - na kwa njia hii kuwa na manufaa zaidi katika zama hizi za VVU na UKIMWI.

## Tatizo

Kanisa la leo, kwa njia nyingi limepoteza dira ya wito wa awali wa kupenda na kupendwa na Mungu. Mara nyingi limejaribu kufanya kazi kwa kujitenga kabisa na masuala mengi yanayoikabili dunia ya leo, mara kwa mara VVU na UKIMWI umetazamwa kama tatizo la kiafya na si la kiroho, bali la kijumuia. Lakini kile kinachoathiri mtu mmoja kinawaathiri wengi, "kwani sote ni mwili mmoja katika Bwana".

Tatizo la kuwa na njia mbili limeleta vikwazo baina ya watu wote ndani na nje ya kanisa. Mtazamo wa "sisi" na "wao" umesaidia sana kugawa badala ya kuponya na kuunganisha. Na uhusiano mkubwa baina ya ngono na dhambi husababisha dhana ya wengine kuhukumiwa kama "wenye dhambi" wanaostahili adhabu.

## Watu Walio Jumuia Moja – Kanisa la Msingi kabisa

Makanisani mara nyingi tunayo taswira hatari ya sisi kuwa maalum sana kana kwamba tu bora kuliko wengine. Kwa njia nyingi mbalimbali tumeunda "sisi" na "wao", tukijitenga wenyewe kana kwamba hatumo tena ulimwenguni. Tunahitaji kuelewa kuwa ina maana gani tunaposema Kanisa lililokamilika. Kwa nini watu wanaoishi na VVU na UKIMWI hawaji kwa uhuru na kwa uwazi kanisani? Kwa njia ile ile ambayo Yesu alijifananisha na wale ambao maisha yao yalikuwa yameharibika kabisa, akikaa mezani na watoza ushuru, wenye dhambi na wagonjwa, sisi kama Kanisa nasi tumeitwa kujiweka katika mazingira yale yale na wale wanaodharauliwa. Kanisa lazima lianze na wale ambao Yesu alihusiana na kukaa nao – waliotengwa, waliokataliwa, waliokandamizwa na watu wenye shida. Watu walio katika hali hizi za kimaisha si lazima wawe vifaa vinavyotoa kielelezo cha matendo yetu mema. Hawa hawapo pale kutupa sisi sifa njema mbele za Mungu. La! Kinyume, ni pale tu tunapojikuta katikati ya mazingira ya jinsi hiyo ya maisha yetu ndipo Mungu hujifunua kwetu. Hii inahitaji mshikamano wa dhati baina ya binadamu wote wenye shida.


Tumejifunza pia namna ya kusoma maandiko kupitia macho ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI; kuendeleza thiolojia ya huruma, kukubalika na kujumuishwa na kuandaa utaratibu wa ibada unaofaa kwa ajili ya kusudi hili.

## Mtazamo kamili wenye msingi wa Kristo

Upo msukumo pia wa kanisa kugawa maisha katika pande mbili, yaani yale ya kiroho na yale ya kimwili – hili la kwanza likichukuliwa kama ndilo hitaji kuu la kanisa na si lile la mwisho. Kanisa linahitaji kukombolewa kutoka msimamo huu wa njia mbili. Yesu alikuja ili tuwe na uzima, na tuwe nao tele – na hii inahusu kila kipengele cha maisha ya kibinadamu. Kanisa lazima liwe kamili katika mwelekeo wake wote, ikiwa na maana ya lizingatie eneo zima linalohusu huduma.

Katika kutafuta utambulisho kamili wa kanisa – yaani nini kilichopo katika moyo wake – chanzo chenye maana chaweza kuwa zile Injili – katika maisha ya Yesu Kristo. Tunahitaji kuangalia alifanya nini, nani alikutana naye, jinsi gani alihusiana na watu, jinsi gani alisikiliza, nini alisema, jinsi gani mtazamo wake ulikuwa na namna gani alipatikana mahali fulani. Kwa mfano katika barabara iliyoenda Emmaus. Yesu alitembea na watu walioteseka alikuwa pale kwa ajili yao.

Yesu alipenda pasipo masharti yeyote. Hii tunaamini inatuonyesha roho halisi ya *diakonia* - kuishi na, kutembea na, kugusa, kuelewa, kushirikiana, kuhudumiana na "kupambana bega kwa bega". Kinachowaathiri waume kwa wake, watoto na vikongwe - tulioumbwa kwa mfano wa Mungu - kinaathiri Kanisa na hivyo kuwa hitaji la kanisa.



## Kanisa linalosikiliza

Ili kuwa na manufaa kwa maisha ambayo wanawake na wanaume wanapitia siku hizi, na kuandaa nyumba yenye ukarimu na inayotoa faraja na mahali pa makimbilio kwa WOTE wenye mahitaji, kwanza inatubidi kupatikana mahali na tayari kusikiliza: kusikiliza kilio cha watu wa Mungu, kusikiliza mahitaji yao, kiu yao na njaa walio nayo.

Kule "kutenda" lazima kutokane na kule "kuwepo": tunapaswa kuwa binadamu "waliyopo" kabla ya kuwa binadamu "watendaji": zaidi "KUWA" Kanisa kwa ajili ya watu wenye shida kabla hatujaanza kutenda na kuzungumza lolote. Tunaamini ya kwamba huu ndio uinjilisti wa kweli – kumfanya Yesu hai na kuwapa matumaini na faraja watu wote wenye mahitaji. Mahubiri ya Kristo kuwa ni Neno yanahitaji kuanza na Mwili wa Kristo. Hatuwezi, katika sifa njema, kuhubiri Neno bila kuutambua Mwili wa Kristo.

## Kuwa Mwili Mmoja

Kama vile Kristo asivyogawanyika, hali kadhalika sisi kama Kanisa hatuwezi kugawanyika. Changamoto tulio nayo kwa sasa ni kubwa sana kiasi kwamba hatuwezi tena kuendelea kubakia tumetengana. Mmoja wetu anapopata mateso, sote nasi tunateseka vivyo hivyo. Muda wa *kairos* tulio nao sasa ni fursa ya kujenga *ekumenia* ilio ya kweli, na kupata Kanisa moja la kiulimwengu - Kaskazini na Kusini, Mashariki na Magharibi. Mwisho wa yote inatubidi kufanya kazi pamoja na watu wote wenye nia njema.

Kanisani mara nyingi kumekuwa na tuhuma kwa wale wasio wanachama wa "jumuia yetu hiyo ya Kanisa", hali ya kushindwa kuchochea mazungumzo na kubadilishana uzoefu, kushindwa kujifunza baina yetu na kuwasiliana na wengineo ambao tunaweza kujifunza mengi toka kwao.

Kuhusiana na VVU na UKIMWI, kukosekana kwa taarifa sahihi na stadi bora kumesababisha mitazamo yenye hukumu, lugha inayonyanyapaa, tabia inayobagua wengine na ukimya juu ya masuala ambayo ni vigumu kuyajadili kwa wazi kanisani.

Uongozi unahitaji mafunzo, maelekezo, vifaa, habari sahihi na mitandao bora. Unahitaji pia nia ya kutaka kushirikiana na wengine wanaoshughulika kwa matokeo mazuri, na utayari kushughulikia hofu zisizo kuwa na msingi pamoja na ubaguzi. Kwa nyongeza, ulimwengu umekwisha tambua umuhimu wa kuyashirikisha makanisa kwa sababu yapo katika jumuia ya watu, sifa yalizo nazo, mamlaka na kibali

## Nuru ya Ulimwengu

Kanisa limeitwa kuwa "chumvi ya dunia", na nuru si kwa ajili yake peke yake, lakini kwa dunia. Ili kuwa nuru kama mshumaa unaowaka ina maana ya kujitoa mhanga mwenyewe katika huduma. Kuwa nuru, kuishi maisha yetu nuruni, ina maana pia kuishi katika mtazamo chanya, na kuuvunja ukimya uliopo juu ya masuala yale ambayo mara kwa mara hatupendi kuyaongelea, kama vile ujinsia. Kanisa pia lina wajibu wa kuanza kuyazungumzia masuala ambayo yanachochea ugonjwa huu unaosambaa kama vile umaskini, fursa zinazotofautiana za kuyafikia mambo, unyanyasaji wa kijinsia, ukatili majumbani, haki za kijinsia na mabadiliko ya kiutamaduni, baina ya mambo mengi. VVU na UKIMWI vinatupa changamoto katika misingi halisi ya imani zetu. Kuyaibua masuala hayo katika mahubiri yetu, katika hali inayogusa watu na kwa huruma za kutosha itasaidia kuuvunja ukimya uliopo.



Kanisa haliwezi kuendelea kuzika kichwa chake mchangani. Je kanisa lawezaje kuwa jamii inayoponya?

**ZAMBIA**

# Kanisa Linaloponya

JAPHET NDHLOVU

Kanisa nchini Zambia, kwa pamoja na Kanisa lote kusini mwa jangwa la Sahara, haliwezi kuvumilia kuzika kichwa chake mchangani. Athari za VVU na UKIMWI zinaonekana katika rika zote za jamii. Hii imekuwa ni tishio katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya mwanadamu kwa kushambulia rika ambalo ni la wazalishaji na kurudisha nyuma umri wa kuishi na ukuaji wa watoto. UKIMWI ni jangwa la kitaifa. Haliwezi kudhibitiwa bila kuunganisha sekta zote ndani ya nchi. Kanisa la Zambia linatakiwa kufanya kinga dhidi ya UKIMWI jambo ambalo ni la lazima kupewa kipaumbele. Kwa kuwa baadhi ya waumini wa Kanisa wameathirika kwa UKIMWI tunaweza kusema kuwa Kanisa – mwili wa Kristo una UKIMWI.

Lakini Kanisa, kwa asili na mafundisho yake ni jumuia inayotunza na kujali na inatakiwa kujihusisha kwenye mikakati ya kutimiza mahitaji ya mwanadamu. Kanisa kama mwili wa Kristo limeitwa kuwa hodari na tofauti. Kutokana na maradhi ya VVU na UKIMWI, kanisa limeitwa kupambana na ubaguzi, unyanyapaa, chuki, udhalimu na dhuluma. Kanisa linatakiwa kuwa mwakilishi wa Yesu kwa kuhimiza kuwatunza, kuwapenda, kuwahurumia wagonjwa na wenye taabu, kuwatambua walioathiriwa na walioathirika katika jumuia, kuwajibika, kusema ukweli na kuishi kama nuru ya ulimwengu (Math 5:13-16).

Kwa mapana yake makanisa ya Zambia hayajajihusisha na tatizo la VVU na UKIMWI kiasi cha kutosha. Mara chache, semina zinafanyika, madaktari hualikwa kuzungumza lakini hakuna mwitikio wa kithiolojia uliokwisha fanyika. Mbali na wajibu wa kutunza uliokwisha fanyika, miongoni mwa jumuia za wanawake, na zaidi ya wanawake wanachama katika kanisa, Makanisa yetu yanaonekana kutojali. Madhabahu imekataa kuhubiri mateso haya ya mwanadamu. Unachoweza kusikia ni shutuma na ibada za kuhukumu (hasa juu ya matumizi ya kondomu kama kinga) na siyo mapendekezo ya namna maradhi haya yanavyoweza kudhibitiwa.

Kukosekana kwa vikundi vya kusaidia katika makanisa ni changamoto kubwa kwa kanisa iwapo litajihusisha kikamilifu dhidi ya VVU na UKIMWI. Ukosefu wa vikundi vya masaidiano katika jamii za kiimani kunachangia shutuma. Jamii za kiimani zinatakiwa ziwezeshwe kutambua matakwa ya Mungu katika hali kama ile inayosababishwa na UKIMWI.

Tatizo linachangiwa na ukweli kuwa katika vyuo vya thiolojia ambako wachungaji hufundishwa, mitalaa na namna ya kushughulikia VVU na UKIMWI imeanzishwa hivi karibuni. Watumishi waliofundishwa kabla ya kuanzishwa kwa mitalaa hii ni wengi na ipo haja ya kuharakisha kuwafundisha. Hii peke yake inaleta changamoto mpya.

Kuwepo kwa VVU na UKIMWI katika jamii ya Zambia, hasa na siyo katika kanisa pekee, inawataka wakristo kutafuta wao ni nani na namna gani wanaitikia katika kushirikishwa na haki. Wakristo hawakuitwa kutoa sadaka kwa wale ambao miili yao ina virusi. Kanisa linawapa changamoto kukubali kuwa virusi vimeingia katika mwili wa Kristo, na wanatakiwa kuitikia haraka mikakati inayoonekana na yenye uhakika. Kukataa, woga, usaliti, upotoshaji, kutaka sifa na ujinga vimekuwa ni vikwazo vikuu katika kushughulika na VVU na UKIMWI.

**Huwezi kumdanganya Mungu, lakini kwa watu unaweza kujaribu. Kwa miaka miwili nimekuwa na siri yangu. Miaka miwili katika hali ngumu kisaikolojia, kiroho na hisia. Miaka miwili ya uongo, sababu na mfadhaiko. Miaka miwili iliyonipeleka mbali, mbali na marafiki na familia, kwenye baridi, giza la upweke. Nililikimbia kanisa. Nikatengwa.**

PREBEN BAKBOSLOTH, ANAISHI NA VVU, DENMARK

## Matendo ya Uponyaji yaliyofanywa na Yesu

Agano jipya linaonyesha uponyaji ulivyofanywa na Yesu. Uponyaji ni sehemu ya kuweka utaratibu mpya katika jamii. Unatangaza wokovu. Unadhihirisha haki. Unathibitisha *Shalom*, kusudio la Mungu juu ya ukamilifu wa uumbaji.

Tofauti na ilivyo, uponyaji mwingi unaofanywa na makanisa leo uko mbali na utaratibu. Badala ya kushuhudia utaratibu mpya unaoendana na kweli ya Mungu ni rahisi kuanzisha makubaliano yasiyo na utaratibu katika mfumo uliopo.

Mara nyingi wanadamu wamefungwa katika maana zao nyembamba kuhusu huduma za afya, mtazamo finyu na kuanzisha taratibu za maisha zinazokataa ukamilifu wa injili. Afya inapokuwa suala binafsi, wakati watu wanapoahidiwa na vivutio vya matumaini kutokana na kukukua kwa teknolojia, inaposhindikana kuunganisha huduma za afya na haki kwa jamii na inapokanushwa kwamba uponyaji una uhusiano wa asili na utunzaji wa dunia, basi, hii ni alama tosha kwamba kuna upinzani katika maana ya kibiblia ya afya, uponyaji na ukamilifu.

Toka mwanzo wa biblia, ni wazi kwamba uumbaji ni mmoja, unaobainika kuwa ni mwema, na unaoonyesha wazi kumtegemea muumbaji wake. Dhumuni la Mungu la uumbaji linajieleza ndani ya maono ya *shalom* katika Agano la Kale: *Shalom* ni neno linaloonyesha utimilifu, ukamilifu, upatanisho na amani inayoonyesha tabia ya dunia na vikaavyo ndani yake. Huu ni mzizi wa maana ya afya katika biblia; unatoa msingi wa uelewa wa wokovu katika agano la Kale. Neno hili *Shalom* si la mtu binafsi bali la wote, lijulikanalo katika jamii. Si la kati ya watu, lakini linaunganisha haki ya mahusiano kwa uumbaji wote. Lengo lake si utawala na mamlaka kwa mwanadamu, bali kuwa sifa na utukufu kwa Mungu.

Yesu Kristo alikuja kama mwana wa mfalme wa *Shalom*. Amani ndani ya mwili wa Kristo – iwe ishara kwamba uumbaji umekombolewa. Utawala wa Mungu utakuja duniani. Hapa ni msingi wa huduma ya kanisa ya uponyaji – uponyaji wa mtu, uponyaji wa jamii, uponyaji wa dunia, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Maana ya kanisa kama jamii iponyayo imejengwa katika kuamini kwamba mwili wa Kristo ni wa ulimwengu wote na wa kweli kiimani. Wakati jamii zinaweza kuwa na maono na njia tofauti za kufanya pamoja kutimiza malengo yao, mwishowe zote zipo ili kuponya mataifa.

## Huduma ya Uponyaji

Kama nyakati za Yesu, huduma ya kanisa ya uponyaji leo lazima ijengwe katika mazingira yanayoendana na maisha ya watu. Hakuna namna ya hitaji la kibinadamu, hakuna eneo la maumivu lililoangukia nje ya huruma ya Yesu.

Katika Agano Jipya tunaonyeshwa mwili na damu , Yesu ambaye anajikuta katika ugomvi juu ya huduma yake ya uponyaji na mafundisho ndani ya hekalu. Mguso wa Yesu ni mguso wa uponyaji wa mtakatifu kupita wote. Amezaliwa katika dunia ambayo magonjwa na mateso yametapakaa. Mwanzoni kabisa anagundua kuwa mamlaka ya hekalu kuhusu utakatifu yatasimama katika njia ya kazi zake za uponyaji. Yesu ataamua ama kufuata sheria za Torati na hekalu au kumtii Mungu.

Yesu alifafanua upya maana na kazi za utakatifu. Kwa Yesu, utakatifu ulihusu kuingia katika maisha ya wengine. Utakatifu ulikuwa tendo la kujishughulisha, siyo hali ya kujitenga. Ndani ya Yesu, utakatifu ulichukua mateso ya wengine: Utakatifu unahusika na unyenyekevu, upole, kudharauliwa. Ndani ya Yesu, mguso wa uponyaji wenye utakatifu ulikuwa ni mguso wa ndani na ushiriki: mguso uliosema 'u mali ya'.

Katika dunia iliyopumbazwa na fikra za mateso yanayosababishwa na dhambi, Yesu aliingia, kujali magonjwa na mateso kama njia ya mtu kuonja huruma na upendo wa Mungu. Katika dunia iliyowahukumu wengine kama wenye dhambi na watengwa na wengine, alikuja mtu huyu Yesu, ambaye, katika kusamehe dhambi na kutakasa mkoma, alionyesha Ufalme wa Mungu ulivyo wa haki na rehema.



Katika historia, sheria za usafi zilisababisha mipaka ya nje kinaganaga kati ya watakatifu na wasio watakatifu, waliosafi na 'wachafu'. Wasiokuwa na unajisi, wasafi na watakatifu walikuwa makuhani na Walawi, wale waliohusika na huduma katika hekalu. Mwishoni mwa mpangilio alikuwa ni mwenye ukoma. Akitengwa kama ambaye unajisi ulimtawala, mkoma alikuwa akiogopwa sana: ambaye alitangazwa kwa maneno 'mchafu, mchafu'.

Ndani ya dunia kama hiyo Yesu alikuja akamshika mwenye ukoma. Katika dunia kama hiyo Yesu alikuja na kuleta taswira ya utakatifu iliyotafsiriwa si kwa kutengwa kwa kile kilichochukuliwa kama kichafu, bali kwa kuwa karibu nacho. Katika dunia iliyogawanyika na kutengana yenyewe alikuja Yesu, ambayo, kwa mguso wa mkono wake, aliirejesha jamii.

Jasiri na mwenye msimamo mkali huyu Yesu alikiuka taratibu za utakatifu. Alikataliwa, akalazimishwa kuwa nje ya miji katika vijiji na mapori kwa sababu ya kushirikiana na kugusana na mkoma. Alibezwa na hekalu kwa sababu alisamehe dhambi za watu. Yesu huyu mwenye miujiza ya uponyaji ni Yesu ambaye wengi wamemsahau tangu mwanzoni mwa mlipuko wa UKIMWI.

Mwanzoni mwa miaka ya 1980 na 1990 wengi walijisikia kutakiwa kuhubiri hasira ya Mungu, kuongea maneno ya Mungu juu ya hukumu na laana; kwa kutangaza kuwa UKIMWI ni adhabu ya Mungu juu ya dhambi. Hii ilikuwa ni kinyume kabisa na Yesu wa miujiza ya uponyaji, aliyepo daima na wagonjwa na wenye mateso; Yesu aliyejionyesha yeye mwenyewe na upendo wa Mungu usio na masharti katika mahali ambapo uumbaji wa Mungu ulikuwa katika uchungu. Kama Yesu aliye katika historia angekuwepo kimwili leo, angejionyesha yeye mwenyewe amevaa alama ya uvimbe inayoonekana. Kwa ukamilifu, kwa ujumla, bila kukwepa ingekuwapo alama yake na wale wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Miujiza ya uponyaji katika Agano Jipya inatuletea Yesu Kristo aliyevunja vikwazo, aliyechukua hatari inayotupa changamoto leo. Yesu alihatarisha vyote, bila masharti, kwa ajili ya jirani, bila woga kwa ajili ya heshima yake. Alihatarisha maisha yake na akayapoteza, na akarudi kufafanua ahadi ya maandiko kuhusu uzima wa milele. Changamoto hii ya Yesu haipatikani katika kipindi hiki cha miungano ya kiimani (kairos). Yesu anapatikana katika kila uso wa anayeishi na VVU na UKIMWI. Kama kanisa likijaribu kujishughuiisha kwa karibu na watu waishio na VVU au UKIMWI, uelewa wa ndani kuhusu upendo utakuwepo. Ukimwi umeufundisha ubinadamu vitu kuhusu upendo unaovuka mipaka ya migongano ya makanisa kwa karne zote. Janga la UKIMWI limelipa kanisa wasaa wa kujifunza kuhusu tabia za upendo unaohimili na kudumishwa katika magonjwa na afya, na kujifunza kusaidiana na kupendana sisi kwa sisi katika nyakati nzuri na mbaya, Katika jamii ya waaminio UKIMWI umeleta uzoefu katika upendo ambao ni mkuu kuliko kitu kilichozoeleka, eleweka au kilichoumbwa. Katika nyakati za maumivu, masumbuko, woga, upweke na hasara kanisa hushikwa na upendo kama huu.

## Jamii Inayojali

Kanisa linatakiwa kujali huduma yake ya uponyaji katika kipindi hiki cha mlipuko wa UKIMWI. Makanisa yanatakiwa kufanya

**Kanisa – kwa undani na mtazamo wa dunia siyo taasisi, muundo au dhehebu. Kanisa ni jamii – jamii inayoshuhudia upendo wa Mungu ndani ya maisha ya watu. Ni jamii inayojaribu kumtumikia Kristo katika dunia ambayo kila siku inaona familia ya mwanadamu ikidhihakiwa, ikiharibika na kuteswa. Kanisa ni mkusanyiko wa kijamii unaokumbuka, fuata na kumtumikia Kristo aliyekuwa mtu wa huzuni, aliyekataliwa na kudharauliwa.**

JAPHET NDHLOVU

maagano ya kutunza, dhana iliyorahisi na iliyojijenga katika Agano la Kale na Agano Jipya.

Kwa kishindo kikubwa kuna ukweli wa kijamii na kisiasa unaolikabili Kanisa la Zambia leo kwamba kuna haja ya kusisitiza juu ya tatizo la UKIMWI katika hali ya kutengwa na mlolongo wa matatizo ambayo ndicho kiini. Umuhimu wa tatizo la UKIMWI hauwezi kupuuzwa, bali kuwekwa katika mtazamo mzuri. Mbali na tatizo la virusi, vitu ambavyo watu wa Zambia wanapitia vinaonyesha matatizo ambayo yamezibwa kwa viraka na vitambaa au yamepuuzwa moja kwa moja.

Kwa ukamilifu, huduma kwa watu waishio na VVU na UKIMWI lazima ihusishe huduma za afya na jamii zilizoandaliwa kuboresha ubora wa maisha, kuongeza uchaguzi wa mtu na kupunguza huduma za taasisi na za ki-hospitali. Huduma za kuhudumia wagonjwa nyumbani zitolewe kwa huruma kiasi cha kuruhusu watu waishio na VVU na UKIMWI na wapendwa wao waishi kama wamoja na watoa huduma. Wale waliowahudumia watu wenye VVU na UKIMWI wanaelewa kuwa ugonjwa, hasa katika hatua zake za mwisho hutoa changamoto ngumu na zenye tabia tofauti. Kwani virusi hukaidi kuwa katika sehemu moja ya mwili au kukubali aina moja ya matibabu.

Uangalizi pia unatakiwa kutofautishwa miongoni mwa makundi tofauti. VVU kwa wanawake hujionyesha tofauti kwa wanaume; na kwa watoto VVU hujionyesha tofauti kama inavyojionyesha kwa watu wazima. Utata wa tabia za virusi unaweza kusababisha changamoto ya kipekee. Wale wenye VVU wana mahitaji pekee ya kijamii na kisaikolojia kutokana na asili ya kutisha kwa ugonjwa na kunyanyapaliwa baada ya uchunguzi.

Kwa ukweli, afya na huduma ya binadamu (pamoja na familia nyingi) tayari zimeelemewa na tatizo, zinaugua kujiandaa kujishughulisha nalo. Bila mashaka Yesu angeishi kwa amani kama nyumbani kama angejikuta katika hali hii - imemzunguka kila upande kwa desturi zinazotawala lipi ni jema na lipi ni baya, lipi ni sahihi na lipi ni tabia ya dhambi, na yupi akaribishwe na yupi afungiwe milango ya makanisa.

## Kuunda Mitandao

Kuunda mitandao na ubia itakuwa jambo la muhimu kwa mipango ya mbeleni. Kanisa nchini Zambia halina uchaguzi katika vita dhidi ya VVU na UKIMWI bali kuunda mitandao yenye mikakati na ushirikiano na asasi zisizo za kiserikali (NGO's) zinazoshughulikia masuala ya UKIMWI ili kuongeza kwa watu waishio na VVU na UKIMWI.


Lazima kuwe na mtazamo sahihi wa kithiolojia unaogusa kweli, uhuru, haki, mapenzi, huduma na uadilifu, mwongozo, uangalizi na elimu. Tunaweza kutambua matakwa ya Mungu kwa wakati huu kwa kuwa na uongozi makini na imara ili kuleta uponyaji wa kweli. Wajibu wa kanisa la mwanzo (la kijamii) na kuunda mitandao ni mambo ya muhimu katika maono ya Zambia isiyo na VVU na UKIMWI.

Hakuna kati ya haya ambacho kinaweza kutimilika na kuwa cha muda mrefu kama hakuna taratibu za urahisishaji, mafunzo na maono. Viongozi wa dini ambao wana majukumu mengi wanaweza wasizifanye changamoto hizi za ziada. Katika nafasi ya juu ya malengo yote haya, kanisa la Zambia linaweza kutoa mchango wenye maana kwa kuihamasisha jamii.

Kanisa huwashirikisha watu katika kiwango kikubwa sana. Katika kila wiki, wakristo kutoka kila kundi la kimaisha wanakutana katika ibada na wanafanya shughuli kadhaa katika jamii yao. Katika maeneo ya vijijini nchini Zambia, kanisa ndicho chombo pekee cha kijamii ambacho watu, Wakristo na wasio Wakristo wanategemea. Asilimia hamsini ya huduma za afya vijijini Zambia hutolewa na taasisi za makanisa.



Kanisa nchini Zambia linashikilia eneo muhimu na linatoa mtandao mpana unaounganisha watu wa kawaida katika sughuli za kijamii na kiuchumi. Kuamsha juhudi za wanachama wake kutatoa nguvu katika kuondoa unyanyapaa na kubaguliwa unaosababishwa na VVU na UKIMWI, na itasaidia kujenga zambia isiyo na VVU na UKIMWI. Kama mwanamke aliye na VVU alivyosema Zambia, " Mungu hakutuita kuhukumu, bali kuongoza, kupenda, kusaidia, kujali na kuleta matumaini kwa watu waishio na VVU. Tafadhali usinihukumu, njoo karibu nami, nifahamu, nisaidie, unategemea nitakua vipi kama hunipi nafasi?"



Watu waishio na VVU

na Jamii ya Kikristo

DENMARK

# Mwili wa Kristo

NA THEODOR JØRGENSEN

Paulo analinganisha jamii ya Kikristo au Kanisa na mwili na kuuita mwili wa Kristo (angalia 1Kor 12:12). Ni ulinganisho mzuri, inatakiwa kuthaminiwa iwapo kukutanika kwa Wakristo kila siku kunawekwa katika matendo. Mwili una viungo tofauti vyenye kazi tofauti, lakini vyote ni vya mwili mmoja. Vikishirikiana maisha kwa namna hiyo, kiungo kimoja kikiumia vyote vinaumia na kiungo kimoja kikifurahi vyote vinafurahi. Hii pia inatumika katika kanisa kama mwili wa Kristo, kama Paulo asemavyo. Kila mmoja ni kiungo katika mwili na anahusika na wote katika maisha ya kawaida katika Kristo.

Paulo anaona kwa undani muunganiko kati ya kanisa kama mwili wa Kristo na maadhimisho ya karamu ya Bwana: " Mkate ule tuumegao si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja". (1Kor 10:16b). Katika karamu ya Bwana, kukutanika kwa kanisa na katika Kristo kama mwili wake kunaonekana dhahiri. Maisha ya Kristo tunayoshiriki kupitia karamu ya Bwana pia ni maisha ya pamoja na mmoja kwa mwenzie, katika furaha na mateso – furaha na mateso ambayo ni furaha na mateso ya Kristo mwenyewe.

Kuna kitu kinachotatiza, namna Kristo alivyosema kuwa atakuwa pamoja na kanisa lake. Lakini hatusumbuki, kwa sababu tu tumezoea kuelewa katika njia mbili tu: katika kuhubiri injili na kusimamia ubatizo na karamu ya Bwana (ekaristi takatifu). Lakini Yesu alisema kwamba atakuwa kwa jirani yetu aliye katika mateso. Hii ni njia ya tatu, Katika mfano wa hukumu ya mwisho katika Mathayo 25:40b, Kristo anadhibitisha hili bila mashaka katika jibu lake kwa wenye haki: " Amin nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo (hii ni kusema wenye njaa, wenye kiu, walio uchi, wageni, wagonjwa na wafungwa) mlinitendea mimi". Na vivyo hivyo kwa wasio haki "Kadiri ambavyo hamkumtendea mdogo wa hawa hamkunitendea mimi". Kwa njia hiyo hiyo Kristo yu pamoja nasi katika karamu ya Bwana. Lazima tuwepo kwa ajili yake akutanapo nasi kwa jirani mwenye mateso. Hii ndiyo

maana ya kushiriki na Kristo katika mateso. Lakini ni kanisa gani linafanya hivi? Wazo juu ya swali hili linaweza labda kutufanya tuwaze swali lote la ina maana gani kuwa jamii ya Kikristo.

Ni katika ngazi ya parishi ambapo maamuzi kwa vitendo yanatakiwa kuchukuliwa, kwa sababu Kristo anakutana nasi ndani ya watu walio na VVU na UKIMWI, kama anavyokutana nasi kwa wagonjwa wengine. Mateso yote ni mateso kwa Yesu Kristo mwenyewe. Kuwaacha wenye mateso ni kumwacha Kristo mwenyewe. Kuwapa upendo na msaada watu wenye UKIMWI kadiri tuwezavyo ni kumpa msaada na upendo Kristo.

## Miiko ndani ya Kanisa

Linapokuwa limesemwa, siyo lazima kusema lolote. Kila kitu kinakuwa dhahiri. Lakini mengi yanahitajika kusemwa. Na hii si haba kwani UKIMWI ni ugonjwa uenezwao kwa zinaa na katika nchi za Nordic umeshambulia vibaya vikundi vya ushoga. Lakini hii ni tabaka ya maisha ambayo imekuwa ni mwiko katika Kanisa. Maendeleo ya kuridhisha yamefanyika katika kuzungumzia mapenzi kama njia ya kuelezea upendo kwa jirani. Kwa sasa kuna kikundi kidogo cha Wakristo ambao wanaweza kuruhusu mapenzi kama njia ya kuendeleza uzazi. Hata hivyo mapenzi kama ilivyo inaweza kusababisha kuhisi au kutohisi hisia za kutenda kosa. Na katika ushoga, njia ya kutambua ndani ya ukristo upendo juu ya jirani kwa mtu mwenye silka hiyo yaonekana kuwa mbali sana. Kinyume chake: Kuna wale wanaodai kuwa UKIMWI ni hukumu ya kutoka kwa Mungu kwa ajili ya usenge, ubasha na usagaji au wale ambao wanasisitiza kwa namna nyingine kuwa hii ni njia ya asili ya malipizi dhidi ya kile wanachoona kuwa kinyume na asili ya kukutana kwa wanadamu kimapenzi.Hii ina maana kuwa watu wengi waliopimwa wakaonekana na VVU au wanaosikia dalili za UKIMWI watalikwepa Kanisa. Wanaogopa mwanzoni kabisa kwa sababu wanaweza kukutana na shutuma. Na hii inahusu pia ndugu na marafiki wa wale wenye UKIMWI.

## Hatia na Wajibu

Kanisa lazima liwe ni jamii ambapo watu waishio na VVU na familia zao wataweza kushuhudia kinyume cha yale wanayoshuhudia. Mara nyingi hutengwa katika sehemu za kazi na hupoteza kazi, marafiki hata jamii zao, wanaonekana kama viumbe vichafu. Hakuna anayedhubutu kuwagusa, wakati mwingine hata na madaktari na wanaowaangalia. Kwa ufupi,wanaonekana kama takataka na wanahisiwa kuwa hatari kwa mazingira yao na hatari katika jamii. Watu wengine wanfikiria kwamba watengwe na ikiwezekana wawekwe magerezani.


Woga wa kifo mara nyingi unaendana na hisia za hatia. Katika nchiza Nordic, UKIMWI unaitwa ni ugonjwa wa mtindo wa maisha kwa saba hatari ya kuambukizwa ni kubwa zaidi kutegemea na tabia ya mtu anavyochukulia mapenzi. Kwa hiyo watu wenye VVU/UKIMWI hawawezi kukwepa swali la hatia na wajibu juu ya maisha yao wenyewe – na pia maisha ya wengine ambao kwa kutojua wamewaambukiza.

"Kama nisingefanya kama nilivyofanya, nini kingetokea katika maisha yangu na labda ya mtu mwingine?" Majuto hupelekea kifo, kwa sababu inasababisha upotevu wa eneo la maisha ya wengine na ya mtu-husika. Mmoja wetu asisahau hilo. Lakini kwa watu wenye UKIMWI, ukweli huo unauma kiasi kwamba unaweza kusikia kama laana. Na hisia za kulaaniwa zikiendana na kukataliwa, mtu hukata tamaa kwa kiasi kikubwa.

## Si Hukumu ya Mungu

Inapokuwa kwamba maumivu ya watu wenye UKIMWI ni ya Kristo mwenyewe, makanisani wanatakiwa wapate kinyume cha shutuma, kinyume cha kutengwa na woga wa kukutana na watu. Hii ina maana gani kwa jamii ya kikristo kukutana na watu waishio na VVU na UKIMWI?

In maana zaidi ya yote, kwamba tunachukuwa kwa uzito mkubwa yale ambayo mara nyingi tunaimba na kukiri Kuhusu



Kristo katika ibada zetu. Kama fungu hili la maneno kutoka katika kitabu cha nyimbo cha kidenmark: " Ulichukua hatia yetu na ukachukua aibu yetu, ili nafsi zetu zipone." Kwa kuwa Kristo alichukua hatia zetu yeye mwenyewe na badala yetu mara moja na kwa wote akateswa hadi kifo kama adhabu ya hatia, kifo hakiwezi kuwa adhabu ya Mungu juu yetu, ukweli unaoelezwa katika kuabudu katika msamaha.

Katika hali yoyote, vilevile, ikiwezekana mateso na uwezekano wa kifo kwa watu wenye UKIMWI watakachopitia isielezewe kuwa hukumu ya Mungu. Kutokana na mtazamo wa Ijumaa kuu na asubuhi ya siku ya Pasaka, kifo ni sawa na mateso yoyote na kifo: kifo ambacho Mungu atatuokoa na kutupitisha ili kutufikisha katika ufufuo na uzima wa milele. Kwa kuwa mateso ya watu waishio na UKIMWI ni mateso pia ya Kristo, Kila mtu anahusika katika ufufuko wa Yesu Kristo. Au katika maneno ya wimbo huo huo " Kwa ajili yetu ulikufa na ukafufuka, ulitununua kwa damu yako ya thamani na wewe pekee ndiye mfariji wetu.

## Jamii ya Kikristo

Inawezekanaje jamii ya Kikristo kufanya jambo hili la kuaminika kuhusu watu wanaoishi na VVU na UKIMWI? Zaidi ya yote kwa mtazamo. Uaminifu, uwazi, motomoto, kukubalika lazima iwe kawaida ya tabia ya Mkristo kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Moja ya matatizo ya msingi ya watu wenye UKIMWI ni kwa wao wenyewe kujitahidi kwa dhati maisha yao jinsi yalivyo, na kushikamana na heshima yao ya utu. Ukiwa na mashaka, haisaidii ukielewa kuwa wewe ni wa thamani kwa wengine, na kwamba maisha yako ni ya maana sana kwa wengine kiasi kwamba hawawezi kuacha kushirikiana nawe. Siyo katika 'sadaka' ukielewa kuwa mwema kwa wale walio na upungufu kuliko wewe: kunaweza kukawa kitu cha kudhalilisha katika mfumo huu wa sadaka. Kujihusisha lazima kuwe katika mfumo wa kuheshimiana na kupendana. Katika mahusiano na watu waishio na VVU na UKIMWI, jamii ya Kikristo lazima iweke wazi na kuwashawishi kwamba maisha yao yalikuwa bado ya thamani kubwa mbele ya Mungu. Watu wenye VVU na UKIMWI wahusishwe katika jamii, si kwamba wao ni wapokeaji tu, lakini kama watu walio na kitu cha kutoa. Kwa Mungu msingi wa kukubalika kwa wale wenye UKIMWI, ni kutumia jamii ya Kikristo kama mkono wake. Na kama sehemu katika Mwili wa Kristo, watu walio na VVU na UKIMWI wana mchango katika maisha ya kawaida ya mwili na makuzi yake.

Kinachotakiwa ni matendo ya dhahiri, ya dhahiri kama mifano ambayo Yesu aliitoa katika mfano wa hukumu ya mwisho (Mathayo 25: ) kushughulika na mahitaji ya kila siku, kutembelea, kusikiliza, kuzungumza kwa pamoja, kuwa na wasaa wa kujadiliana matatizo yanayoweza kutokea kadiri muda unavyokwenda, lakini pia kuwa na wakati wa kuzungumzia uzima na kifo, makosa na msamaha na uzima wa milele. Kwa njia



zote lazima iwekwe wazi na yenye ushawishi kwamba maisha hayakomi baada ya kifo. Lakini itambulike kwa imani kupitia ufufuo wa Yesu Kristo kutoka katika mauti maisha ya mtu yatafikia ukamilifu katika upande mwingine baada ya kufa. Na mwisho, jambo rahisi lakini la muhimu sana: Wakristo lazima waonyeshe huruma kwa kugusana, kusalimiana na kukumbatiana. Watu wenye UKIMWI hujisikia kusumbuka kugusana na watu wanaokutana nao. Hii ni jazba na siyo sahihi, kwa sababu tunaelewa njia ya maambukizi na hatari kidogo ilivyo katika maambukizi. Woga wa kugusana unawafanya watu wenye VVU na UKIMWI kuwa wapweke mpaka kifo. Katika jamii ya Kikristo wasiwasi wa kugusana wala usifikirike.

Lakini, Je kama wengine wakifikiri kwamba hatari ya maambukizi ni kubwa kuliko ilivyodhaniwa na hatari ya kuambukizwa inaongezeka? Yesu alisema "Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza; na mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona." (Math 10:39). Kwa hiyo, katika Kanisa, kuna utamaduni wa mtu kuhatarisha maisha yake mwenyewe kwa ajili ya mtu mwingine, kama maisha ya mtu mwingine yanahatarishwa. Majumba ya watawa yalithibitisha hili katika milipuko ya magonjwa katika nyakati za kati, wale wanaowaangalia wenye ukoma wanathibitisha hilo tangu wakati huo. Na tangu nyakati za kale imekuwa ni sehemu ya kanuni za kitabibu. Kama tumaini la Mkristo kushawishi, jamii ya kikristo lazima ikombolewe kutoka katika woga wa kifo unaojionyesha katika woga wa kugusana.

## Kanisa la Mahali

Katika Kanisa la mahali, kuaminiana na kukutana pamoja kunaweza kufanyiwa kazi kwa kuunda vikundi vya kusaidiana. Hivi vinatakiwa kuhusisha familia na watu binafsi ambao katika kushirikiana na vikundi vya masaidiano katika eneo lao wako radhi kuwakaribisha katika nyumba zao, kutoa msaada fulani na kuwatembelea watu waishio na VVU/UKIMWI majumbani mwao au katika hospitali. Vikundi hivi vya masaidiano lazima kuwepo kwake kujulikane kwa namna fulani, ili wale waishio na UKIMWI wajue wanapohitaji msaada waende kwa nani bila woga, kama – kwa mfano, mtu ambaye amejulikana kuwa na VVU anataka asijulikane mwanzoni lakini anahitaji mtu wa kumfariji kutokana na jinsi alivyo. Vikundi hivi vya kufarijiana vinatakiwa kujengwa katika hali ya ushirika katika mfumo wa ngazi ya chini kijamii na kuweza kusherehekea karamu ya Bwana (ekaristi) kwa pamoja – Kwa sababu ekaristi ni alama yenye nguvu ya ushirika katika Kristo ambayo kila mtu anahusika.

VVU na UKIMWI ni changamoto kwa usharika na zinaweza kupelekea kujua kwa vitendo nini maana ya kuishi kama Mwili wa Kristo, kushiriki kwa pamoja raha na maumivu ya maisha, kwa matumaini ya uzima wa milele yaliyoandaliwa kwa sababu ya huduma ya mapendano ya sisi kwa sisi ambayo tunakutana na Yesu mwenyewe katika mateso yetu.

Juhudi za ulimwengu lazima ziendane na shughuli zinazofanyika katika ngazi za chini ili kutengeneza ushirikiano na mshikamano kwa watu waishio na walioathirika kwa VVU na UKIMWI

MSUMBIJI

# Unyanyapaa

NA ELIAS ZACARIAS MASSICAME

Unyanyapaa kwa watu waishio na VVU /UKIMWI na kubaguliwa kwa familia zilizoathiriwa kunaweza kuzuiwa kama VVU/UKIMWI utaachwa kuangaliwa katika mtazamo wa kawaida na katika mwelekeo uliopo sasa. Mtu aliyeathiriwa na VVU/UKIMWI bado ni mwanadamu anayestahili kushi na kuheshimiwa. Je, kuna wakati VVU/UKIMWI utaangaliwa kwa umakini na kama ukweli halisi wa ustaarabu au utamaduni ulimwenguni?

Mgonjwa yeyote anastahili kutiwa moyo na kupewa umoja kutoka kwa wengine ili kupambana na madhara ya kisaikolojia yanayosababishwa na ugonjwa. Lakini udhaifu wa mmoja wa wanafamilia, katika udogo wowote, unaathiri wanafamilia wengine hasa kama aliyeathirika ni mkuu wa familia. Kama alivyo mtu mwingine, ana hisia na anahitaji upendo, kuangaliwa na msaada kutoka kwa wengine, hasa kutoka kwa marafiki na jamaa. Ni katika mateso umoja na upendo vinatakiwa sana, kwa sababu kukata tamaa huongezeka.

Kanisa kama jamii limeitwa kusaidia kuelewana, umoja, kuangalia, upendo na huruma, kama vile Yesu Kristo. Mungu daima yuko na kila mtu na tunafahamu kuwa hawaachi walioathirika au kuathiriwa na VVU/UKIMWI.



Ukristo kama kundi la watu waaminifu kwa Yesu Kristo lazima uwe chombo cha upendo kwa wengine na kimbilio la wale walio wadhaifu. Lakini ili kuleta mshikamano kwa kila mmoja, tunatakiwa kujifunza kuthamini maisha kwanza na kujithamini sisi wenyewe, ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kupenda wengine. Katika mazingira ya VVU/UKIMWI hali ya kuwa na thamani na kuthamini wengine ni muhimu sana.

Katika kila jamii, mabadiliko katika tabia na mtazamo yanaathiriwa sana na desturi na namna ambavyo taasisi za kijamii zinakumbatia desturi hizo. Kanisa, kama taasisi iliyoshikilia nafasi muhimu katika mahusiano na muingiliano wa jamii, hasa wakati wa magonjwa au shida, daima litafute mazingira mazuri kama linataka kuwa nuru na chumvi ya dunia.

## Dhambi ni nini?

Watu wengi hufikiri kuwa tatizo kubwa watakalokumbana nalo wakipimwa na kuonekana na VVU ni kuonekana kuwa ni watenda dhambi. Njia hii hasi ya kufikiri imewapelekea wengi kujitenga. Kuwaona watu wanaoishi na VVU/UKIMWI kwa jicho la kuhukumu kunasababisha unyanyapaa na kukataliwa na jamii. Jamii inatakiwa kuelewa kuwa VVU/UKIMWI hauhusiani na dhambi. Kinyume chake, ni dhambi tunapowabagua na kuwakataa kaka na dada zetu kwa sababu wameathirika kwa VVU.

Upendo na huruma vinaainisha huduma ya Yesu na hivi vinakuwa vya muhimu kuliko vyote kwa wale walioitwa kwa Jina la Yesu Kristo. Kama Wakristo tumeitwa kupenda na si kuhukumu. Yesu mwenyewe alituonyesha mfano kwa namna alivyoonyesha upendo na huruma kwa wagonjwa. Yesu anatuambia, "... pendaneni kama mnavyojipenda ninyi wenyewe". Kwa hiyo, kwa makusudi, lazima tuwe na huruma "kwa makusudi ya kuugua sisi kwa sisi".

Kanisa na wakristo wameuvaa mwili wa Kristo, kwa hiyo, wameitwa kuonyesha upendo wa Yesu kwa wale walioathiriwa na VVU/UKIMWI na kuwahudumia kwa upole na uangalifu. Hii ina maana kuwa, kama wawakilishi wake, Kristo lazima aonekane ndani yetu na tusifanye kwa namna inavyotupendeza sisi wenyewe, bali kwa namna ambayo Yesu angefanya kama angekuwa nasi leo hii. Tunatakiwa kuelewa kuwa, virusi ni adui na kutambua kuwa watu waishio na VVU/UKIMWI wana uzoefu mkubwa na maradhi haya ambao unaweza kutumika kwa manufaa ya wote.

## Wajibu wa Makanisa

Kanisa na jamii za kikristo zina nafasi ya muhimu katika mapambano dhidi ya maradhi ya VVU/UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa. Kwa kuwa VVU/UKIMWI umeathiri hali zote za kibinadamu: kiutamaduni, kiroho, kiuchumi, kisiasa, na kisaikolojia nk. Tunaamini kanisa linaweza kutoa mchango wake kama ifuatavyo:

- Kufundisha na kuongea na jamii kuhusu mahusiano ya kimapenzi.
- Kushawishi na kutetea kwa ajili ya watu waishio na VVU/UKIMWI ili kupunguza unyanyapaa na kubaguliwa.
- Kushauri na kuwahudumia wagonjwa kwa kuwapa upendo na kuwahudumia.
- Kulinda yatima na watoto walio katika mazingira magumu.
- Kuanzisha na kutia moyo matibabu ya magonjwa nyemelezi ya VVU/UKIMWI.



**Kanisa ni mahali pa kuabudu, kufarijiana na urafiki. Lakini kuwa na VVU kumechukuliwa kama hali ya kudharaulisha. Kwa sababu hatuwezi kuelezea mambo ya kujamiiana waziwazi, watu wengi wananyanyapaliwa.**

DUARA ZA MATUMAINI, ZAMBIA

## Haja Ya Kuishi kwa Afya Njema

Askofu mkuu wa kanisa Anglikana la Cape Town, Njongonkulu Ndungane alisema kuwa sababu moja inayofanya watu wasite kuongea kuhusu VVU/UKIMWI, hasa wazazi kwa watoto na vijana ni woga wa kusumbuliwa na jamii na kanisa. Wakati huo huo, desturi ya kutoongea kuhusu kujamiiana mpaka kijana anapokaribia kuoa au kuolewa, imekua ni kikwazo pia. Hali hii inawaacha vijana na watoto katika hatari ya kuambukizwa VVU.

Kwa bahati kuna kuongezeka kwa ufahamu kuhusu VVU/UKIMWI na kuna majaribio ya kukabiliana kwa namna ambavyo watu wamehusishwa katika jamii na ulimwengu: ambapo ubora wa maisha katika upatikanaji wa maji, usafi,vyakula na lishe, ajira, kugawana utajiri, upatikanaji wa huduma za afya na kuhusishwa katika siasa, kati ya vichache inatambulisha hali ya mtu kiafya. Kuufanya mwili kuwa na nguvu, kujiamini, na hali ya kumiliki ndani ya mtu ni msingi ambao unaweza kuwafanya kuishi kwa maisha mazuri.

Kwa mwananchi kuishi maisha salama haitoshi kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi. Kama mifumo ya kutolea uchafu ni mibaya, kama ubora wa maji ni wa chini, hali hii itaathiri mazingira ambamo watu wanaishi na hii itatoa magonjwa yaliyoenea kama malaria na uti wa mgongo. Kukosa fedha kwa ajili ya kutibu magonjwa kunaweza kuchangia upatikanaji wa damu isiyo salama inayoweza kuathiri maisha ya wananchi. Kuhusisha elimu ya watu kuhusu afya ya jamii na VVU/UKIMWI inaweza kufanikiwa iwapo juhudi zinazoendelea hazikwami na zinashughulikia kiini cha tazizo.

Mpango wa VVU/UKIMWI wa Umoja wa Makanisa ya Kikristo nchini Msumbiji umechukua hatua ya kwanza ya jumla kuunganisha shughuli zake za VVU/UKIMWI na mapambano dhidi ya magonjwa mengine yaliyotapakaa kama malaria, kuhara, magonjwa ya zinaa, magonjwa ya ngozi na utapiamlo.

Juhudi kidogo zilizochukuliwa katika mifumo ya kiimani ya pamoja kama kuanzishwa kwa miundo inayoshughulikia VVU/UKIMWI na vitabu vya maombi vilivyokwisha tengenezwa, lazima visambazwe kwa lugha za mataifa zinazotambulika katika umoja wa kiimani duniani ili zisomwe na kila mtu. Nchi za kiafrika zitafute njia ambazo lugha za kiafrika zinaweza kutumika kueneza habari juu ya VVU/UKIMWI.

Tatizo linaweza kutatuliwa kama kuna utashi wa wale wanaomiliki taarifa, ujuzi wa kisayansi, uchumi na utashi wa kisiasa kufanya mabadiliko. Juhudi za kimataifa zikienda sambamba na juhudi katika ngazi za jamii ambako watu ni sehemu ya majibu, itapunguza athari za kisaikolojia katika mlipuko wa ugonjwa wowote.

Mawazo, tafakuri, uzoefu kutoka kwa watu wanaoishi au walioathirika kwa VVU

NORWAY

# Bila Woga

Katika mikutano yetu na watu wenye VVU na wasio na VVU Oslo, tulijifunza kuwa kadiri watu walivyozidi kuzoeana ndivyo walivyoaminiana zaidi. Tulishirikishana mawazo na maswali, jinsi ugonjwa ulivyoenea, imani, kukata tamaa na hasira. Kwa nini sasa ni vigumu kwa Kanisa kuwa mahali salama pa kupitia kwa aina hii ya uponyaji wa kushirikiana?

Tatizo ni kwamba makanisa ni vitu tofauti kwa watu tofauti. Vyombo vya habari, mahubiri na matamshi ya wale wenye mamlaka vyote vinachangia kuonyesha kuwa vitu vingi katika maisha vinatakiwa viachwe nje kwa sababu havina sehemu ndani ya Kanisa. Kama mwanamke aishiye na VVU alivyosema " unapata hisia kuwa maisha yako yanakaguliwa unapoongea na mchungaji". Kujamiiana na VVU ni vitu ambavyo haviongelewi. Kama mshiriki mmoja alivyosema, " ni haramu au mwiko". Matakwa ya kutunza alama ya kanisa – ambacho ni halali – inaonekana kuwa kama tamaa ya kushikilia 'sheria', na utengaji au uathirikaji wa wale wasiozifuata, na kwamba inakuwa vigumu kwa kanisa kutimiza wajibu mwingine, ambao ni kuwafundisha watu kujikubali wao wenyewe na wengine katika njia ya unyoofu.

'Kanisa', alisema mshiriki mmoja, "linaweza kuwajibika vizuri katika kutoa nafasi salama ambapo inawezekana kuwa muungwana na kuongea ukweli kuhusu maisha yako binafsi na kuhusu maswali na mashaka uliyonayo". Hii siyo rahisi kama inavyoonekana . "Wakati mwingine tunakutana na misimamo na matendo ambayo tunayakataa kwa nguvu. Lakini tunatakiwa kujifunza kukubali tofauti, siyo kuwaweka watu katika makundi tofauti na kuwahukumu kwa kuchagua nani awemo na nani asiwemo. Na tuwe radhi kutambua kuwa sote tuko katika kiwango cha msingi cha ubinadamu- kwa kufanana." Kwa ufahamu wa ndani, huu ni ufahamu uliomo ndani ya kila mtu, lakini kwa watu waishio na VVU ni ufahamu wa kwanza ambao wako radhi kuutoa kama rasilimali katika jamii yote ya kanisa.

Kwa kutiwa moyo na ari hii ya uwazi na usalama, kanisa linaweza kujifunza kufanya kazi na watu walio katika viwango visivyoeleweka mahali ambako "woga na udaku unaweza kuwekwa wazi." Ili mazingira haya yawepo, ni lazima kuwa huru kuja na kuongea kuhusu chochote kilichomo katika maisha yetu. Ni katika magumu haya na maumivu katika kiwango hiki ambapo tabia ya unyanyapaa inaota, kukua na uharibifu wa mwelekeo wa maisha unaanza miongoni mwa 'waliokata tamaa ambao ni waathirika wa chuki zinazosababishwa na watu wengine'. Kama mshiriki mmoja alivyosema, " Iwapo ushirika haupo, mtu mwenye VVU anaweza kuwa hata kwake na kwa watu wengine. Anaweza kupita katika giza na kuwa mharibifu. Kinachofanya iwezekane kujithamini mwenyewe na wengine ni kuwa na mazingira salama na kuyakubali.

## Maadilii ya Jumuia

Katika kuchunguza thamani za msingi za jumuia, vikundi vilihitimisha majadiliano kwa kuainisha mambo matatu yanayotakiwa kuzingatiwa kwa pamoja:

1. Thamani mbalimbali ya mwanadamu, inayoelezewa katika kuheshimu tofauti ya kila mmoja.
2. Uwanja mmoja wa woga, kutokuwa salama na utu uliomo katika matabaka tofauti ya mwanadamu.
3. Uelewa kuwa sote ni tofauti lakini tu wamoja na tu katika mwili mmoja.

Kwa nini ni vigumu kwa hili kutokea? "Kwa sababu, kama alivyosema mshiriki mmoja, 'kanisa mara nyingi huonyesha thamani ya mashindano, kujiweka mbali na mafanikio ya kiuchumi yanayoonekana katika jamii. Badala yake huunga mkono thamani au manufaa hayo kwa kupitia mfumo wake wa kiutawala. Lakini ukweli ni kwamba kanisa linatakiwa kuwa na mfumo wa kiutawala ambao ni tofauti na mfumo wa kidunia: Yesu alisisitiza kuwa wale wanaotengwa na dunia ndio wale walioitwa kuwaaibisha wenye nguvu na hekima'". Kwa ajili ya uthamani wetu na utambulisho wetu halisi ni katika kufanya kwa kuelewa kuwa tumeumbwa na tunapendwa na Mungu. Hii ni sehemu ya mfano wa Mungu ndani yetu: Mungu asemaye "Mimi ndiye ambaye ndiye".

Mtazamo huu unaonyesha mgongano kwenye kiini tunachotarajia kutoka katika kanisa na ni changamoto kubwa. Kwa upande mmoja tunataka makanisa yetu kuwa jamii zenye nguvu zinazotuweka salama kutoka kwa vile tunavyoogopa. Kwa upande mwingine, tunataka yawe wazi, yakubali na kutusaidia kupambana na vile tunavyoviogopa na si kuvidhibiti. Tunakataa hali yetu ya kutokuwa salama na ile ya wengine kwa sababu tunaiogopa. "Kwa hiyo hatutaondoa moja kwa moja

unyanyapaa, kwa sababu unatokana na uelewa wetu wa kinachotutisha".

Mtazamo wa Mtakatifu Paulo wa kanisa kama 'mwili' ulitazamiwa kuwa na nguvu za kipekee. " Jamii za kibinadamu, ki ukweli, mtu mmoja, mwili mmoja ni muhimu tukajua," alisema mshiriki mmoja . "Tunapoteketeza mtu mwingine, tunateketeza kitu fulani ndani yetu na kuathiri ubinadamu wetu wote.

Unachowafanyia wengine, ujifanyie mwenyewe na sisi sote. Lakini hii haina maana kuwa sisi wanadamu tunafanana. Kuna tofauti kubwa miongoni mwetu, kwa namna ilivyo ndani ya kila mmoja wetu. Matengano na kukataliwa kunatokea wakati ambapo tofauti zetu hazitambuliki.



## Mahali Salama

Uzoefu wa matengano ulichangiwa na washiriki karibu wote. "Mamlaka za Kanisa" – wanaume, kwa sehemu kubwa – mara kadhaa wameanzisha kanuni zinazofafanua kuwa wako nje kwa kushauri kwamba hatufanani na 'taswira halisi' inayoelezwa katika kipengele cha 'kuwa mtu'. Kulikuwa na hasira pamoja na kuchanganyikiwa , pale washiriki walipoongelea aibu ambayo ubaguzi huu unasababisha. " 'Inawezekanaje hata Ushirika Mtakatifu umetumika kubagua watu?' 'Na kama uzoefu wetu katika maisha unatufanya tusikubaliwe na kanisa, basi wanadhani tunajisikiaje sisi wenyewe?'"

Ni muhimu sana, walisema washiriki wetu, kwa makanisa yetu kuwa ni mahali pa matumaini, kwa watu wote - wale waliotengwa au kubaguliwa na zile sehemu zetu zilizojitoa au kujificha. Lakini tunawezaje kufanya haya yatokee?

Washiriki walipendekeza haya yafuatayo:

1) Ni muhimu kufanya VVU ionekane katika makanisa yetu. 'Wachungaji wanatakiwa kuongea kuhusu unyanyapaa na chuki kutoka katika madhabahu'. 'Mahubiri yalenge maisha yetu ya kila siku ikiwemo maisha pamoja na VVU. Mmoja alieza maisha ya kila siku yalivyo kwa mtu mwenye VVU: kuna ujinga mwingi! ' Lazima tuunganishe kati ya kile biblia inasema na kile tunachokumbana nacho leo.'
2) Makanisa yanaweza kujaribu kuwa mahali salama ambapo huhitaji kuwa imara kila wakati na ambapo watu wataweza kupatambua na kushirikiana wasiwasi wao na mashaka yao.
3) Kuna umuhimu kwa makanisa kuchunguza misimamo yao juu ya mahusiano na kujamiiana.
4) Makanisa yatafaidika kutokana na kuangalia upya suala la kuishi kama mwili mmoja, vyote katika mtazamo wa mwili kama taswira ya jumuia ya kikristo na uthamani halisi wa maisha, mateso na miili binafsi.
5) Makanisa na mikusanyiko (sharika zake) yanatakiwa kufikiri na kuishi kama sehemu za matumaini, siyo matengano wanaweza kusema "Tuko hapa kama zawadi kutoka kwa Mungu kufanya maisha yawezekane, na kufanya maisha kuwa ya kupendeza na kuwa kamati ya kukaribisha nguvu za uponyaji". Fikiria kama kila mmoja angefikiria hivi!

Kwa nini Ukimwi unaonekana kutisha hivi?

Kufanya kazi dhidi ya VVU ni kujifanyia mwenyewe

– woga wetu na ukomo, na uwezo wetu wa kutoa badala ya kutesa

DENMARK

# Kuushinda Upweke



NA ELIZABETH KNOX-SEITH

Kama wewe ni mwanachama wa dhehebu la Kikristo na unataka kujihusisha na masuala ya VVU na UKIMWI, utakutana na changamoto nyingi.

Kwanza kabisa utapata changamoto ya kuonyesha namna unavyofikiri, ili ufanye kazi na 'kutoelewa mambo' hii ni kusema namna ya kuelewa hali ambazo kwa kutojua zinaonyesha namna unavyopambana na majukumu yaliyo mbele yako. Kama huelewi kuwa hali hizo zipo, zinaweza kuwa na matokeo hasi, si tu katika mahusiano yako na watu unaotumaini wanaweza kukusaidia.

Ni muhimu hasa kuzingatia suala la aibu, hatia na adhabu – kwa sababu mara nyingi ni katika kufichika kwetu kiakili kulikojengeka katika hisia katika eneo hili na linaloonyesha mtazamo wetu juu ya ugonjwa na kifo.

Njia sahihi inayofaa kutumiwa kutimiza hisia za udhibiti, ni kurejea kiini cha ugonjwa kwa mgonjwa mwenyewe. Ni tabia ya mtu iliyofanya apate ugonjwa. Ili kudhibiti ugonjwa, aina ya tabia iliyosababisha kuongezeka kwake lazima ibadilike. Hii kwa kiwango fulani inaweka kiasi, uwezo na nguvu mikononi mwa wahusika – lakini pia inaweza kuwa chanzo cha hisia kali za kujilaumu. Kama aina fulani ya tabia ilisababisha watu waugue, wanaweza kushutumiwa kirahisi na wale wanaowazunguuka – na wale walio wagonjwa kwa urahisi wanaweza kujisuta wao wenyewe nafsi zao na wakaanza kujilaumu.

Wasiwasi na kujihukumu ni nyuso mbili zilizofichika ambazo UKIMWI umeleta duniani – ni lazima ziwekwe wazi.

Tunaweza kuyashughulikia vipi matengano yetu ya ndani? Wasiwasi wetu juu ya kifo ni sawa na wasiwasi tulionao kuhusu kujamiiana? Kwa nini VVU na UKIMWI yanaonekana kutisha kuliko magonjwa mengine wakati yote huathiri mwili? Tufanye nini kuwafikia watu walio na UKIMWI ili kutoa wasiwasi huu?

## Kuwa Msikilizaji ni Kuvuka Vikwazo

Kujishughulisha na VVU/UKIMWI ni kujishughulikia wewe mwenyewe – mipaka yako mwenyewe, uwezo wako, uwezo wako wa kutoa badala ya tamaa zako mwenyewe. Kwa kukutana na wahusika unajifunza kuhusu maisha na kifo tofauti na ambavyo ungejifunza kwa kusoma maktaba iliyojaa vitabu – hata hivyo, ni muingiliano wa elimu na uwezo wa kushughulikia maoni ya wengine ambayo ni mwanzo na mwisho (Alfa na Omega) katika kuongea na watu wenye VVU. Uelewa wa namna virusi vinavyo sambaa na ugonjwa unavyoanza unaweza kuwa muhimu unapokabiliwa na dukuduku lako na la wengine – lakini elimu hii haitoshi unapokutana tha mtu mwingine, uso kwa uso. Hapa unahitaji kusafisha rekodi yako vizuri na ukutane na mtu kwa uwazi na shauku, ukiwa tayari kujifunza nini kiumbe huyu wa pekee atakupa. Kupitia katika

**Kinachoniangusha ni kwamba wajibu wangu kwa jamii umebadilika. Siyo rahisi kukutana na marafiki kama ilivyokuwa kabla. Ninafahamu kuwa wanafikiria kuhusu kuathirika kwangu. Mara nyingine naifanya hali kuwa mbaya mimi mwenyewe. Najisikia ninaweza kuishi na ukoma au VVU, kwa kujitoa. Siyo VVU peke yake inayonifanya niteseke, ni watu wanaosababisha niteseke.**

HADITHI ILIYOSIMULIWA NA MWANAMKE AISHIYE NA VVU KUTOKA LUSAKA

matatizo inaweza kuwa tukio kubwa la - Kuelimisha katika maisha – na wale wanaoishi sambamba na mtu aliyeko katika mchakato huu hujifunza mambo mengi na huanza mwanzo mzuri katika historia kwa kila hatua inayochukuliwa.

Kuwa macho kwa mambo mapya ya kujifunza katika matatizo na mtu mpya ni jambo la msingi kwa kutiwa nguvu (au kufanywa upya), kuridhika katika kazi na uzima.

Katika mwendo wa maisha yao, watu wengi wenye VVU na UKIMWI wamekumbana na kutoelewana na Kanisa. Ni vyema kujua namna migongano hii ilivyojikita na namna inavyofanya mtu afikiri kuhusu Mungu, Kanisa na dini leo. Kama, kwa mfano, Mungu anafanana na baba anayeadhibu aliyemzuia mwanaye kujipenda na kujijali mwenyewe, basi hakuna maana ya kuongea kuhusu Mungu apendaye. Mungu atakuwa kinyume cha upendo katika fahamu za msikilizaji – na ni vyema kuongea kuhusu uzoefu wao halisi na Mungu, kuliko kuongea kuhusu Mungu kinadharia, katika lugha na mtazamo ambao utakinzana na uzoefu alionao mtu yeye mwenyewe.

Kuchukua nafasi katika maongezi kuhusu masuala haya, Zaidi ya yote inatakiwa kuwa karibu, kujaribu kuacha mitazamo yako unayoipenda na maelezo na uichukue dunia katika mtazamo mwingine kupitia macho ya mtu unayeongea naye. Huruma na upole vitaweza kutenga na havitoshi – kama majibu ya papo hapo na ya kufurahisha yanavyoweza kuwa kikwazo kwa mwingine kuwa wazi. Ni lazima uwe mwangalifu na mwenye busara; jaribu kumfuata mtu anayeumwa katika mazingira yanayomfanya mpweke, wa tofauti na mbinafsi.

Ugonjwa hudhoofisha hamu ya kujamiiana na wakati huo huo huongeza hamu ya kuhurumiwa na kuangaliwa kwa ukaribu. Mapenzi yanaweza kuwa yalitimiliza haja hii mwanzoni – lakini haiwezekani kufumbia macho haja ya urafiki wa karibu inayoweza kujumuisha mapenzi, lakini ikazidisha. Hii inakuwa ngumu zaidi kwa watu waishio na UKIMWI, kwa sababu inaweza kuwa ngumu kupata yeyote anayeweza kushiriki katika urafiki. Ni rahisi kuhisi kuwa ni kwa sababu ya ugonjwa Ndiyo maana ni vigumu kupata rafiki. Hofu kuwa rafiki anaweza kuambukizwa mara nyingi huwazuia watu kudhubutu hata kugusana – na maraafiki (au wapenzi) wengi huona ugumu kuambatana na mtu ambaye wanajua pengine atateseka. Watu wenye VVU na UKIMWI huona ugumu kuweka maumivu na kifo ambacho wote wanajua kitakuja – hii inamaana kuwa wapenzi wote wanajisikia si salama, na hakuna mmoja wao atakaye jihusisha na mwenzake kwa kadiri wanavyotaka. Ufahamu juu ya kifo inakuwa ni kikwazo –katika njia ileile ambayo uwingi au uchache wa ufahamu juu ya hatari ya kuambukizwa, nk, ni kikwazo kuzuia kugusana.

## Kuvunja Vikwazo vya Woga

Ni muhimu kuvunja vikwazo hivi vya woga na hasa kuwasaidia watu waishio na VVU waone kuwa mwili bado ni hekalu la uzuri na unastahili kuangaliwa, kupendwa na kutiwa joto, pia katika mgusano na uangalizi. Kama mtu kwa mfano ameanza kuwa na kansa ya ngozi au ugonjwa mwingine wa ngozi, hali ya kuonekana kinyaa inaweza kusababisha akakataa kuguswa na mtu yeyote au kuonyesha mwili wake kwa mtu yeyote. Pamoja na hayo hamu ya kuonewa huruma itakuwa imejificha katika uso na kwa hiyo ni muhimu kusaidia wanaohusika kushughulikia aibu kwa ajili ya miili yao ambayo ni matokeo ya dalili za ugonjwa. Kuweza kutoka nje na kuuliza mtu wa kugusana naye inaweza kuwa ni hatua muhimu katika kudhibiti aibu – na kushikwa, kwa upole na uangalifu na upendo, badala ya kujisikia kutoguswa, inaweza kuwa hatua muhimu katika kurudisha hadhi ya utu, heshima na hamu ya kuishi.

Katika injili ya Luka 4, Yesu anakuja katika mji wa kwao wa Nazareth, ambapo anaambiwa asome katika kitabu cha Isaya. Ujumbe ni habari njema kwa maskini, kufunguliwa kwa wafungwa, vipofu kuona. Maneno yanayojulikana vyema kutoka katika kitabu cha kale yanadhihirishwa kwa wasikilizaji; "Leo maneno haya yametimia masikioni mwenu" akasema Yesu, ki ufunuo na kinabii. Ujumbe wake ni mkuu mno, wa watu wote. Wakazi wa mji wakajawa ghadhabu na wakamtoa nje ya mji katika ukingo wa kilima ambacho Nazareth ulijengwa, wakidhamiria kumuua.'Lakini alipita katikati yao na akaenda zake.'"

Yesu aliona namna ilivyo mtu aliyetengwa, hata kwa majirani na ndugu zake katika mji wa kwao Nazareth. Watu wenye VVU na UKIMWI mara nyingi wanakumbana na hali hii wakienda katika nyumba zao kwa familia na marafiki katika mji mdogo: mahali walipoondoka walipoanza kusikia maumiyu ya kuwa 'tofauti'.







Wengine wana hisia tofauti za kimapenzi, wengine ni mashoga, kitu ambacho hawakujisikia kuzieleza familia zao. Walikimbia maneno ya vijijini hadi mijini wasikojulikana – mahali ambapo wanaweza kukubalika na kutendewa wema, maisha na marafiki wapya, ambayo asili ya mtu haijulikani sana.

Wengine ni vijana waliokwenda mjini kupata elimu – siyo kukimbia kutoka kijijini, lakini kujifunza kitu kipya. Wakipata VVU wanajisikia wao wenyewe kujinyanyapaa kama wasioenda kwa utaratibu au wazinzi – hawathubutu kurudi nyumbani kueleza woga wanaoupitia. Wakati kabla walijisikia 'kawaida' lakini sasa ni wa tofauti. Ndani yao kuna hisia kali katika jambo lolote linalothibitisha woga walionao.

Wengine ni watumia madawa ya kulevya, ambao waliondoka katika familia na vijiji vyao na hisia za kujitawala. Katika mazingira ya uharibifu ya mijini wanakutana na mwangwi wa hekaheka walizojisikia ndani yao – na wakapata njia mbadala iliyowapa ahueni katika maumivu yao. Lakini wanaweza kupata VVU katika kutafuta maslahi na kujisikia watu wasio na thamani mara mbili.

## Lisiloonekana Linaweza Kuonekana

Uzoefu kutoka kaskazini unaonyesha kuwa VVU vinasambaa kirahisi katika mazingira ambayo maumivu na uharibifu wa mtu mwenyewe una nguvu. VVU katika kiwango cha juu ni kitu kinachosababishwa na tabia ya jamii – japo virusi vyenyewe havibagui kati ya jinsia, utashi wa kimapenzi, asili au daraja. Yeyote anayefanya mapenzi yasiyo salama au anashirikiana sindano yupo katika hatari ya kuambukizwa, lakini sababu za kijamii na kisaikolojia zinasababisha wengine kuchukua tahadhari, na wengine kutochukua tahadhari, kila wakati kama tabia ya maisha yao.

Mara nyingine inaweza kuwa ni hali za kijamii na kisaikolojia sababu wengine japo wameshaarifiwa hawawezi kubadili tabia zao hatarishi.

Hii inaonekana hasa kwa wale ambao ujasiri umezorota – na hasa, wale walionyanyasika kimapenzi au aina fulani ya ukatili. Mipaka yao imetishiwa – vikwazo vya hisia ambavyo watoto hutengeneza kati yao na wale wanaowazunguka. Utambulisho wao uko mashakani, na wanahitaji upendo – na mara nyingi hugundua kuwa ni vigumu kudai mapenzi stahili. Wanashindwa kuweka ukomo ambao kwa wengine ni uadilifu na hufikiri kwamba wanaweza kupata mapenzi ya karibu na mwandani wanaoutafuta katika kipindi kifupi cha mahusiano ya kingono. Tena na tena kiwewe chao huthibitika: Sina thamani ya kupendwa. Wanaonewa na kukataliwa.

UKIMWI si tatizo la mji peke yake. Ni la Nazareth pia, ni jukumu la mji mdogo. Wanaishi hapa, watu wanaowakataa watoto wao moja kwa moja au vinginevyo, kwa kutokubali tofauti miongoni mwa watoto.

Wazazi wengi leo wanahangaika na swali, Wapi tulikosea? Walikuwa na makusudio mazuri, wakawalea watoto kwa Biblia na Kikristo, hata hivyo wakaona watoto wao wanawageuka, wanahama nyumbani na kutafuta mazingira mapya ambayo ni mageni kabisa kwao.

Yesu alikuja katika sinagogi ndani ya mji wake mwenyewe na ujumbe uliovunja vikwazo. Hivi ndivyo watu waishio na VVU na UKIMWI wanatufanyia leo. Ni ujumbe, katika roho ile ile kuhusu uzima na kifo, kuhusu hamu kwa kanisa kuacha mifumo mikongwe, imara na kuwa kanisa lililojaa ari na maisha.

UKIMWI kama moja ya magonjwa mengi, ni kioo kwa maisha yetu, mtazamo wetu kwa majirani na kwetu sisi wenyewe. Je tunaweza kuvuka mipaka yetu na kuingia katika nchi yenye namna tofauti ya kufikiri, desturi zingine na utambulisho usiojulikana?

VVU na UKIMWI unatulazimisha tufikiri kuhusu masuala ya kuishi ambayo kwa kawaida huwa tunakwepa akili zetu kuyashughulikia - na kiini chake ni suala la upendo. Tunawaendeaje vijana wanaoishi katika namna tofauti na wazee walivyotegemea? Kwa maonyo, au uelewa wa kiungwana sote tunajua ni daraja la ushupavu kati ya watu? Kuzama katika kujifunza juu ya VVU na UKIMWI inatupa uwezekano wa kuvunja unyanyapaa ambao ugonjwa huja nao; uwezekano kwa wazazi kukutana na watoto wao kwa namna tofauti; uwezekano wa kanisa kuacha maneno mengi na badala yake kufanya kwa upendo.

**Sisi tunaoishi na VVU kwa urahisi tunaweza kuwa wahanga na tukajiteketeza sisi wenyewe. Kama hatujiangalii sisi wenyewe na kutegemea kitu kutoka kwa watu wengine hatutategemea chochote kutoka kwa wengine. Tunachotakiwa kufanya ni kuweka wazi tunachotegemea miongoni mwetu na kusema nini tunataka. Sisi si masikini tuliokata tamaa tunaokataliwa tu sawa kama wengine. Tunahitaji kuheshimiwa kwa jinsi tulivyo na si zaidi. Ni suala rahisi la kuwa mwanadamu wa huruma ya kibinadamu.....wa upendo. Ni rahisi kuusema lakini unahitaji kujipenda mwenyewe kabla ya kupenda watu wengine. Kwa hiyo wale wanaotukataa na kwa hivyo hawatupendi wanasema "Sijipendi mimi mwenyewe".**

USHUHUDA WA RONNY ALIYEKUFA KWA UKIMWI, DENMARK



VVU na UKIMWI umekuja kama changamoto kwa kanisa – kilio ili kuangusha kuta, kuvuka mipaka, kuacha chuki. Kila mmoja ana kitu cha kujifunza kutoka katika mazungumzo, kwa mfano kuhusu raha, aina na wajibu unaohusika katika mapenzi. Utafutaji wa majibu kwa pamoja unatusaidia wote katika kusonga mbele, na tunayo mengi ya kushirikiana na wale wanaokabiliana na kifo.

## Changamoto yenye kutatiza

UKIMWI hutoa mwanga kwa vile ambavyo kwa kawaida havionekani – na hivyo pia katika kutokukubaliana kuliko-po katika makanisa na madhehebu yote. Baadhi ya Wabatisti, Walutheri Waanglikana, Wakatoliki na Waorthodox wanaweza kukubaliana kuwa ni muhimu wakahusishwa katika masuala ya UKIMWI – wakati wote wanapambana na vikwazo vigumu katika madhehebu yao. Ni muhimu kujaribu kukutana katika mipaka au vikwazo – na wakati huo huo kuchukua uhalali na swali la kiimani ambalo hutokea katika masuala ya UKIMWI.

Kila siku huleta maswali na changamoto mpya – ni muhimu kuweza kuangalia katika hamu yako mwenyewe na kusita katika macho, pamoja na kuwa na sababu na uwezo wa kukutana na watu wengine. Hakuna mwenye jibu la mwisho katika maswali yote yanayojitokeza juu ya VVU na UKIMWI. Hapa zaidi ya mazingira mengine, tunaona 'changamoto katika kioo' (1 Kor 13:12) UKIMWI ni kioo, fumbo, kwa ishara na dhahiri.

Wasiwasi na kujitenga hutokea ndani ya makanisa – na kuna kazi ngumu ya kushinda matengano. Yesu mwenyewe ndiye ambaye zaidi ya mwingine yeyote aliweza kuvunja vikwazo juu ya mateso na mifarakano – si dogo, kwa kuelewa maumivu ambayo daima yako katika kiini. Ndani ya kanisa leo tunahitaji kuangalia namna ambavyo Yesu katika njia zake aliwafikia si tu wagonjwa na waliotengwa na jamii, bali pia wale waliowadaharau na kuwakataa. Ukristo unahusika na changamoto ya kuchukua nafasi ya mtu mwingine na kuelewa sababu kwa nini watu hufanya jinsi wapendavyo – watu wengine na sisi pia. Kama hatuelewi maumivu yanayotufanya tuonyeshe hisia kama tunavyofanya, matokeo yake ni uharibifu wa kupuuzwa – siyo tu kwa wengine, bali hata kwetu pia.Shutuma na kutojali ni sura mbili katika sarafu moja.

Mwanathiolojia wa Kijerumani Dorothee Solle katika mwaliko alivutia msimamo mkali, alipotambua maana tatu katika maneno 'Chukua msalaba wako na unifuate':

- Kuachana na kutochukua hatua au upande wowote.
- Kufanya visivyoonekana vionekane.
- Kuwa na maono ya pamoja.

Anasisitiza jinsi Kristo, katika hali zote alivyokuwa upande wa wenye shida.Katika hali hii kifo kimevuka uwezo wa mwanadamu, akimaanisha kuwa kufa katika maisha ambako kumewafunga baadhi ya makundi ya watu katika majukumu fulani: kama 'watenda dhambi', 'waliotengwa', 'waliotwezwa', 'wasiojali'. Kuachana na kutochukua hatua si kuona vitu kwa namna ambayo wale waliodharauliwa na kukataliwa wanavyoona, ila kufanya visivyoonekana vionekane – hii ni kusema, kutoa usiri mbali na mawazo na hisia ndani yetu ambazo zimezimwa, usiri ambao katika hali ya kawaida ya jamii kufikiri, inafanya mambo haya kuonekana 'hayafai', 'siyo hayafai kuyafikiri' na mwishowe ni 'ushetani', Ina maana kuona uthamani wa vitu vinavyoonekana havina thamani, vilivyo zimwa – na kujitahidi kuvionyesha vikubalike na kupewa haki ya kuishi. Hapa katika mfano wa mwisho ni maono – maono ambayo yanaweza kuleta yale yasiyoonekana na yaliyofichika katika mwanga ili macho yasiyoona yaone ulimwengu katika upya.

Mateso si mateso tu, ni nafasi kwa kile kilicho kipya kimsingi, kwa badiliko maalum. Kuteseka ni nafasi ya kupambana, kwa maono ya maisha tofauti na mazuri. Hapa mategemeo na matumaini ya UKIMWI yamelala – siyo katika moja bali katika ngazi nyingi.



Neema, Upendo na Huruma

# Sura Za Mungu

MADA, MAJADILIANO, KUNDI LA NORDIC-FOCCISA, LUSAKA, 2004

Tangu mwanzo wa maradhi ya UKIMWI kuanza, watu wengi wameyachukulia kama adhabu kutoka kwa Mungu. Tafsiri hii ina maanisha Mungu mwenye kuhukumu na kuadhibu. Hatimaye, sura hii ya Mungu inachochea unyanyapaa na ubaguzi wa watu walioathiriwa au kuathirika kwa ugonjwa. Zaidi ya hayo, sura hii ina madhara kwa watu waishio na VVU na UKIMWI.

Katika uchunguzi wa mwanadamu ili kuelewa mateso yanayosababishwa na VVU na UKIMWI, mara nyingi watu huelekea katika kuonyesha sura mbaya za Mungu. Sura ambazo wakati mwingine huchochewa na mafundisho ya makanisa. Sura hizi za Mungu ni pamoja na hizi zifuatazo:

- Mlipa kisasi – kutokana na mwanadamu kutoelewa haki yenye uungu.
- Mtunza kumbukumbu za makosa yetu asiyeyumbishwa.
- Katili mbabe anayefurahia mateso yetu.
- Nguvu iliyokwisha amua mwisho wa kila kitu.
- Mungu wa tofauti asiyejali mateso ya wanadamu.

Kanisa linatakiwa kutangaza na kufundisha taswira halisi za Mungu katika mapambano yake dhidi ya unyanyapaa, ubaguzi na hali yakujisikia hukumu na aibu. Kwa pamoja ndani ya Agano la Kale na Jipya kura sura kadhaa za Mungu. Kwa ajili ya somo letu tutaangalia hizi zifuatazo:

## Kutoka Agano la Kale

**Mungu kama Muumba:** Mungu aliumba vitu vyote kwa uzuri na akafurahia uumbaji wake mwenyewe. Akamuumba mwanadamu mwenye uchaji na wa ajabu kwa sura yake mwenyewe. Sura ya Mungu ndani ya watu walioathirika kwa VVU haiharibiki.

**Mungu kama Emmanueli:** Mungu pamoja nasi: Tunaposoma mateso ya Ayubu, inakuwa wazi kwetu kwamba mateso yale hayakusababishwa na dhambi kwa upande wake. Biblia inasema hakuwa mtu wa kulaumiwa, alikuwamtu mkamilifu aliye mchaji wa Mungu na kuepuka uovu. Hakuna muunganiko wa matendo yake na hasara aliyoipata. Kwa hiyo hakuna sababu yoyote ya kuunganisha aina yoyote ya ugonjwa na hatia. Magonjwa si sehemu ya mpango wa Mungu kwetu – wala kama adhabu au majaribu.

Inaonekana kama Mungu alimwacha Ayubu, Lakini Ayubu alisisitiza katika uwepo wa uungu wake. Mungu yupo pamoja na Ayubu katika kipindi chote cha mateso – kama nguvu sikivu na angalifu ambayo inamrehemu mwishowe. Mungu yu pamoja nasi hata tunapojisikia tumetelekezwa.

## Kutoka Agano Jipya

**Mungu aliyejaa neema:** Katika fumbo (mfano) la mwana mpotevu (Luka 15:11-32) tunaona sura ya Mungu ikionyeshwa katika matendo ya baba. Anaonyesha upendo, rehema, uvumilivu, huruma na furaha kwa kurudi kijana wake. Ndani yake tunaona sura ya Mungu anayetukimbilia, mwenye hamu ya kukutana nasi popote tulipo. Kwa hakika, ana hamu kubwa ya kukutana nasi " hata akamtoa mwanaye wa pekee ili kila amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

**Mungu anayeteseka:** Wakati wa kusulubishwa tunaona sura ya Mungu ambaye anaweza kudhuriwa, asiye salama na anayeteseka. Hana nguvu na kuna nguvu ndani ya kutokuwa na nguvu kwake. Katika ufufuo, nguvu inaonekana na anatoa matumaini kwa wale walio katika mateso na maumivu. Ni Mungu anayestahimili pamoja nasi.

Mshikamano wake unaonekana katika hadithi ya safari ya Emmaus. Hapa tunaona mfano wa Mungu kama rafiki. Hii kwa karibu inafanana na Mungu kama Emanuel ( rejea katika hadithi ya Ayubu). Hakika, ni Mungu akiwa msalabani vilevile Mungu katika safari yetu yenye mashaka na huzuni. Kwa hiyo yuko nasi katika uzima na mauti.

**Mungu mponyaji:** Katika hadithi ya kumponya mtu aliyezaliwa kipofu (Yohana 9:1-12) tunaona sura ya Mungu anayekataa muungano wa hatia na majaliwa. Wakati wanafunzi wake walitaka sehemu ya kulaumu, Yesu aliwajibu waziwazi kwamba alikuwa kipofu ili nguvu ya Mungu iweze kudhihirishwa. Maandiko yanaonyesha (Mathayo 6:45) kwamba Mungu husababisha jua kuwaka kwa waovu na wema na hunyesha mvua kwa wenye haki na wasiohaki, akionyesha kuwa vitu vizuri hutokea kwa wasio wema na vibaya hutokea kwa wema – rejea habari ya Ayubu.

Maelezo mengi ya Biblia yanatuonyesha Mungu kama mponyaji. Inaweza kuwa hakuna dawa ya VVU na UKIMWI kwa sasa na bado Mungu anawaponya watu kwa kuwapatanisha na yeye na kila mmoja pamoja na ugonjwa. Mfano wa Mungu kama mponyaji unatusaidia kukubali ukweli wa ugonjwa na kumtegemea yeye.

**Mungu kama mtumishi:** Katika simulizi ya Yesu akiwaosha miguu wanafunzi wake (Yohana 13:1-17), tunaona mfano wa Mungu kama mtumishi mnyenyekevu. Mwana wa Mungu haogopi kupiga magoti na kutumika. Huo ni mfano bora kwa uongozi wa kanisa leo. Kumfuata kristo kwa kutoka na kuwafikia wenye shida, na hasa, kuwafikia watu waishio na VVU na UKIMWI.

**Mungu kama Msaidizi:** Kwa kawaida Mungu huwa upande wa wanyonge na maskini – alilionyesha hili ndani ya mwanae Yesu. Yesu daima huudhika na kujifanya mwenye haki na unafiki kwa sababu anapenda watu waishi maisha ya ukamilifu. Yesu anapowakosoa Mafarisayo na walimu wa sheria, anafanya hivyo kuonyesha namna mahusiano ya wanadamu yanavyoharibiwa kama tukihukumiana kwa sheria na tafsiri za kibinadamu juu ya nguvu za Mungu.

Kila mwanadamu ni mtoto mpendwa wa Mungu. Kwa hiyo ili tulielewe hili, Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kama Mponyaji na Msaidizi.

Mtazamo katika hadithi
mbili za kibiblia

NORWAY

# Utambulisho Wetu Mkuu ni Upendo

NA HELGE FISKNES

## Uumbaji

Mungu akasema,"'Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu...' Kwa hiyo Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu akawaumba; mwanaume na mwanamke akawaumba...Mungu akaona vyote alivyoviumba, na tazama, vinapendeza'". (Angalia Mwanzo 1).

Tunapendwa. Tumeumbwa kwa upendo.

Sisi ni sehemu ya ulimwengu uliodumu katika upendo. Utambulisho wetu mkuu ni upendo. Tu zaidi ya maneno na matendo yetu. Tunapendwa kuliko tujuavyo. Kwa nyakati tofauti tumesikia Mungu akinong'oneza katika masikio yetu, 'ni vizuri sana'. Tunaweza tusitambue kuwa ni sauti ya uungu, hata hivyo...Tumejisikia kuwapo kitu kizuri pamoja nasi. Tumekihisi ndani ya miili yetu, tumejinyoosha, tumejiachia kiwe nasi. Kinatutambua, kabla ya kingine chochote kututambua. Kimeleta tabasamu na kicheko.

Ni kama kuona watu wawili wapendanao wameketi katika kiti kirefu. Hawawezi kujizuia kushikana. Hawawezi kuacha kutazamana. Wanatabasamu na kucheka. Hawawezi kuacha. Katika sekunde moja hujiona wamekuwa hai zaidi ya ambavyo wamekuwa kabla.

Sisi tunaoangalia lazima tutabasamu pia – na tunasikia uchungu wa kupoteza. Wakati mwingine ni kukata tamaa. Upendo hutoa utambulisho muhimu tunaoweza kuupata. Miaka baadaye wasaa katika kiti kirefu unapotea. Ndani ya kumbukumbu zetu, kunatunzwa na kunaonekana wakati wa sherehe tu, kuna hisia kali za kutazama, hisia kali za kuwa uliishi.

Sisi ni hadithi iliyosimuliwa na Mungu. Nyuma na chini ya misingi iliyomo ndani yetu tunaelewa hivyo, vyote kumbukumbu tunazoweza kuzitoa na zile ambazo hatuwezi kuzifikia, kuna kiwango ambacho Mungu pekee anafahamu. Katika YEYE tunatakiwa kupenda vile visivyoenda katika vile vyote tulivyovitengeneza na vile ambavyo hatukuvitengeneza. Tunapendwa wakati wa kutungwa kwetu mimba. Tunapendwa tukiwa katika matumbo ya mama zetu. Tunapendwa wakati tunapoona mwanga wa siku kwa mara ya kwanza. Hakuna linalotokea litakaloondoa hili katika maisha yetu.

### Anguko

Walikuwa uchi, wote mwanamume na mke wake, lakini hawakuona aibu. Lakini mambo yakabadilika, na katika wasaa mfupi – kwa kula tunda lililokatazwa – tumetupwa katika ulimwengu tunaoufahamu kwa kina. Ambako ujasiri katika upendo na heshima vinapotea kila wakati.

Kwa njia ile ile kwamba wanadamu ni chanzo kisichoisha cha upendo, na pia ni chanzo kisichoisha kinachosababisha masumbufu. Tuseme wazi: Tunachagua kifo mara nyingi kama tunavyochagua uzima. Kila mmoja anafanya. Tunaishi katika mvutano wa uzuri na ubaya, kati ya uzima na mauti, kati ya kile kinachotunza uzima na kila kinachouharibu, kati



ya kile kinacholeta ushirika na kile kinachowatenganisha watu – au katika mtazamo wa dini: tunaishi kati ya Mungu na shetani. Hakuna hata mmoja anayeishi upande mmoja na hakuna anayeishi upande mwingine. Utashangaa pale utakapohisi sehemu yako ya juu iko katika utakaso – na unaweza kutahayari wakati ukigundua kuwa una sehemu za ushetani ndani yako.

Hatuwezi kusema kweli kuhusu mwanadamu mpaka sote tujione ni sehemu ya uungu unaoleta uzima na kinyume chake kile kinacholeta mauti.

Lakini utambulisho wetu mkuu ni upendo.

Vile vile, ni sehemu ya mateso, kujibidiisha na ulimwengu unaojeruhi. Ni watoto wa mito inayojitutumua na majanga ya asili, ya vita na vurugu, ya milipuko ya magonywa na njaa. Watoto wenye hasira (wabamizao milango) na kupandisha sauti, wasiotaka mapatano na wanaoharibu wengine. Uongo unafanya mema na mabaya kuwa fahari. Kwa mema na mabaya, tumefumwa pamoja na lazima tushiriki mwisho wa kila mmoja wetu. Kama vile tulivyofungwa kwa mema milele. Tumefungwa pia katika mabaya.

Lakini utambulisho wetu mkuu ni upendo. Wazo hili linatakiwa kuwekwa bayana.

Wakipambana na VVU, upendo ndicho kile wale walioathirika walikuwa wakikililia. Kulikuwa fedheha kuu. Ilitishia maisha. Virusi vimetishia maisha yao sana. Wameomba msaada kanisani. Wametaka kanisa lipunguze kasi ya maambukizi duniani, ili kwamba virusi vionekane jinsi vilivyo – bila ya kuambatanisha hukumu. Wametutaka kusimamia utu wa mwanadamu katika wakati ambapo wengi hawaujali.Lakini kanisa limejifungia, limefunga milango yake. Halikutambua jinsi ilivyo muhimu katika maisha ya ulimwengu. Halikuona mateso, bali 'uovu'.

Ni dhahiri tunahitaji uadilifu ili tuishi pamoja. Inatusaidia kuona upeo, kuchukuliana sisi kwa sisi. Wengine wamesema UKIMWI ni alama ya kushuka kwa uadilifu na upungufu wa uadilifu katika kujamiiana. Hii haiwezi kuwa uwongo, lakini ni makosa kuwafanya watu wenye UKIMWI kuwa ishara yake. Katika hilo hatuzungumzii kuhusu uadilifu bali tuna adilifya. Na kama vile uadilifu ni mzuri, uadilifyaji ni uovu. unawafanya baadhi ya watu kujiona ni bora kuliko wengine na unaweka alama kwa watu.

Biblia inasimulia hadithi ya Yesu. Ni dhahiri watu wengi walikuwa wakifurahia akiwa miongoni mwao. Ni kama imani zao zilikuwa zinaongezeka kwa kukutana naye. Alifufua imani zao katika utu wao. Wakati ambapo utu wa mwanadamu unaonekana una thamani kidogo, hii ni lazima iwe ni jukumu muhimu kwa kanisa leo. Kuongeza heshima ya mwanadamu kuwa ni viumbe wapendwa wa Mungu kama walivyo. Hii haihusiani na mahitaji ya mwili tu, bali ya kisaikolojia pia.

Kutambuliwa kama mwanadamu au kujitambua mwenyewe kama mwanadamu ni kuvumbua uzuri ndani yako. Utambulisho wetu mkuu ni upendo.

DENMARK

# Sura Za Kubuni Na Zile Zenye Kasoro

NA CARINA WØHLK

Katika miaka yangu nane ya ushauri wa kichungaji, kama kasisi kwa watu waishio na VVU na UKIMWI Denmark, nimekutana na zura ziharibuzo za Mungu na zetu wenyewe. Sura hizo ni:

1) Mungu kama hakimu – wanadamu kama wahalifu wa kuadhibiwa. Haki ndilo neno la msingi. Tuko katika mahakama. Sheria inatawala na Mamlaka inatumika.
2) Mungu kama dhalimu – wanadamu kama wahanga. Udhalimu ndilo neno la Msingi. Tuko katika chumba cha mateso. Hakuna sheria za kututawala. Mamlaka inatumiwa vibaya.

Katika mambo yote sura ya Mungu na sura zetu zinahusiana na dhana ya haki – pengine zilizounganishwa na haki au zinazopambana kinyume chake.

Katika Agano la Kale Mungu anajitambulisha mwenyewe kama: 'Niko ambaye Niko'. Na katika Agano Jipya anatuonyesha katika Kristo, sisi pia tunaweza kuwa kama tulivyo. Hiki ni kitu cha muhimu katika ukweli wa injili. Katika ushauri wangu wa kichungaji nimejaribu kuwatia moyo watu kukubali, badala ya, sura ya Mungu ambayo imelenga katika Kristo na sura binafsi ambayo ina asili yake katika injili ya kikristo, inayoelekea kuonyesha:

3. Mungu kama mpenzi – wanadamu kama wapendwa. Haki ndilo neno la msingi. Tupo wakati tuliofichwa katika uungu wake. Upendo na neema vinatawala. Kutotumia nguvu ndilo sharti la maisha.

## Mungu Kama Hakimu – Wanadamu kama Wahalifu Waliohukumiwa

Katika ufahamu wa watu wengi, Mungu ni mtendaji katika mfumo wa sheria. Wengi wetu tuna ufahamu mkubwa kuhusu haki. Tunaufikiria uhai kimsingi na kwamba kwa kawaida tunapata tunachostahili. Kwa maneno mengine tunaamini katika mahusiano yenye sababu, matokeo ya matendo yetu na yale yanayotokea kwetu. Tumeshawishika na madhara ya bumerangi – kwamba tunayotoa au kutenda ipo siku yatatturudia na kutudhuru. Na kama tulitenda vibaya itatugharimu – katika mfumo wa magonjwa, ajali au bahati mbaya. Wakati jambo baya linapotokea, tunalitafsiri kutokana na historia ya maisha yetu.

Katika huduma yangu ya kushauri, mara kwa mara ninakutana na watu wenye VVU/UKIMWI hasa wasenge wanaodhani wameshaambukizwa kwa sababu hawakujiheshimu. Wanaamini kuwa wana hatia kwa sababu ya makosa na ni lazima wateseke – kwa bahati mbaya wapo watu wengi wanaotaka kulazimisha yale wanayoaamini.

Ukweli ni kwamba tunakutana na ugumu katika kupambana na kutokuwepo na maana. Wakati mateso yasiyoelezeka yanapotupata, tunatafuta maelezo yanayotupa mtazamo unaoambatana na dunia inayoangamia.

Kujisikia hatia huumba mtazamo unaomaanisha uendawazimu. Hatujisikii kutokuwa na nguvu kwa yale yanayotupata. Sisi wenyewe tumehusika kwa sehemu kwa yale yanayotupata na tuna majukumu kwayo. Hatia huelekea hukumu na wengi wanaamini Mungu huwashughulikia wakosaji. Hukadiria uzito wa kosa na kutoa hukumu. Taswira hii ya Mungu na sisi inaonekana sahihi kwa sababu wote – Mungu na wanadamu wana nguvu. Tatizo kwamba vyote, chanzo na madhara ya maradhi lazima vichukuliwe kwa uzito wa hali ya juu pamoja na magonjwa mengine.

Mtazamo wa Mungu kama mhasibu na wanadamu kama hesabu za kujumlisha na kutoa katika kitabu chake ni badiliko katika jambo lile lile. Mungu huchukuliwa kuwa anajibu kwa ukali juu ya wale wanaopindisha hata jambo dogo kutoka njia nyembamba na iliyonyooka. Na ukweli halisi huchukuliwa kuwa wa haki na sahihi hivyo tunapata tunachostahili. Ni makosa yetu wenyewe.

Mtazamo huu juu ya haki chanzo chake ni katika thiolojia ya Agano la Kale. Katika Agano la Kale, wakati fulani Mungu anaonyeshwa kama mtawala mwenye wivu ambaye hawezi kuvumilia kutokuwa na imani. Wanadamu wanapokosa, hasiti kuangamiza uumbaji wake mwenyewe: mfano wake ni Gharika ambalo lilimfanya Mungu afikirie upya na kuahidi kutoangamiza tena kwa namna kama alivyoangamiza. Kuna matukio ya hukumu katika Agano Jipya: kwa mfano Mathayo 25, inayoeleza mfano wa wanawali kumi (wasindikizaji wa harusi) na utabiri juu ya hukumu ya mwisho.

Kimsingi Agano Jipya linaonyesha na kutoa sura tofauti ya Mungu, sura inayovuka mtazamo juu ya haki. Mfano mzuri wa hili ni hotuba ya mlimani (Mathayo 5): "Hufanya jua lake liwake kwa wema na waovu, na kunyesha mvua kwa wenye haki na wasiohaki" au mfano wa mwana mpotevu (Luka 15).

## Mungu Kama Dhalimu – Wanadamu kama Wahanga


Katika baadhi ya maongezi na watu wenye VVU nimekutana

na mitazamo juu ya Mungu na uelewa wao juu ya Mungu uliojengeka katika uzoefu wa kutotendewa haki kwa namna maisha yao yalivyobadilika.

Mungu hachukuliwi kama mkali au mwenye shuruti, lakini mwenye haki, hakimu –hapana, anatazamwa kama katili na sisi wanadamu ni wahanga wa tabia yake ya kubadilikabadilika. Hutupiga bila mpangilio na katika hali tusiyostahili. Si wanadamu walio waovu! Bali Mungu! Hutuadhibu kwa kadiri anavyoona inafaa bila sababu ya msingi. Na tumehamishwa ghafla kutoka katika chumba cha mahakama kuliko na lugha zinazohitaji ushahidi mpaka kwenye chumba cha mateso. Mungu si mhusika katika mfumo wa sheria, bali mvunja sheria anayesikitisha. Sisi ni wahanga wa uendawazimu wake. Mungu aliyemtoa kafara mwanaye wa pekee msalabani lazima ni kichaa, au siyo? Kama yuko radhi kumtoa kafara mwanaye wa pekee, kwa nini asituwambe katika kuta pale anapojisikia kufanya hivyo? Mtazamo huu juu ya Mungu unahusika na mtazamo wetu sisi wenyewe unaotuacha katika hatari ya kudhurika. Kutokuelewa na upotevu wa uthabiti unaongoza siku.

Mfano juu ya hili ni C.S Lewis, 'Uchunguzi wa Huzuni', katika kitabu hiki, Lewis anamwonyesha Mungu kama mpasuaji anayejaribu wanadamu katika maabara – dunia. Wanadamu hawaadhibiwi kutokana na uovu wao; Mungu anaonyesha uovu wake mwenyewe kwa kuadhibu wanadamu wasio na ulinzi.

Nimekutana na sura hii ya Mungu binafsi na hasa kwa watumiaji wa dawa za kulevya walioathirika kwa VVU. Wana mtazamo juu ya kuachwa na kuwa katika hatari. Na katika hali ya unyonge wao Mungu amewatokea kama mtesaji.



## Mungu Kama Mpenzi – Wanadamu kama Wapendwa

Kama mshauri mchungaji wa watu wenye VVU, ni muhimu kwangu kutoa sahihisho la Kikristo kwa sura hizi za Mungu zinazoharibika.

Kuhusiana na hili ninaona ni vyema kuanzisha wazo la 'kutojihesabia haki'. Ninavyoliona, Mungu ni zaidi ya mitazamo yote ya haki. Mungu hapimi haki katika milimita. Anapenda – na hilo ndilo jambo tofauti la maana. Yeye ni Mpenzi (mpendwa). Anawapenda wanadamu – na upendo wake hautabadilika. Hili linadhibitika katika 2 Timotheo 2:13.

Mungu si mwenye mashaka wala kutokuwa na mashaka. Hataki kutuponda ponda, anataka kutujali sisi. Mfano wa Mungu kama Mpenzi inapatikana katika thiolojia ya mtetezi wa haki za wanawake. Mwanamke mwanathiolojia aitwaye Sallie McFague anatumia mfano wa Mungu kama mpenzi, pamoja na Mungu kama mama na rafiki, katika kitabu chake 'Mifano ya Mungu'.

Mtazamo wa mantiki hii unaonekana katika Yohana 15:13-15, ambapo Yesu anasema, 'Hakuna aliye na upendo mkuu kuliko huu, kuweka uhai wako kwa ajili ya rafiki yako. Ninyi ni rafiki zangu mkifanya yale ninayowaamuru. Siwaiti watumwa tena, kwa sababu mtumwa hajui afanyalo bwana wake; lakini nimewaita marafiki, kwa sababu nimefanya yajulikane kwenu yote niliyoyasikia kutoka kwa baba yangu'.

1 Yohana 4:17-18 inasisitiza kuwa 'hakuna woga katika upendo'. Upendo ni ujasiri na sura zenye hofu na kuogofya za Mungu na mtu lazima zifungamane na sura ya Mungu ambaye ni upendo. Wale wanaoamini katika Mungu wa Upendo, wanaona rahisi kulinda kujiona, hisia za kuwa unapendwa, hata pale matatizo yanapokupata.

Tunaweza pia kukubaliana nalo kwa pamoja: hakuna mpango wa chanzo na madhara kati ya hatia na matokeo yake. Maelezo ya Yohana 9:1-15 ya kuponywa kwa mtu aliyezaliwa akiwa kipofu yanasisitiza hili. Na tunalielewa vyema, kama tukipata wasaa kufikiri. Wakati mwingine huwa vyema kwa watu wabaya na vibaya kwa watu wema. Ukweli uko hivyo. Mungu hafungwi na sheria ya chanzo na madhara inayotawala upeo wa kufikiri kwa wanadamu. Mungu anatupenda kwa sababu hawezi kuacha kutupenda – si kwa sababu tunafanya jambo fulani kustahili kupendwa, si kwa sababu tumempa sababu ili atupende. Mungu ni pendo – na upendo hauwezi kuwa mwembamba na mgumu kama haki. Yuko pamoja nasi hata kama kila kitu kiko kinyume nasi.



Mawazo Uzoefu na
Mtazamo wa Watu Wanaoishi
au Walioathiriwa na VVU

NORWAY

# Maana Na Utambulisho

Kwa washiriki katika mikutano ya Wanorway, uzoefu wetu kuhusu Mungu umethibitika kuwa jambo muhimu kwa namna ambavyo hali ya VVU na fedheha inayoambatana nayo inavyochukuliwa. Majadiliano yetu yalijikita katika sura za Mungu kwa namna tulivyofundishwa katika miaka ya awali, sura za Mungu tulizonazo tukiwa watu wazima na zile tunazotamani kuwa nazo. Polepole ilikuwa wazi kuwa kuna mahusiano katika uelewa wetu juu ya ubinadamu na uelewa wetu juu ya Mungu. Namna tunavyojiona na tunavyowaona wengine katika mitazamo yetu ya Kikristo na kiimani, kwa kiasi kikubwa inategemea namna tunavyomuona Mungu.

Sura za Mungu kwetu inategemeana na uzoefu wetu juu ya wazazi wetu, makanisa na watu wengine katika mamlaka. Wakati wa majadiliano ikaonekana baadhi ya washiriki walikutana na Mungu mwenye hasira nyakati za awali. Mungu aliye mwema kwa wengine lakini mwenye hasira kwa wengine; Mungu mwenye sura mbili anayewaweka baadhi ya watu 'ndani' na wengine 'nje'. Washiriki walihisi kuwa wakati tatizo la VVU au mambo mengine mabaya –yalipowapata, ilikuwa ni sura ya awali ya kitoto ya Mungu iliyojitokeza na kuchukua nafasi yake kuendesha mambo.

Kwa washiriki kwa jumla, nyakati za utoto, sura ya Mungu iliyotawala ilikuwa ni ile ya kutisha na sahihi ya Mungu: hakimu, mtunga sheria; ya ukali na mwalimu mwenye hasira na anayeadhibu matendo maovu, Mungu ambaye 'haeleweki', mwenye hasira hata ninapojaribu kutenda mema. "Wazazi wangu walimtumia Mungu kunitisha: 'Utakwenda jehanum usipotenda mema!', walisema. Kwa mtazamo Mungu alikuwa ni mtunga sheria, akitekeleza mlolongo wa sheria katika maeneo mbalimbali ya maisha hasa katika masuala ya kujamiiana.

'Nani alitenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, kwa kuzaliwa kipofu?' wanafunzi wake wakauliza (Yohana 9:12). Mungu huyu anapoadhibu, ni kwa sababu tumetenda dhambi, iwe tumefanya kwa makusudi au vinginevyo, kwa sababu Mungu huyu ni mhusika wa sheria ya kusababishwa/kusababisha na madhara. VVU ni adhabu kwa na ushahidi wa dhambi. Mungu huyu ni mwenye kigeugeu, hasira, anayeadhibu, anawajibika kuangalia unachokipata ni kile unachostahili, hata kama uamuzi usipoelekea kuwa wa haki.

Washiriki wawili walihusisha uzoefu wao wa awali kuhusu Mungu na mwitikio wao baada ya kupimwa VVU. Kama mmoja alivyosema, 'VVU vinahusiana na kujamiiana, lakini niliathirika kutokana na matunzo na upendo. Mwanzoni, nilimchukia Mungu kwa sababu ya VVU na niliona kama adhabu kutoka kwake. Wapi nilitoa wazo lile?' Mwingine alijibu: 'Sikustahili. Nilikuwa binti mzuri na niliamini kuwa Mungu yupo. Lakini mambo yalibadilika kwa sababu nilikuwa sifanyi vizuri shuleni na katika masomo yangu na sikuwa mwerevu. Lakini bado nilikuwa na mawasiliano na huyu Mungu anayehukumu. Na ndipo VVU vikaja, kama maumivu yanayotishia maisha na nikapata.'

Katika jibu la swali, 'Nani alitenda dhambi?' Jibu la Yesu lilikuwa, 'Si yeye wala wazazi wake.' Kwa washiriki hawa waw-

**Makanisa mengi yametambua kuwa ushahidi wa watu waishio na VVU/UKIMWI umetoa changamoto katika maisha yao. Wamelikumbusha kanisa kuwa inawezekana kukiri uzima hata pale unapopitia magonjwa ya hatari yasiyotibika na vikwazo mbalimbali, kwamba magonjwa na kifo siyo kanuni ambayo hupima uzima, kwamba ni hali au umaridadi wa uzima – kwa marefu yoyote- hilo ndilo muhimu. Shahidi wa namna hii anakaribisha kanisa kuitika kwa uangalizi wa upendo na uaminifu.**

JAPHET NDHLOVU

ili, na kwa ajili ya wengine wengi, VVU imekuwa sababisho la kuongezeka fikra kwamba Mungu haadhibu, Mungu anayehukumu katika utoto wao. Kama mmoja alivyosema:'Tangu nilipochagua kuwa wazi na kuongea kuhusu VVU, nimeiona njia ya kwenda kwa Mungu wangu na maana ya yale yaliyonipata na hiki kilichofanyika kwangu.' Au kama mwingine alivyoliweka, ' Nilikubaliana na hali yangu, niliwekwa huru na mashutumu. Kama wengine hawawezi kunikubali, basi hayo ni matatizo yao. Na hapo ni pale nilipoanza kutafuta sura yangu mwenyewe ya Mungu.' 'Siyo Mungu anayegeuza VVU kuwa adhabu, ni watu,' alithibitisha mshiriki mwingine.

## Kuanza Upya tena

Hata hivyo, kwa watu wengi wenye VVU mpango wa kujiondoa katika kuona sura hizi za awali za Mungu umekuwa mgumu, wenye maumivu na upweke. ' Uelewa wangu kuhusu Mungu ulibadilika kwa sababu ya haja ya kukubali VVU na kuogopa kutoa uhai wangu. Lakini ilinilazimu kuanza upya tena, kuanzia mwanzoni, pamoja na watu walionikubali. Nilijilazimisha mimi mwenyewe kujiona kuwa bado ni wa thamani, kwamba ninastahili upole na urafiki kutoka kwa watu wengine. Ilikuwa ni muhimu kufuata njia hiyo kuliko kujidharau. Ilichukua muda mrefu, hasa kabla ya kuweza kuchukua ushirika mtakatifu.'

Ilikuwa inachanganya pia. Hizi sura hasi (za kukatisha tamaa) zinatoka wapi na zina nini – kama tukienda mbali zaidi - tunaweza kuzibadilisha? 'kwa hiyo wapi tunampata Mungu? Kwa kutii amri? Hatuwezi kumkamata Mungu: Mungu hatendi kazi pamoja na "u - ndani" na "u – nje" ambapo pengine yupo au hayupo. Labda pengine ni sisi wanadamu tunaotaka kumtawala Mungu na tumtumie kujihalalishia nguvu zetu na tabia zetu.' Na bado wakati wote Mungu 'mwingine' anatusubiri, akituita. 'kama mtu mzima nilielewa upya kuhusu Mungu aliye na sura moja tu. Nimemshuhudia Mungu akinitoa kutoka mahali nilipoishi bila kuwa naye na mahali nilipokuwa na taabu. Kwa hiyo inawezekana kutoka katika sura ya Mungu 'aliye na amri na mkali wa aina ya Agano la Kale' hadi sura mpya ya Mungu kama mwenye 'nguvu anayeleta uponyaji na ambaye Kwake uzima wote unapatikana.' Au kama mshiriki mwingine alivyoliweka, 'Nikiangalia nyuma, ninaweza kuona sasa kwamba Mungu alikuwapo kwa ajili yangu wakati wote.'

Washiriki katika vikundi vya majadiliano walionyesha kuwa watu wengi kati yao, wanaamini kuna imani juu ya mema na wanaamini kuwa 'Mungu wa kweli' ni Mungu mwema. "Mungu wangu" Kama alivyosema mshiriki mmoja, " ni tofauti na Mungu wa Kanisani": na baadhi yao wakakubali. 'Inanilazimu kufika katika sura ya Mungu wangu', akasema mshiriki huyu; 'Mungu anayependa, asiyehukumu na anayenisaidia kutoka katika kuhukumiwa.' Washiriki kadhaa wakasisitiza umbali na upweke wa safari kwenda – au kurudi kwa 'Mungu mwema'. Kama mtu mmoja alivyosema, 'ilikuwa katika kusoma kwangu mwenyewe Agano jipya iliyonipeleka katika uamuzi kuwa Mungu niliyempata humo alikuwa ni tofauti na Mungu anayeletwa katika maombi na mahubiri ninayosikia kanisani. Na baada ya hapo ibada za kanisani hazikuniumiza tena'. Au kama mwingine alivyohitimisha 'Ilibidi nifanye kazi mimi mwenyewe kubadilisha picha ya Mungu niliyekuwa naye. Ilinilazimu nisitishe mtazamo wangu kwa wengine ya matarajio na kurudi nyuma. Mwishoni, ilinilazimu kumtafuta Mungu ndani yangu, kutafuta ukweli wangu mwenyewe na kusimama katika huo.'

**Injili na Imani ya Ukristo vinaachana katika mahusiano kati ya chanzo na sababu. Wokovu wa Mungu ni jambo la kupokea kile ambacho mtu hastahili. Hii ni kanuni ya neema. Kanisa lazima liwe la kwanza kupinga mtazamo kwamba kuna waovu na wenye haki walio na VVU.**

KUTOKA KWA MTAZAMO WA KINORWAY

## Mungu Mponyaji Mwenye Upendo

Kwa hiyo nini? Halafu nini tabia ya huyu Mungu apendaye, aponyaye ambaye ni lengo la safari yetu na barabara tunayoipitia? Na inatugharimu nini kuondoa sura ya Mungu mwenye hasira anayetukataa? Kwani Mungu huyu anayetupenda na kutujali siyo salama, anaweza kudhuriwa, kila wakati akigongwagongwa siyo tu na uzoefu lakini na uzoefu wa watu walio katika taasisi kanisa. Washiriki wengi walisema kwamba wanaweza kuandaa mkutano na vikundi au watu maalum watumishi na makasisi wa kanisa – ili waweze kupata badiliko hasa katika mtazamo wao juu ya sura ya Mungu. Waligundua jamii, ndani ya kanisa, ambamo Mungu mwenye upendo, anayejali ameanza kuonekana dhahiri kuliko Mungu mwenye hasira. Kwa washiriki wengi imekuwa ni ajabu kugundua mabadiliko makubwa ya Ukristo wao na injili. Kama mshiriki mmoja alivyosema, 'Injili inasisitiza umuhimu wa kujipenda na kupenda jirani yako.' Au kama mwingine alivyosema, 'Wanaweza kuwa vyombo ya ajabu kwa ajili ya maisha, kuwekwa huru; kuoshwa na kusafishwa kutoka kwa kila kitu kinachoweza kumpeleka mtu chini; kutolewa katika mtazamo wa kuvunjwavunjwa kwa mwanadamu na kwa vitu vinavyosababisha hatia na aibu!'

Ni katika kutafuta uponyaji huu, kusafishwa, sura za ukombozi za Mungu tulizoangalia, katika kukutana kwetu mara ya kwanza, katika maandiko ndani ya Injili ya Luka 13:10-17, tunapokutana na hadithi ya Yesu akimponya mwanamke mlemavu siku ya sabato. Katika majadiliano ya baadaye, hadithi hii ilileta maana ya tofauti kwa kikundi. Ukweli kwamba Yesu aliponya siku ya sabato inathibitisha umuhimu wa kuelewa moja kati ya sifa muhimu za Mungu. Hapa tunakutana na sura ya Mungu anayepingana na mamlaka na kufungua vifungo kwa wale waliofungwa. ' Ni Mungu ambaye hafungui kwa ajili ya shughuli kuanzia saa tatu mpaka saa kumi na moja, lakini ni nguvu isiyo na kikomo.' Katika hadithi hii tunamwona Mungu akivunja sheria za maandiko 'kwa sababu Mungu aliweka watu na huruma juu ya sheria. Yesu alichomaanisha ni kwamba lengo la sheria ni muhimu sana kuliko uaminifu kwa sheria binafsi'. Au kama mshiriki mmoja alivyosema, ni asili ya Mungu kupenda, na lengo na maneno na matendo yake ni kulegeza vifungo, kuwanyenyua wanaoonea, kuwaweka watu huru, kuponya na kuokoa.'

## Kuwa Mwanadamu – Bila kusahau kuwa unaishi na wanadamu wengine – inahusishwa na kujisikia Hatia

NA CARINA WØHLK

Dhamira ya muhimu katika huduma yangu ya kushauri ni hatia. Watu wengi waishio na VVU/UKIMWI hawajisikii kusumbuka kwa sababu wameshindwa kuwajibika . Wanapambana na hatia isiyo halisi – hisia yenye nguvu, ya uharibifu iliyojengeka katika hitaji la kuchukua na kutawala maisha yao wenyewe.

Ni jambo muhimu sana kutofautisha kati ya hatia ya kweli na bandia. Hatia halisi hufungamana na ukweli kuwa wote tunayo kwa sababu ni wanadamu, kwamba tunashikilia maisha yetu wenyewe mikononi mwetu. Hatia halisi tunayoishi nayo ni jambo ambalo lazima tulikubali na tujifunze kuishi nalo. Hatuwezi kuendelea katika maisha bila kujisikia kuwa na hatia – kwa maneno yanayoumiza, magomvi yasiyo na sababu, ujinga wa kutotenda mambo au pengine kitu ambacho ni kibaya zaidi.

Tofauti na hatia halisi, hatia bandia si sehemu ya maisha halisi ya mwanadamu. Badala yake, ni hali ya kuudhi, uzito wa ndani unaotuzamisha – kwa sababu hatia bandia inahusika na mtu kujichukulia maamuzi zaidi ya ambavyo anapaswa kufanya. Mzigo unakuwa mzito sana. Na unakuwa mahali pasipostahili. Ni lazima kuutoa.



DENMARK

# Hatia na Msamaha

Watu wengi wenye VVU huambiwa kuwa hali walizonazo ni kwa sababu ya makosa yao wenyewe. Sauti zisizo na upendo zinatafsiri kuwa VVU na UKIMWI ni adhabu kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watu wasioishi maisha yanayopendeza.

Kwa bahati mbaya, katika utofauti wao juu ya ukweli katika ulimwengu, watu walio na VVU wamejiingiza katika tafsiri hii mbaya. Hatia mbaya ambayo wanajisikia inatengeneza maana katika uendawazimu. Wanaweza kuona mahusiano kati ya chanzo na madhara, kati ya yale waliyofanya na yanayowapata. Udhaifu wao si matokeo ya makutano ya maangamizi yasiyo na mpangilio.Lakini, kuikumbatia tafsiri hii mbaya kunasababisha gharama kubwa, kuna madhara kwa sura za watu wenyewe na sura ya Mungu. Gharama juu ya fikra hizi za uongo kuhusu hatima yao ni kujitukuza kuliko na uharibifu. Kwa wale walioathirika, VVU si mtazamo wa Mungu juu ya kuonya kwa upendo lakini ni ushahidi wa wao wenyewe kutopendeka. Ni lazima waishi na sura yao wenyewe kama wenye aibu na hatia – na sura ya Mungu kama ahukumuye, bwana asiyesikiliza wala kupatana. Mateso yanaongezwa juu ya mateso.

## Uponyaji Halisi

Hatia halisi husababisha uhitaji wa msamaha, uhitaji wa kuweza kuishi bila hatia iliyofunika maisha ya mtu. Msamaha una maana ya kuendelea kuishi pamoja, kuwa pamoja na kuongea pamoja na mtu aliyekusababishia maumivu. Au msamaha una maana kuweza kuishi kama wewe mwenyewe – bila kujali chochote. Injili ya Ukristo ina mengi ya kusema kuhusu nguvu ya upendo katika uponyaji – pia pale maisha ya mtu yanapoonekana kuwa yamejeruhiwa na kuharibiwa kiasi cha kutotambulika. Msamaha mara zote hufika kwa wengine. Yesu Kristo amekuja kwetu, hii ina maana kuwa tunaweza kupatana na maisha yetu wenyewe na historia ya maisha ya watu wengine, hata kama ni waoga na wamekata tamaa kiasi gani.

Kama Wakristo ni wajibu wetu kuwa watumishi wa maisha na nuru. Hii ni kusema kuwa kumhuisha mgonjwa na kumuelimisha aliyedhulumiwa. VVU na UKIMWI husababisha kivuli cha mauti kwa maisha ya watu wengi. Uelewa mbaya kuhusu virusi umepofusha akili za wengi. Ni juu yetu kuondoa giza – pamoja na Bwana wa uzima.

Kujisikia aibu ni kujisikia hufai kwa upendo. Hisia ya aibu, najisi na uchafu vinaambatana. Mungu anatupatanishaje na ubinadamu wetu?



Kujisikia fedheha ni kujiona hustahili kupendwa.

Hisia za aibu, najisi na kutokuwa msafi zinaambatana.

Mungu anatupatanisha vipi na fikra zetu?

DENMARK

# Fedheha

NA CARINA WØHLK

Fedheha ni hali ya kuwa mtu usiyepaswa kuwa, ambapo hatia ni hali ya kujisikia baada ya kuwa umefanya jambo usilopaswa kufanya. Uelewa wa njia hii, fedheha kwa kweli ni ngumu zaidi kuishughulikia kuliko hatia, kwa sababu inahusika na utambulisho wetu si tabia peke yake.

Tunaweza kujisikia aibu kwa vitu vingi – magonjwa ya akili, ulevi, kujiua katika familia, ushoga au VVU. Aibu inatufanya tujisikie wabaya na kukemewa – na mazingira yetu yanachangia kujisikia hivyo. Kama una mfadhaiko, kama baba yako ni mlevi, kama kaka yako alijinyonga, kama kijana wako ni shoga, au binti yako ana VVU, basi hatari ipo, kwamba jamii inayokuzunguka itakufanya ujisikie aibu.

## Madoa na Alama ya Aibu

Kwa bahati mbaya, aibu ni kile unachokipata kutokana na hata kujiondoa kutoka katika maisha yaliyosawa na yanayopendeza. Aibu na najisi au uchafu vina uhusiano. Tunaongelea kuhusu 'doa' katika sifa ya mtu. Kwa Kidenmark mahusiano yako wazi zaidi: neno 'doa' katika mtazamo wetu ni 'alama ya aibu'. Lakini ulaghai wake ni kwamba aibu inajumuishwa katika jawabu la mateso ambayo watu wamejaribu na kuona ni lazima waishinde. Aibu au fedheha ni zaidi ya bugudha, zaidi ya kudharauliwa, haya (au staha), zaidi ya kuficha uso wako na kutamani ungezama ardhini. Aibu ni shambulio la heshima ya mtu na heshima ya mwanadamu.

Katika mila zetu aibu si kupoteza heshima bali ni kupoteza thamani. Wale wenye aibu hujisikia hawana thamani, thamani ya kupendwa, wanainamisha vichwa vyao badala ya kuviinua juu wakijiamini – na kumwamini Mungu aliyemfufua Yesu Kristo kutoka kwa wafu ili kufanya iwezekane kwetu kusimama wima katika pendo lake.

Katika maisha na mauti ya Kristo, Mungu alitupatanisha na hali zetu wenyewe. Hii ina maana kuwa tunaweza kuwa jinsi tulivyo – kwa mema au mabaya. Vyovyote tulivyo, chochote kinachotokea katika maisha yetu, Mungu yu pamoja nasi na anatupenda. Tuna heshima na uthamani unaotolewa na Mungu.

Kumbuka kuwa kuna vyumba vingi katika nyumba ya baba yetu. Tusisinyae kwa aibu, lazima tunyooke na kuwaangalia majirani zetu kwa ujasiri. Tusifiche yaliyomo ndani yetu, tujaribu kuwa wawazi. Tusijiruhusu kuvunjika mioyo, ni lazima tujijenge wenyewe kwa ujasiri katika uzima na maisha.

## Maumivu ya Petro

Aibu na uongo vina mahusiano ya karibu. Tunagundua hili tunapochunguza hadithi ya Mtume Petro katika Agano Jipya. Ni mfuasi wa kuaminiwa wa Yesu Kristo. Ni ambaye anapata bahati ya kuwa na Yesu katika Mlima ambapo Yesu alibadilika na anapewa jukumu la heshima la kuwa na funguo za ufalme wa mbinguni katika kabrasha la funguo zake. Ni wa kwanza kukiri kuwa Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu.

Pamoja na hayo, anakosa nguvu ya kumtia moyo Bwana wetu mambo yanapokuwa magumu. Yesu alikwisha mwandaa Petro kiakili kwa uwezekano kuwa angemkataa, lakini Petro alikataa tahadhari hiyo.

Lakini Yesu alipokamatwa na Petro akatishiwa, hiki ndicho kinatokea: anakataa kumfahamu Mungu na Bwana wake; anakataa kuwa hajawahi kuwa na uhusiano wowote na



**Siyo tu kwamba UKIMWI umepora watu kutoka katika familia zao, wapendwa na marafiki zao, UKIMWI umepora makanisa kumbukumbu ya Yesu mwenye huruma, masihi wa wanyonge, nabii aliye karibu na watu waliotengwa.**
JAPHET NDHLOVU

Yesu. Anavunja mahusiano na Yesu ili kuiponya ngozi yake. Anasema mambo ya uongo ili kujilinda.

Wakati ukweli wa maumivu unapomwingia Petro, wakati yale aliyomweleza Yesu yanapotimia, anapasuka kwa machozi. Yesu alikuwa sahihi, ni mtu wa namna hiyo – mnyonge ambaye hawezi kuwakubali marafiki zake. Anajishughulisha na uhai na usalama wake mwenyewe kuliko wa Yesu. Ukweli huu ulimjaza Petro simanzi. Anatoka nje na kulia kwa uchungu, kama biblia inavyosema. Machozi ya uchungu ni machozi ya aibu – na Petro anafanya kama ambavyo watu wengine hufanya wanapofedheheka: kujitenga peke yao.

Aibu inaweza kuja kutokana na kukataliwa na kufadhaika. Kwa sababu hatuna ujasiri wa kukubali namna tulivyo, kukubali historia ya maisha yetu wenyewe na tabia zetu. Au kwa sababu tunasahau kanuni na maadili yetu.

## Kuuficha ukweli unaoumiza

Ni aibu kuchuja au kuficha ukweli, na aibu inaweza kusababisha kujifanya na kujificha. Wale wanaoona haya kwa yale wasemayo au wanayotenda wanahitaji kuficha ukweli wenye maumivu. Wale wenye fedheha wanahitaji kujificha,

Ondosha aibu zote kichwani na weka maisha yako mikononi mwa Mungu! Hatakutupa chini. Anakupenda na atakushikilia – hata pale ambapo utajikinahi, hata wakati watu watakapokuchukia au watakapokusukumia mbali.

Pengine hauna ujasiri au uwezo wa kujisimamia mwenyewe. Lakini Mungu atasimama pamoja nawe – hatakuacha. Pengine unasikia aibu kwa chaguzi ulizofanya katika maisha yako. Lakini Mungu anakupenda kama ulivyo – bila chuki wala mashaka. Na hilo si la kuonea aibu......

Thiolojia inayofaa wakati

wa VVU Na UKIMWI

ZAMBIA

# Huruma yake Mungu



NA JAPHET NDHLOVU

Hali ya hatari ya ugonjwa unaoihuzunisha dunia na hadithi za kishujaa kuhusu mateso wanayopata wanadamu inahitaji mwitikio na mtazamo wa Kikristo. Hali ya hatari ya ugonjwa wa VVU/ UKIMWI ulio na tabia tofauti kupita matazamio ya ulimwengu na masikitiko makuu, ikiendana na mchanganyiko wa hatari wa nguvu ya mwanadamu katika kujamiiana na kifo. Ni kwa jinsi gani mchanganyiko huu unaathiri thiolojia, ni suala la matamanio kwa wale wanaojihusisha na thiolojia katika maisha yao.

Kanisa la Zambia limekumbwa na changamoto kubwa kutokana na maradhi ya VVU/UKIMWI. Hakuna thiolojia nje ya mahusiano na Mungu, kwa wale tu ambao wameunganisha maisha yao na mzingo wa desturi za Mungu wanaweza kuelewa kwa undani maisha ya mwanadamu. Imani inatafuta kujumuisha kile Mungu anataka kutoka kwa watu wake. Maradhi ya UKIMWI kipekee yanatuonyesha wakati muhimu na wa hatari, wasaa wa kweli , pamoja na wasaa wa neema na unaofaa – wakati wa kairosi.

Jamii ya kiimani zambia ambayo imekumbwa sana na VVU na UKIMWI inatakiwa kutafuta mfumo mbadala wa mageuzi ili kuendelea mbele.

Mungu muumba anahusika na hali ilivyo kwa sababu sura yake katika uumbaji imeguswa. Kwa asili na malengo (au ujumbe) yake, kanisa haliwezi kupuuzia wito kupambana na shutuma, chuki na udhalimu. Kanisa lazima liishi na kushuhudia hata nyakati hizi za UKIMWI. Wanadamu waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27) na kanisa lazime liwe mwili wake. Kristo ndiye kichwa cha mwili huu na wakati huohuo ni yeye, kwa kuwapo roho mtakatifu, analipa uhai.

Kukosekana kwa mtazamo wa kithiolojia nyakati za VVU/ UKIMWI hakika ni tanzia ambayo imelisumbua kanisa katika miongo miwili iliyopita. Linapokuja swali la changamoto ya VVU na UKIMWI, wana thiolojia wetu wamekuwa taratibu na kimya na makanisa yamenyamaza pia.

Thiolojia ni shughuli ya jamii kwa wote – wataalamu na wasio wataalamu; hukua katika maisha pamoja na watu wenye imani. Inakua kadiri watu wanavyoshirikiana kwa pamoja katika maisha na ufafanuzi wa matukio yanayowazunguka katika mtazamo wa kiimani.

Shauku juu ya thiolojia inawezekana kuongezeka nyakati hizi kwa sababu Wakristo wengi katika Zambia wameelimika kwa kiwango cha shahada ambapo wana ujasiri kuainisha mawazo yao na mitazamo thabiti katika kutafsiri maandiko.

Pamoja za hayo, tofauti miongoni mwa watu ni halisi – hata tofauti kithiolojia. Tunahitaji kukaribisha na kulea utajiri na hali mahususi ya mahusiano, historia na karama. Tofauti hizi pamoja na tofauti kwa namna watu wanavyomwona na kujihusisha na kumwelewa Mungu katika nyakati za VVU na UKIMWI, kwa namna ambavyo watu wanazingatia matendo kwa utashi na kimaadili na kwa namna ambavyo Mungu mmoja wa kweli anavyoabudiwa. Umoja wa kanisa la Kikristo daima umekuwa mundu katika Kristo. Tunahitajika kufanya mambo pamoja katika mbawa za uambatanisho wa Mungu.

Thiolojia daima imekuwa jambo lililo hai la jamii ya kiimani inayotafuta maana ya imani yao machoni mwa magumu katika maisha. Katika mpango huu, safari ya imani ya watu wengine na jamii, wote wale waliotangulia na wale ambao safari zao ni za sasa, ni wa muhimu sana. Thiolojia kama ilivyotolewa na – au ndani ya kanisa imetokana na majaribio magumu yenye maingiliano makali miongoni mwa maoni tofauti. Maoni haya yamekinzana sana mpaka kufikia makubaliano, na wakati mwingine maana mpya na pia kuingizwa kwa maana tofauti tofauti.

## Mapambano Kutambua Matakwa Ya Mungu

Watu wengi waishio na VVU/UKIMWI wanajitahidi kuelewa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya hali zao za sasa. Nafasi lazima zitengenezwe kwa watu wa kawaida kuandaliwa na wawezeshwe kufikiri mahusiano kati ya maisha yao ya kila siku na imani zao. Ni katika jamii za kiimani ndipo thiolojia hutokea, jinsi watu wa imani wanavyoshirikiana katika jamii uzoefu wao katika Mungu, ubinadamu na uumbaji.

Katika mchakato wa kuwa na mfumo wa thiolojia iliyo hai unaohusiana na maisha ya watu, hakuna mjuzi, mitazamo katika uzoefu huo huzalisha thiolojia iliyo hai. Kwa hiyo hii inatusaidia vipi sisi katika kutafuta mfumo wa thiolojia unaoendana na UKIMWI?

Kwanza, ni wale wanaoishi maisha ambayo mitazamo yake ndiyo msingi wa matokeo ya thiolojia inayoendana na maisha husika. Kusisitiza, kama Kanisa likitafuta thiolojia juu ya VVU na UKIMWI, linatakiwa kuwasikiliza wale wanaoishi na virusi, wale wanaowahudumia, pamoja na marafiki na familia zao. Kwa hakika waliokaribu na virusi ndio wanaotakiwa kuunda thiolojia juu ya UKIMWI. Hii ina maana kuwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI hawawezi kufukuzwa kutoka kanisani. Wao ndiyo rasilimali inayotakiwa kufanya jukumu la kutazama thiolojia.

Hapa ndipo mahali wanachama wa jamii hii ya watu wa Mungu, walioumbwa kwa mfano wake, wanapohusika katika msingi wa wito mkuu na tafsiri sahihi juu ya kuishi kwao na VVU. Kama wakipuuzwa, utajiri wa pendo la Mungu na neema umetolewa si tu kwao, bali pia kwa jamii yote ya kiimani.

Jamii ya Kikristo lazima iweke mazingira kwa watu wote wa Mungu kumtafuta Mungu, kumsifu Mungu, kuchunguza uzoefu wao kuhusu imani na kuangalia mitazamo ya thiolojia zao na uadilifu kama sehemu ya thiolojia, kuabudu na uadilifu wa jamii yote. Matengano kimatabaka yanaonyesha kukosekana kwa imani kwa Mungu na kukosekana kwa utambuzi juu ya upendo wa Mungu usio na mipaka.

Yesu alijihusisha katika kuvunja mipaka iliyowekwa kuwabagua watu kama wanawake, Wasamaria, wenye ukoma na wenye mapepo, Utaratibu huu umekuwa ni endelevu kwa jamii ya kiimani popote inapokuwa. Jamii ya kiimani mara nyingi imejikuta ikipambana na suala la kuhusisha na kuvunja mambo yanayowagawa watu kati yao wanapoelewa maono mapya ya Mungu katika kuwakubali watu wote.

Wenye imani wanatakiwa kujichunguza wao wenyewe katika uzoefu wao juu ya Mungu na siyo kuwahukumu wengine. Mambo mengi ya kimaadili yamezalishwa na wale ambao suala hili si sahii kibinafsi wala katika jamii zao, lakini ambao kimsingi wameweza kuweka kanuni ya mahusiano.

Maana hutokea katika hadithi za kila mmoja, familia na jamii yote iliyoteketezwa na woga, mateso na vifo vilivyotokea duniani kote kwa muongo mzima na zaidi. Kutambua changamoto halisi kwa thiolojia wakati wa UKIMWI, ni muhimu kusikiliza hadithi hizi, wasimulizi wake, watu waishio na VVU na UKIMWI wao wenyewe, walioathirika na VVU, familia zao, wenzi wao, wapenzi na waangalizi wao.

## Mateso ya Ayubu na Huruma ya Yesu

Kufanya mtazamo wa thiolojia nyakati hizi za VVU/UKIMWI lazima kuanza na Mungu kwa sababu vyote vilitengenezwa kwa mfano wa Mungu na kwa sababu kanisa, kwa asili yake lazima liwe chombo chake hapa duniani. Ni jambo linalokubalika kuwa maradhi hayasababishi maswali mapya kuhusu Mungu. Lakini angalau yanasababisha maswali kidogo ya kizamani kwa mapya – na kwa watu wa karibu wanaohusika –utaratibu mpya. Maswali juu ya mahusiano ya Mungu na mateso ni ya msingi tunapojadili VVU na UKIMWI. Maumivu makali kama hayo yanayosababishwa na VVU/UKIMWI yanaumba mtazamo kuwa Mungu hayupo.

Kitabu cha Ayubu (Ayubu 1-42) kinaweza kuchangia ukweli juu ya mtazamo kuhusu mahusiano kati ya mateso ya mwanadamu na uwepo wa nguvu za uungu. Mateso katika mwili wa Ayubu na majonzi katika akili yanaweza kuamsha hisia za maumivu kwa msomaji leo anayepambana na athari za VVU/UKIMWI.

Mapambano ya Ayubu na Mungu wa ajabu wa upepo uvumao unamwacha akiwa na hofu na mnyenyekevu mbele ya uwepo na nguvu ya Muumba wake. Ameshinda hoja zake. Dhambi zake si chanzo cha mateso yake na Mungu hamuadhibu kwa sababu ya dhambi hizo. Somo hili lazima lirudiwe kila wakati na kitabu cha Ayubu kisomwe kila wakati mbele ya Wakristo ambao bado wanafikiri mateso ya mwanadamu katika mtazamo wa adhabu kutoka kwa Mungu na kutokana na dhambi na kupata aina fulani ya mafundisho kuhusiana na VVU/UKIMWI.

Kama mafundisho ya kibiblia katika Agano jipya yanavyoonyesha, uwepo wa Mungu haukuwa kwa ajili ya wenye nguvu na utajiri, mara ya kwanza. Wenye dhambi na makahaba, maskini na waliotengwa walikaribishwa kwanza. Kwa kulitambua hilo, kwa kula na kunywa pamoja nao, Yesu alibadilisha kanuni zilizokubalika za kidini na heshima za kisiasa. Ilikuwa imgharimu maisha yake, kwa kuwa alionekana akipindua taratibu zilizowekwa. Baada ya onyesho la mashtaka alisulibiwa nje ya lango la mji, Yerusalem. Kwa Wakristo wanaohimiza kuwakataa, kuwakwepa na kuwapuuza watu waishio na VVU/UKIMWI mfano wa Yesu uwe ni ukumbusho wa lazima, kwa kusema: 'kadri mnavyowafanyia kati ya mdogo wa hawa...'

Tunakabiliana na fumbo la Mungu katika kushughulika na mambo muhimu katika uhai, hadi katika kiwango cha kuchukulia mateso na kifo cha mwanadamu katika hisia na kifo cha Yesu Kristo. Ufunuo muhimu sana wa mateso ya Mungu pamoja na wanadamu katika huruma ya Yesu, unadhihirisha mwelekeo mpya wa fumbo liitwalo upendo. Fumbo hili halitambuliki kirahisi, lakini linathibitisha uwepo wa Mungu.. Katika wakati wa kukata tamaa na maumivu Mungu yupo kupitia Yesu Kristo aliyekufa katika mwili uliodhaifu msalabani, uponyaji na ufufuo unafanyika. Upendo wa Mungu usio na ukomo hautelekezi wale ambao kwao kalvari ilifanyika mara ya kwanza. Mateso hubadilisha mtazamo na tabia ya mtu na unamwezesha mtu kushiriki katika uangalizi na uwepo wa Mungu.

Yesu hakutaka ushirika na waliotengwa kwa sababu ya urahisi wa kuwapata; alikuwa akianzisha mfumo mpya kimahusiano, aina fulani mpya ya jamii, Israeli mpya itakayopamba utawala wa Mungu alioutangaza. Katika jamii hii mpya, uwepo wa Mungu na nguvu zitaonekana juu ya vyote katika upendo. Na utakuwa upendo wa kweli, wa kuwalisha wenye njaa, kuwapa wafungwa uhuru wao, kuwafumbua vipofu, viwete kutembea, kuponya magonjwa yote. (Luka 4:16-18)

Huduma ya uponyaji ya Yesu Kristo imevutia vizazi vingi vya Wakristo. Kwa uwazi alipinga makosa ya marafiki wa Ayubu waliodhani Ayubu alikuwa na mateso kwa sababu ya dhambi: 'si mtu huyu wala wazazi wake aliyetenda dhambi;' aliwaambia wanafunzi wake juu ya mtu aliyezaliwa akiwa kipofu (Yohana 9). Katika mfano huu na mifano mingine, uponyaji unadhihirisha nguvu na utakatifu wa Mungu kwa kushughulikia mahitaji ya wagonjwa na waliotengwa.

Katika uangalizi wa Kikristo na maendeleo ya kisayansi ya mwanadamu, rasilimali hizi za kimungu (zinazotolewa na Mungu) zitumike kurejesha afya na matumaini ya wanaoteseka. Upendo baada ya namna ya Yesu, kukubalika bila masharti na uangalizi kwa mahitaji, lazima uelezwe kwa usahihi kadiri inavyowezekana. Hii inatakiwa ifanyike kitabibu, kijamii na kibinafsi katika huduma zote za kanisa.

## Tumaini

Imani ya Kikristo ni imani ya tumaini. Wakristo wanatiwa nguvu na tumaini hili kadiri wanavyopambana na maswali kuhusu mateso. Wanakiri kuwa mateso haya hayatoki kwa Mungu. Wanakiri kuwa Mungu yuko pamoja nao hata nyakati za ma-

**Kanisa kama mwili wa Kristo uwe ni mahali ambapo upendo na uponyaji wa Mungu unaonyeshwa na kutumika. Kanisa linalazimika kuingia katika mateso ya wengine, kusimama nao dhidi ya kutengwa na kukata tamaa. Kwa sababu ni mwili wa Kristo aliyekufa kwa ajili ya wote na anayeingia katika mshikamano na wale walioathiriwa na VVU/UKIMWI, Tumaini letu ni kwamba, ahadi ya Mungu ni hai na inaonekana kwa ulimwengu.**

JAPHET NDHLOVU

gonjwa na mateso, wakitumika katika uponyaji na wokovu katika 'bonde la uvuli wa mauti (Zaburi 23:4). Kupitia mateso ya Yesu Kristo msalabani uumbaji wote umekombolewa. Tumaini la Mkristo limejengwa katika uzoefu wa matendo ya Mungu ya wokovu katika Yesu Kristo, ndani ya maisha ya Kristo, kifo na ufufuo kutoka katika wafu.

Ukimchukulia Kristo kama mtumishi anayeteseka, Wakristo wameitwa kushiriki mateso ya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, wakijiweka wazi wao wenyewe katika mapambano haya katika hatari na mauti. Mwitikio wa wakristo na kanisa kwa wale walioathiriwa na kuathirika kwa VVU/UKIMWI unatakiwa kuwa wa upendo na mshikamano, ukielezwa na vyote- uangalizi na faraja kwa wale wanaoguswa moja kwa moja na ugonjwa na katika jitihada za kuzuia kusambaa kwake.

Wakristo wengi na makanisa wameonyesha upendo wa Kristo kwa walioathiriwa na kuathirika na VVU/UKIMWI, kwa bahati mbaya baadhi wamesaidia kunyanyapaa na kubaguliwa kwa watu hao, hivyo kuongeza maumivu ya mateso. Kikwazo kikuu cha kufikia malengo ya kuzuia VVU ni woga, kukataliwa na ujinga. Malengo ya tumaini, yakiendana na ufafanuzi wa kiroho na kimaadili kuhusu maana ya maisha baada ya kifo, unaotumia lugha ya kawaida ya watu, utaongeza maelezo juu ya njia mbadala za kuishi na VVU na UKIMWI. Mfumo wenye kujali wa kithiolojia utaendelea kuwa wazi kwa maswali na changamoto ambazo maradhi haya yameleta.







# Hitimisho

NA GILLIAN PATERSON

## Safari

Historia ya imani yetu imejaa safari nyingi: safari ya kwenda nchi ya ahadi, safari kama ya Mamajusi, safari ya kuelekea kwenye msalaba. Kuna hisia kuhusu safari hizi, majaliwa yanayotakiwa kufikiwa, wakati ambapo barabara ni giza na inachanganya na kusudi lake limegubikwa na usiri. Kuna hisia pia kuwa safari hizi zinafichua ukweli muhimu wa kusudi la Mungu kwa dunia, na maana ya msingi kuhusu vitu. Kuna ulazima hapa, pia: ulazima uliosababishwa na msukumo kuwa sasa (na siyo mwaka ujao, au miaka kumi kutoka sasa) ndiyo wakati safari zinatakiwa kufanywa. Nyota inayotuelekeza Bethlehemu haitasubiri.

Mchakato uliotoa kitabu hiki ulizaliwa katika hisia za haraka zinazofanana na hizo, hisia sawia kwamba hii ni safari ambayo ilitakiwa kufanyika. Ilitiwa msukumo kwa uelewa, miongoni mwa viongozi wa kanisa katika kusini mwa Afrika na nchi za ulaya kaskazini, kwamba fedheha (au shutuma) zinazofungamana na VVU na UKIMWI ni changamoto zinazotukaribisha kutafuta njia mpya za kuchunguza imani yetu, mahusiano yetu kibinadamu na aina ya jumuia ambayo kanisa limeitwa kuwa. Katika kuingia katika mchakato, jambo la lazima likawa kwamba makanisa ya kaskazini na ya kusini yafanye kwa pamoja: hatua yenye mashaka na ugumu, katika wakati ambao mahubiri juu ya UKIMWI yamejawa hasira, matengano na manufaa yenye mikinzano, kwa dini zenyewe kushutumiwa kuchangia katika mlipuko kutokana na asili tofauti ya jumuia zake na ujumbe kutokana na asili ya mahubiri yake.

Kwa kuwa UKIMWI umezalisha makundi yanayoelezeka, hasa kutokana na tofauti zilizopo kati ya mtazamo wa Kiafrika na ule wa nchi za kaskazini. Kwa mfano, miundo ya kitabibu ya magharibi juu ya mlipuko inayoonekana ikiwa bega kwa bega ikipambana pamoja na Waafrika ni ile iliyojikita katika mtazamo wa jumuia pekee. Ni mapambano yasiyo sawia, kwa kuwa Afrika inategemea magharibi kiuchumi na wataalamu wa sayansi kuhudumia mwitikio wake, taasisi za mawasiliano na uchapaji hutumia mitazamo ya kimagharibi na lugha za Ulaya kusambaza mawazo yao.

Kwa mtazamo wa kithiolojia, tofauti hasa zinaweza zisionekane. Kimtazamo wa kusini, Wakristo wa kaskazini wanaweza kuonekana kujitawala na binafsi, imani yao imepambwa na pengine maamuzi ya mkondo wa kulia au yenye msi-

mamo wa kiliberali. Watu wa Ulaya (kama wanajua lolote kuhusu dini katika Afrika) wanaweza wakachukulia kuwa urithi wa elimu kuhusu ulimwengu na jamii katika mila za kiafrika kama kitu kinachotakiwa kukomeshwa ili kuruhusu mahubiri ya dini na falsafa ya kisasa. Uigizaji wa namna hii unasababisha hasira na kufarakana: unahujumu mijadala ya muhimu; unajificha, kama virusi kati roho ya mijadala ya kimataifa kuhusu UKIMWI.

Lakini kanisa, kama utangulizi ulivyosema 'limeitwa kuwa tofauti'. Makusanyo haya ya mitazamo ni jawabu mojawapo la maamuzi: matokeo ya mchakato uliochukua miaka miwili wakati ambapo nchi za Nordic na mabaraza ya makanisa kusini mwa Afrika yalifanya kazi, yakiwa mbali na kwa pamoja, katika mambo matatu ya kithiolojia yaliyotokea katika sehemu hizi mbili (na kwingineko duniani) kama vichocheo vyenye nguvu vya unyanyapaa na ubaguzi.

## Zaidi ya Vikaragosi

Maandishi haya yanafanya nini, kwanza, ni kutoa changamoto kwa mambo yasiyo na asili yaliyoonyeshwa juu na kuyaweka katika mtazamo. Tunachokiona hapa ni vikundi vya wakristo na wana thiolojia binafsi wanaoingia katika mapambano ili kuonyesha imani zao kwa namna ya desturi zao: mapambano tuliyonayo, sisi sote, ni kutegemea kuwa makanisa yetu yatashirikiana.

Unyanyapaa umetengenezwa, kwa undani sana, katika mfumo wa jamii na katika mfumo ambao wanachama wake wanaona ni wa maana katika maisha yao. Kuukabili unyanyapaa kutaamsha hisia kali sana za ndani, lakini inaweza isiingie akilini, kwa kuwa unyanyapaa ni utumwa wa miiko. Miiko haina madhara kiundani. Kwa vingine, ni katika miiko yao, kwa kadiri ilivyojikita ndani ya jumuia na akili zao, kwamba jamii, taasisi au makundi ya kijamii yanajilinda kutokana na madhara, hatari na kutokana na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na tofauti au vinginevyo. Kiasili na kimaendeleo, dini imejishughulisha katika njia ambayo inaimarisha tamaduni za miiko, na kwa kufanya hivyo, kutoa maana na maelezo kiroho kwa desturi ambazo jamii inazifuata.

Hata kama, kwa sifa zote za msingi katika mila, zile ambazo zinaelekea katika kuwazia miiko ni zile zinazohusu kujamihiana, jinsia, asili, magonjwa, dhambi na mauti. Ni katika mambo haya ambapo masuala yote yanayohusu unyanyapaa kutokana na UKIMWI yamejikusanya. Kwa sababu hiyo dai lenye nguvu la Japhet Ndhlovu kuhusu uwiano katika jinsia katika desturi za Zambia, ikisisitizwa na kutambulika kwa tafsiri ya maandiko yanayoheshimika sana, na pia ikisisitizwa na hitaji la kuthamini kujamihiana kama zawadi inayotuwezesha kushiriki na Mungu, kazi ya uumbaji. Kwa sababu hiyo utambuzi wa Carina Wøhlk jwi ya unyanyapaa unaosababishwa na UKIMWi na hukumu na fedheha inayoambatana na kujamihiana, hasa katika vitendo vya kishoga na usagaji. Kwa sababu hiyo madai ya Elias Massicame kwamba waafrika wa Msumbiji unachukulia kujamihiana kama kitu kilicho nje ya mamlaka ya Mungu, na kutafuta kwa kukimbilia katika ukimya na hivyo kuwa wahanga wa vyombo vya habari vya magharibi vinavyohimiza uhuru katika kujamihiana. Ndiyo sababu ya nakshi ya Elizabeth Knox-Seth juu ya utamaduni wa kifo ambapo vijana wanahatarisha maisha yao ili kutimiza haja zao kimapenzi na katika hilo wanakatisha muunganiko kati ya mwanzo na mwisho wa maisha yao.

Tumependelea, katika kurasa hizi, kukutana na wakristo ambao, ili kuelezea unyanyapaa unaosababishwa na UKIMWI kwa ukweli – wamekuwa na ujasiri wa kuangalia maficho yao ya ndani sana katika nafsi zao na pia ndani kabisa mwa roho za jamii zao: au kama Carina wøhlk alivyoliweka, kukabiliana na 'Mimi Niko ambaye Niko' ili kwamba katika Kristo, tunaweza kuwa jinsi tulivyo.

## Mwili Mmoja

Inaweza kusemwa kuwa ukimya wa wakristo kuhusu mapenzi na kujamihiana umejengeka katika kuukataa mwili wenyewe na hapo ndipo ambapo tunatakiwa kusisitiza uangalifu wetu kitheolojia. Katika desturi na miiko za jumla zilizoelezwa mwanzo, mapenzi na kujamihiana, jinsia, asili, magonjwa,dhambi na mauti vyote ni vile ambavyo miili yetu hufanya. Inaonekana basi kuwa huwezi kuwa katika mwili bila ya kuhisi kitu fulani cha hatia na aibu kinachoambatana na mwiko: bila ya kufikiri kukihusisha na dhambi. Na bado ni katika mwili tunabebwa tumboni, tunazaliwa, tunaishi, tunapenda na kupendwa, tunaugua na kufa. Ni katika kuwa mwili, Neno lilikuwa mwili na damu. Ambalo lingeufanya kuwa si la kibiblia, zaidi tena kwa

Wakristo kupaka matope miili yao. Ni katika miili yetu na si katika majengo, wanadamu wakawa hekalu la Mungu. Ni katika ekaristi – karamu ya mwili na damu ya Kristo – inaonyesha kuingizwa au kutolewa katika jumuia ya kikristo. Na bado miiko ni jambo lenye nguvu sana na uwezo wetu kukubali ukweli wa neno kuwa mwili kumefichwa bado, ndani sana katika hisia gizani.

Uchunguzi wa wazo kuhusu mwili umekuwa ni kiini katika safari kama lilivyoelezwa katika kitabu hiki. Katika hatua binafsi, makundi ya watu wenye VVU waliokutana Norway waliongelea umuhimu wa imani inayokiri muunganisho wa roho na mwili. Katika Zambia Japhet Ndhlovu anaandika juu ya umuhimu wa kanisa kuanzisha huduma za uponyaji kama zilizounganisha mwili na roho: kuuona utakatifu kama tendo kuunganisha siyo hali ya kutengana; sura ya utakatifu kama 'inapakana' na 'haiko mbali' na uchafu.

Kama njia za kufanya kazi katika kanda zikiundwa, sura ya mwili wa Kristo kwa Mt. Paulo kama sitiari kwa kanisa duniani itakuwa dhahiri. Ni dhahiri kulikuwa na ugumu. Kwa mfano, uwazi wa kaskazini kuhusu matamanio ya kimapenzi kulitoa changamoto kwa makundi kutoka kusini. Vile vile umashuhuri wa dhana ya dhambi katika maandiko kutoka kusini ilithibitika kuwa ni ngumu kwa washiriki kutoka kaskazini.



Katika mitazamo iliyochunguzwa vizuri, ni rahisi kutafuta wasaa wa kukumbuka na kuandika: wakati asasi zilizojitandaza zaidi zinaweza kuona mradi huu ni wa kukaribisha japo ni wa nadharia, kama jani kavu la mwisho linalovunja mgongo wa ngamia. Haya ni mawazo halisi juu ya tofauti za uzoefu wetu, mambo ambayo kwayo utawala wa Mungu unaendelezwa. Lakini safari kwa mwendo wake, na kama kawaida inapoonekana ni vigumu kusonga mbele, huonekana vigumu zaidi kurudi nyuma.

Mwishoni, hakukuwa na kupinga kuhusu jina la kitabu 'Mwili Mmoja'. Kwa kuwa mwili ni mmoja na una wafuasi wengi na wafuasi wote wa mwili, japo ni wengi ni mwili mmoja, hivyo ni kuwa na Kristo. Na kama mfuasi mmoja akiteseka, wote wanateseka pamoja naye: kama mfuasi mmoja akitukuzwa wote wanafurahi pamoja naye. (1Koritho 12:12,26)

## Kuendelea Mbele

Kwa hiyo, wapi katika uzoefu wa wenye VVU/UKIMWI kuna Mungu?

Vikundi vya kaskazini pamoja na vya kusini vilimuongelea Mungu kama baba wa mwana mpotevu, aliyemtambua mwanaye mpendwa kwa mbali na akakimbia kwenda kukutana naye; na Mungu wa Kumbukumbu la Torati aliyetuchague si kwa sababu tulistahili, au wazuri kuliko watu wengine, lakini kwa sababu tulipendwa. Ni miongoni mwa tunaokataliwa na kujitenga sisi wenyewe na taasisi na tamaduni zetu kwamba Mungu amefunuliwa kwetu, nasi kuunganishwa na Kristo anayeteseka.

Na ufunuo ni utatu mtakatifu kwa tabia. Unatoa ujuzi, ukiturudisha kwenye Neno, na kutupeleka katika shughuli za Roho Mtakatifu. Ndipo ufunuo unakuwa sehemu ya mwaliko uliojaa neema kujihusisha na simulizi ambazo muktadha wake ni kuonyesha shauku ya utawala wa Mungu, lakini kwa kupitia njia ya mlango wetu wenyewe. Safari yetu wenyewe mwisho inakuwa ni sehemu ya safari ya kanisa, katika mtazamo wa uumbaji na simulizi za wafuasi wa Mungu.

Nilialikwa kuchukua sehemu katika safari hii, katika hatua za mwisho, kama mshauri na rafiki. Imekuwa ni faida na kwa hakika nimepata zaidi kuliko nilivyochangia. Katika makelele ya sauti zinazopinga zinazounda mazungumzo ya kimataifa juu ya VVU/UKIMWI, wasaa wangu wa ufunuo umekuwa neno moja la mpatanishi Kristo anayesafiri na wanaobaguliwa, akiwaalika wengine kujiunga katika safari. Ndani ya kitabu hiki, katika mkusanyiko wa maandiko, ni mwaliko ambao umeletwa kwako. Wewe msomaji.

# MwiliMmoja

Mwili Mmoja ilianzishwa kwa pamoja na Kikundi cha Kuweka Mikakati kilichokutana Lusaka 2004.
Kutoka Zambia: Japhet Ndlovu, Joy Lubinga, Munalula Akakulubelwa, Rose Malowa. Kutoka Msumbiji: Dinis Matsolo, Elias Massicame. Kutoka Norway: Jan Bjarne Sodal, Estrid Hessellund, Steinar Eraker. Kutoka Denmark: Carina Wøhlk, Birthe Juel christensen. Kutoka EHAIA: Sue Parry

**WALIOCHANGIA**

ZAMBIA

Rev Japhet Ndhlovu, Katibu Mkuu wa wa Baraza la Makanisa nchini Zambia. Akishirikiana na Duara za Tumaini

MSUMBIJI

Rev. Elias Zacarias Massicame, Mratibu wa Kitaifa wa VVU/UKIMWI katika Baraza la Makanisa Msumbiji akishirikiana na Rev. Dinis Matsolo, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Msumbiji na Bonaventura Zita, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Baraza la Makanisa Msumbiji

DENMARK

Rev. Birthe Juel Christensen, Afisa Habari, DanChurch Aid
Rev Carina Wøhlk, Baraza la UKIMWI la Kilutheri
Elizabeth Knox-Seith, Afisa jamii na tamaduni
Rev. Theodor Jørgensen, Professa wa Systematic Theology

NORWAY

Rev. Helge Fisknes, Oslo City Mission
Jan Bjane Sodal, Mratibu wa Miradi kuhusu VVU/UKIMWI Baraza la Kikristo Norway akishirikiana na watu waishio au walioathiriwa na VVU Oslo.

HITIMISHO

Gillian Paterson, Mwandishi na Mshauri wa Maendeleo, hasa katika mahusiano kati ya Thiolojia ya Ukristo na UKIMWI